**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA YA TUME KWA MWAKA 2015/2016

***Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,***
***S.L.P. 2643,***
***DAR ES SALAAM***
***Simu 0222135747/8***
***Nukushi: (022) 2111533/(022)2111281/(022) 2135226***
***Barua pepe:chragg@chragg.go.tz***
***Tovuti:*** *www.chragg.go.tz*

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Simu: 2110607 - 10, 2135747-8
Fax Na: 2111533/2111281.
Simu Pepe: chragg@chragg.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.JA 295/362/01

S.L.P. 2643,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

Mhe. Prof Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (MB),
Waziri wa Katiba na Sheria,
Jengo la Taaluma Na.1
Chuo Kikuu cha Dodoma,
Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 315,
**40404 DODOMA**

Mheshimiwa Waziri,

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 131 (3) (a) na (b) na Sheria Na. 7 ya mwaka 2001 kifungu cha 33 (1) (a), (b) na (c) kama kilivyorekebishwa kwenye marekebisho ya Sheria Na. 19 ya 2004, kwa heshima tunawasilisha kwako taarifa ya mwaka 2015/2016 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Taarifa hii inayojumuisha shughuli za Tume katika mwaka 2015/2016 na hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu inawasilishwa kwako kama Waziri anayesimamia haki za binadamu kwa ajili ya kuwasilishwa mbele ya Bunge. Aidha nakala ya taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali imeambatishwa pamoja na taarifa hii.

# SALAMU KUTOKA KWA MWENYEKITI



Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inayo heshima kutoa taarifa yake ya mwaka wa fedha wa 2015/2016, ambayo Tume imeratibu na kufuatilia matukio na hali halisi ya haki za binadamu nchini. Taarifa hii ya mwaka 2015/2016 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni ya 15 tangu kuanzishwa kwa Tume mnamo mwezi Julai mwaka 2001. Kwa mwaka huu wa 2015/2016 Tume imeendelea kukuza uelewa na kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kuhimiza uwepo wa viwango vinavyotakiwa kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Tume katika utekelezaji wa majukumu yake imebaini kuwa wananchi wanayo shauku ya kutaka kuelimishwa zaidi juu ya haki za binadamu, na misingi ya utawala bora. Uwepo wa haki hizo katika Katiba na mikataba ya Kimataifa peke yake haitoshelezi kuonesha iwapo haki za binadamu zinaheshimika Tanzania, kama Watanzania hatukuonesha kwa dhamira na vitendo vyetu kuheshimu haki hizo na misingi ya utawala bora.

Lengo kuu la uwepo wa utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora ni kupunguza pengo kati ya matamshi na dhamira zetu kuhusu haki za binadamu kwa upande mmoja, na matendo yetu katika shughuli zetu za kila siku. Kuwepo kwa Tume ni njia mojawapo ya kuthibitisha umuhimu uliowekwa kwenye suala la haki za binadamu nchini. Haki za binadamu zinalinda utu wa binadamu *(human dignity).* Misingi ya utawala bora imejikita kwenye nguzo kuu ya utawala wa sheria. Kwa hiyo jukumu la Tume ni kuhakikisha kuwa yote haya mawili yanatimia hapa Tanzania. Hata hivyo, katika kutimiza majukumu yake, Tume inashirikiana na kufanya kazi kwa pamoja na wananchi na wadau mbali mbali ikiwemo Serikali, Bunge na taasisi za kiraia za ndani na nje ya nchi.

Taarifa hii ya mwaka 2015/2016 inatoa tathmini ya namna Tume ilivyotekeleza majukumu kufikia malengo niliyoyataja hapo juu. Kwa kuelezea hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini, kazi za uchunguzi na ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora na mapendekezo ya Tume kuhusu masuala iliyoyashughulikia. Aidha, taarifa hii inaelezea namna Tume ilivyoshirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kutekeleza kazi zake.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Tume, taarifa inaonesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuinua viwango vya haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika nchi yetu. Taarifa hii ya kuanisha maeneo ambayo Tume imeona kulikuwa na uvunjifu na ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Kwa kupitia taarifa hii na nyinginezo zinazotolewa na Tume, natoa wito kwa wananchi kuitumia Tume ili kupata uelewa mpana wa haki zao na namna ya kuzidai zilizokiukwa na kutekeleza wajibu wao. Tume inatoa wito kwa viongozi wa Serikali, Mashirika ya Umma na watu binafsi kuendelea kushirikiana na Tume katika kukuza uelewa wa wananchi juu ya masuala ya haki zao na hivyo kuimarisha utawala wa sheria na demokrasia katika nchi yetu.

Ni matumaini yangu kuwa taarifa hii itaendelea kujenga uelewa zaidi wa kuifahamu Tume na kazi zake, pia na masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa ujumla wake hapa nchini na katika ngazi ya kimataifa.

Kwa heshima na taadhima nawasilisha taarifa hii kwenu na kuwatakieni usomaji mwema. Tume itashukuru kupata mrejesho.

Bahame Tom Mukirya Nyanduga
Mwenyekiti
**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACT | *Alliance for Change and Transparency* |
| ALAPA | Association for Law and Advocacy for Pastoralists |
| AOMA | *African Ombudsman and Mediators Association* |
| BVR | *Biomertic Voters Registration* |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CHAUMA | Chama Cha Umma |
| CHRAGG | *Commission for Human Rights and Good Governance* |
| CUF | *Civic United Front* |
| EAC | *East African Community* |
| EPZA | *The Export Processing Zones Authority* |
| GANHRI | *Global Alliance for National Human Rights Institutions* |
| GEPF | *Government Employees Pension Fund* |
| *GGM* | *Geita Gold Mining* |
| IJA | *Institute of Judicial Adminstration* |
| IWGIA | *The International Work Group for Indigenous Affairs* |
| LAPF | *Local Authorities Pension Fund* |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MKURABITA | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania |
| MOCLA | *Ministry of Constitution and Legal Affairs* |
| MoVET | *Ministry of Education and Vocation Training* |
| MTEF | *Medium Term Expenditure Framework* |
| *NANHRI* | *Network of African National Human Rights Institutions* |
| NEC | *National Electroral Commission* |
| NRA | *National Reconstruction Alliance* |
| NSSF | *National Social Security Fund* |
| OHCHR | *Office of High Commissioner for Human Rights* |
| PGO | *Police General Orders* |
| PPF | *Parastatal Pension Fund* |
| Prof. | *Professor* |
| PSPF | *Public Service Pension Fund* |

| | |
|---|---|
| R.E. | *Revised Edition* |
| SACCOS | *Savings and Credit Cooperative Society* |
| SADC | *Southern African Development cooperation* |
| SANAPA | *Saadani National Park* |
| SDGs | *Sustainable Development Goals* |
| SMS | *Short Message Service* |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SOSPA | *The Sexual Offences Special Provison Act* |
| SSRA | *The Social Security Regulatory Authority* |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANAPA | *Tanzania National Parks* |
| TBC | *Tanzania Broadicasting Corporation* |
| TCRA | *Tanzania Communication Regulatory Authority* |
| THBUB | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora |
| TKU | Tume ya Kudumu ya Uchunguzi |
| TV | Televisheni |
| UKAWA | Umoja wa Katiba ya Wananchi |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UPDP | *United People's Democratic Party* |
| UPR | *Universal Periodic Review* |
| UVCCM | Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi |
| WEO | *Ward Executive Officer* |
| ZAN ID | *Zanzibar Identity* |
| ZBC | *Zanzibar Broadicasting Corporation* |
| ZEC | *Zanzibar Electroral Commission* |
| ZSSF | *Zanzibar Social Security Fund* |

# YALIYOMO

SALAMU KUTOKA KWA MWENYEKITI ........ 3

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA ........ 4

VIFUPISHO ........ 4

YALIYOMO ........ 6

MUHTASARI WA TAARIFA ........ 9

SEHEMU YA PILI ........ **Error! Bookmark not defined.**

HALI YA HAKI ZA BINADAMU NCHINI NA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME KWA TANZANIA BARA ........ 16

SURA YA KWANZA ........ 17

1.0 MUUNDO NAMAJUKUMU YA TUME ........ 17

1.1 Historia ya Tume ........ 17

1.2 Uongozi wa Tume ........ 17

1.2.1 Makamishna na mgawanyo wa usimamizi wa maeneo kazi ........ 18

1.2.2 Katibu Mtendaji ........ 20

1.3 Ofisi za Tume ........ 21

1.4 Majukumu ya Tume ........ 21

1.4.1 Masuala ya Makundi ya Haki (Thematic issues) ........ 23

1.5 Malengo na Mipango ya Utekelezaji wa Kazi kwa Mwaka 2015/2016 ........ 24

1.5.1 Mpango mkakati wa Tume (2011/2012 – 2014/2015) ........ 24

1.5.2 Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013-2017) ........ 24

SURA YA PILI ........ 26

2.0 HIFADHI YA HAKI ZA BINADAMU NA MISINGI YA UTAWALA BORA NCHINI ........ 26

2.1 Haki za binadamu na utawala bora ........ 26
2.2 Haki ya usawa wa binadamu, na heshima ya utu ........ 27
2.2.1 Usawa mbele ya sheria na haki ya kutobaguliwa ........ 27
2.3 Haki ya Kuishi ........ 29
2.3.1 Vifo kutokea mikononi mwa Polisi ........ 29
2.3.2 Adhabu ya Kifo ........ 30
2.4 Haki ya uhuru wa mtu binafsi ........ 32
2.5 Haki ya faragha, usalama wa mtu ........ 33
2.6 Uhuru wa Mawazo, habari na mawasiliano ........ 35
2.7 Uhuru wa kukusanyika na kuungana katika vikundi mbalimbali ........ 36
2.8 Uhuru wa kushiriki shughuli za umma na utawala wa nchi ........ 37
2.8.1 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ........ 38
2.8.2 Uchaguzi mkuu wa 2015 ........ 39
2.9 Haki ya Kufanya kazi ........ 41
2.10 Haki ya kumiliki mali ........ 43
2.10.1 Matumizi mabaya ya madaraka katika mgawanyo wa umiliki wa ardhi ........ 43
2.10.2 Kutokuwepo kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi na uwekezaji ........ 44
2.10.3 Jamii kutokutimiza wajibu wake wa kulinda rasilimali za Taifa ........ 45
2.11 Wajibu wa jamii katika kulinda usalama na amani ........ 46
2.12 Hifadhi ya Haki za Makundi Maalum ........ 47
2.12.2 Haki za Wanawake ........ 47
2.12.3 Haki za Watoto ........ 49
2.12.4 Haki za wazee ........ 53
2.12.5 Hali ya haki za watu wanaoishi katika maisha ya asili ........ 55
SURA YA TATU ........ 60
3.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME ........ 60
3.1 Kupokea na kushughulikia malalamiko ........ 60
3.1.1 Utangulizi ........ 60
3.1.2 Malalamiko yaliyopokelewa na kuchunguzwa ........ 60
Chanzo; THBUB 2015/2016 ........ 61
3.2 Ufuatiliaji wa Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora. ........ 61
3.2.1 Migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi ........ 61

3.2.2 Uchunguzi wa lalamiko la bomoamoa uliofanyika Dar es Salaam ..... 69

3.2.3 Ufuatiliaji wa Hali za Wazee na Watu Wasiojiweza katika Makazi ya Wazee Nunge, Dar es Salaam 72

3.2.4 Utekelezaji wa haki za watu wenye ualbino ..... 75

3.3 Elimu, Mafunzo na Uhamasishaji kwa Umma ..... 77

3.3.1 Elimu kwa kutumia machapisho na vipindi vya redio na luninga ..... 78

3.3.2 Kushiriki katika Maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa ..... 78

3.3.3 Mafunzo ya haki za watu wanaoishi maisha ya asili ..... 82

3.3.4 Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa/Kikanda na Kitaifa ..... 85

3.3.5 Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa na Kikanda ..... 88

3.3.6 Taarifa ya Tathmini ya Hadhi ya Tume katika Umoja wa Mataifa ..... 92

3.4 Utoaji wa huduma za kisheria ..... 92

3.4. 1 Msaada wa sheria kwa wananchi ..... 92

3.4. 2 Mapitio ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa ..... 93

3.5 Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu ..... 94

3.5.1 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi ..... 94

3.6 Ziara ya Mhe. Rais Jakaya Kikwete Tume ..... 95

SEHEMU YA TATU ..... 97

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA, ZANZIBAR ..... 97

SURA YA NNE: ..... 98

4.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME ZANZIBAR ..... 98

4.1 Kupokea na kushughulikia malalamiko ..... 98

Chanzo; THBUB 2016 ..... 100

4.2 Kufuatilia uchaguzi Mkuu ..... 100

4.2.1 Uangalizi wa Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. ..... 100

4.2.2 Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu ..... 103

4.3 Ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar ..... 106

4.3.1 Hali ya Haki Wafungwa na mahabusu ..... 107

4.4 Tathmini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora baada ya Uchaguzi –wa marejeo ..... 112

4.5 Utoaji wa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora. ..... 114

SURA YA TANO ..... 115

5.0 CHANGAMOTO, MAPENDEKEZO NA MATARAJIO ..... 115

5.1 Changamoto ... 115
5.1.1 Ufinyu wa bajeti na changamoto zake ... 115
5.1.2 Ushirikiano kutoka kwa baadhi ya taasisi za umma ... 116
5.1.3 Upungufu wa Watumishi katika ofisi za Tume ... 116
5.1.4 Changamoto zinazoikumba ofisi mpya ya Pemba ... 116
5.2 Mikakati ya kukabili changamoto zilizojitokeza ... 116
*5.3* Mapendekezo ya kuboresha haki za binadamu na utawala bora nchini ... 116
5.3 Matarajio ya utekelezaji wa majukumu yaTume kwa mwaka 2016/2017 ... 117
Viambatanisho; A ... 119
Halmashauri wilaya ya Simanjiro ... 119
Shinyanga ... 121
**Ruvuma** ... 121
Halmashauri wilaya ya Nyasa ... 121
Halmashauri wilaya ya Kalambo ... 121
Halmashauri wilaya ya Rufiji ... 121
**Mjini Magharibi** ... 122
**Kaskazini Unguja** ... 122
Halmashauri wilaya ya Tarime ... 122
Micheweni ... 122
Wete ... 122
Chake chake ... 122
Mkoani ... 122
B; TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ... 123

# MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mwaka 2015/2016. Masuala yanayojadiliwa ni pamoja tathmini ya hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini, kazi za uchunguzi na ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora na mapendekezo yaliyotolewa na Tume kwa serikali na taasisi zake na wananchi kwa ujumla katika kuboresha haki za binadamu na utawala bora nchini.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zenye sura tano ambapo sehemu ya kwanza inaelezea muundo, wajibu na utekelezaji wa kazi za Tume Tanzania Bara, na sehemu ya pili inaelezea utekelezaji wa majukumu hayo Zanzibar na hitimisho na mapendekezo.

Sura ya kwanza inaitambulisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) kama idara huru ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa mwaka 2000 na Sheria ya Tume Sura ya 391 ya Sheria za Tanzania, rejea ya 2002) kuhamasisha, kulinda na kutetea hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Majukumu ya Tume yamefafanuliwa katika Ibara ya 130 ya Katiba na Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391. Dira ya Tume ni kujenga jamii inayozingatia haki na utamaduni, ambamo haki za binadamu na misingi ya utawala bora inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na inahifadhiwa nchini Tanzania. Dhima ya Tume ni kukuza na kulinda haki zote za binadamu, misingi ya utawala bora ili kudumisha demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora bila kuingiliwa na mtu au taasisi yeyote.

Kwa mujibu wa Sheria iliyotajwa hapo juu, Tume inaundwa na makamishina wasiopungua saba wakiongozwa na Mwenyekiti akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti .Shughuli za utendaji zinasimamiwa na Katibu Mtendaji akiwa na ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam (Makao Makuu) na Zanzibar na matawi katika mikoa ya Mwanza Lindi na Pemba. Ofisi hizi zimeanzishwa kwa ajili ya kuwafikia wananchi wengi zaidi

Katika mipango ya utekelezaji wa kazi zake, Tume inaongozwa na Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitano ambao umebeba malengo makuu ya kiutekelezaji yaliyo katika kazi katika Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) pamoja na Mpango Kazi (Action Plan) , a majukumu yake yaliyoainishwa ndani ya Katiba na sheria, MKUKUTA (nguzo ya Tatu), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 (Ibara ya 185 (f)), Malengo ya Milenia 2015, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 (lengo la (ii) na (iii), Maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (2030), na Mpango wa Umoja wa Afrika wa Maendeleo ya Afrika mwaka 2063. Aidha, katika utekelezaji wa majukumu yake Tume iliongozwa na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013-2017).

Sura ya pili inaelezea hali ya hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini kulingana na Ibara ya 131 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tanzania imeridhia na kutia saini mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ya kulinda haki za binadamu na kuitafsiri baadhi ya Haki katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kama nguzo za kusimamia haki za msingi za binadamu. Maelezo ya tathmini hii yamegawanywa katika makundi makuu ya haki za binadamu (haki za kiraia na kisiasa, haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na haki za makundi yenye mahitaji maalum). Haki hizo ni usawa wa binadamu, heshima ya utu, usawa mbele ya sheria, kutobaguliwa, haki ya kutoteswa na kutodhalilishwa, na haki ya kuishi.

Haki nyingine zilizojadiliwa ni ya uhuru wa mtu binafsi, haki ya faragha, usalama wa mtu, hifadhi ya nafsi na familia, uhuru wa mawazo, habari na mawasiliano, Uhuru wa kushiriki shughuli za umma na utawala wa nchi, kufanya kazi na kupata kipato halali, kumiliki mali na hifadhi ya haki za makundi maalum. Makundi maalum kwa mtazamo wa haki za binadamu, ni

makundi ambayo kwa sababu ya nafasi zao kijamii, kiuchumi au kimwili wanaweza kuwa waathiriwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu hivyo haki zake zinahitaji kupewa kipaumbele.

Taarifa inaonyesha kwamba hali ya haki za binadamu kiujumla ni nzuri pamoja na kuwepo kwa changamoto chache zilizoonekana kuathiri ustawi wa haki za binadamu na utawala bora nchini. Baadhi ya changamoto ni kama vile mauaji ya watu wenye ualbino na wazee, kuwepo kwa vifungu katika baadhi ya sheria vinavyoathiri haki za watoto na uhuru wa haki ya kupata taarifa, ubomoaji wa nyumba unaoathiri haki za kumiliki mali, faragha na utu wa watu. Changamoto nyingine zinaonekana katika eneo la utawala bora ni ukiukwaji sheria na taratibu unaofanywa na baadhi ya vyombo vya kutekeleza sheria.

Pamoja na tathmini hiyo, Tume imesisitiza kuwa haki inaendana na wajibu wa jamii kulinda na kutii Katiba na sheria za nchi, kukuza uchumi, na kulinda rasilimali za taifa na kuheshimu mali binafsi, kwa faida ya wote kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 25 hadi ya 28 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Hivyo, Taarifa hii inatoa ushauri kwa serikali na taasisi zake, kwa asasi za kiraia na kwa umma kwa ujumla kuzingatia Katiba, sheria, kanuni ili kulinda na kuendeleza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Sehemu ya pili inayoelezea juu ya utekelezaji wa kazi za Tume Tanzania Bara. Kupokea na kushughulikia malalamiko kwa mwaka 2015/2016, Tume ilipokea malalamiko 579, hivyo kuendelea kushughulikia malalamiko 7,913, ikiwa ni 7,334 yalitokuwepo na mapya yaliyopokelewa. Kati ya hayo malalamiko 1,106 yalihitimishwa na kufungwa hivyo kuwepo kwa malalamiko 6,807 yatakayoendelea kufanyiwa uchunguzi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Katika sehemu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, Tume ilifanya uchunguzi kutathmini migogoro ya ardhi na changamoto zake kwa Tanzania Bara. Katika eneo hilo, Tume ilifanya uchunguzi wa ubomoaji wa nyumba katika maeneo ya Bonde la Msimbazi katika Manispaa za Ilala na Kinondoni. Wananchi katika maeneo yaliyobomolewa walilalamika kufanyika kwa zoezi hilo bila kuzingatia haki zao. Uchunguzi huu uliwashirikisha wananchi katika kubaini aina za migogoro ya ardhi, vyanzo, athari zake na hatua zilizochukuliwa na kutoa mapendekezo ya kutatua migogoro hiyo.

Matokeo yanaonyesha kuwa matumizi mabaya ya madaraka, kutofuata au kusimamia sheria, kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kumesababisha migogogo ya ardhi nchini. Migogoro hiyo imesababisha vifo, na uharibifu wa mali, mazingira na kurudisha nyuma maendeleo katika maeneo ilikotokea. Hivyo Tume inatoa mapendekezo kwa Serikali juu ya uimarishaji wa usimamizi na matumizi ya ardhi.

Tume ilifanya ufuatiliaji wa haki za wazee kupitia mikutano na ukaguzi wa Makazi ya Wazee. Tume ilibaini kuwa hali ya haki za wazee umekumbwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuapata huduma zisizotosheleza za afya, umasikini, na kutokushirikishwa katika maamuzi ya nchi, hivyo ikatoa ushauri kwa serikali na wadau kuboresha haki za kundi hili.

Hali kadhalika, Tume ilifuatilia hali ya haki za watu wenye ualbino kwa kushirikiana na wadau wengine kuandaa mijadala kupanga mikakati ya kumaliza ukatili unaofanyia watu wenye ualbino. Aidha, ilishiriki katika maadhimisho ya siku ya kitaifa na kimataifa ya watu wenye ualbino kutoa mada kwenye warsha na matamko katika vyombo vya habari, kukagua sehemu

wanazoishi watoto wenye ualbino na kufanya mikutano na wadau mbali mbali kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kukomesha mauaji dhidi ya watu wenye ualbino.

Kwa mwaka huu pia, Tume ilifuatilia haki za watu wanaoishi maisha ya asili wanaoishi katika Vijiji vya Mongo wa Mono na Domango katika kata ya Yaeda Chini katika Wilaya ya Mbulu na Mang'ola katika wilaya ya Karatu. Tathimini hiyo iliongezewa na warsha za mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa Tume na wawakilishi kutoka katika wizara na idara za serikali zinazo simamia haki na ustawi wa watu wanaoishi maisha ya asili. Baadhi ya idara hizo ni Idara ya Ustawi wa Jamii Ofisi za Mkuu wilaya ya Mbulu, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa wilaya za Mbulu, Kiteto, Babati, Simanjiro na Hanang kutoka mkoa wa Manyara na wilaya za Karatu, Arusha Mjini, Monduli, Ngorongoro na Aru-meru kutoka mkoa wa Arusha.

Tathmini hiyo inaainisha changamoto za kutoa huduma na ustawi kwa jamii hizi, kama kutokutambulika rasmi kisheria, utamaduni wa kutokuwa na makazi ya kudumu na maeneo wanayoishi, ,imani yao kuhusu magonjwa na tiba, kubadilika kwa hali ya hewa, na uvamizi wa maeneo yao kutoka kwa jamii za kifugaji.Tume.. kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kwa makundi haya kwa kuzingatia kutengwa kwao na maisha yao ya asili ya kuhamahama, na kuendelea na kampeni za ushawishi na utetezi ili watu asilia watambuliwe rasmi.

Sehemu hii pia, inaelezea utekelezaji wa jukumu la Tume la kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa, (kifungu cha 6(1)(d) cha Katiba na Sheria ya Tume Tume iliandaa na kusambaza kwa umma machapisho mbalimbali ya habari, elimu na mawasiliano kwa kupitia mabango, majarida, vijitabu, vya elimu kwa umma. Makamishna na watumishi wa Tume walishiriki katika vipindi na mijadala iliyorushwa katika luninga na redio lengo likiwa kufikisha ujumbe kwa wananchi wengi zaidi.

Aidha, katika kutekeleza jukumu hilo, Tume ilishirikiana na wadau wengine wa kimataifa na kitaifa katika kutekeleza majukumu yake kama vile maadhimisho mbalimbali yakiwemo ya Siku ya Haki za Binadamu 10 Desemba, 2015, Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 16 – 23, 2016), Siku ya Watetezi wa Haki za Binadamu Duniani, Aprili 27, 2016) na Wiki ya Sheria Tanzania (Januari 30 – Februari 3, 2016) na Siku ya Haki za Binadamu ya Afrika ambayo huadhimishwa Barani Afrika kila mwaka tarehe 21 Oktoba. Kupitia shughuli hizi wananchi wengi zaidi walifikiwa na Tume na kunufaika na elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, pamoja na msaada wa kisheria uliokuwa ukitolewa.

Tume ilishirikiana na wizara, idara na taasisi mbalimbali za Serikali katika kuyapatia ufumbuzi malalamiko yaliyowasilishwa mbele yake. Pia ilihamasisha elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora na mafunzo juu ya masuala ya haki za binadamu na ufuatiliatiaji wa hali ya haki za binadamu nchini. Ushirikiano huu ulichangia Tume kutekeleza majukumu yake ya kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Aidha, Tume ilitoa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kugharamia huduma za mawakili. Huduma za msaada wa kisheria ulijumuisha msaada na ushauri wa kisheria, uwakilishi mbele ya vyombo vya kisheria, uwezeshaji wa kufikia vyombo vya kutoa haki, elimu ya sheria na usuluhishi wa migogoro.

Tume ilitoa huduma za ushauri kisheria kwa walalamikaji waliofika katika ofisi zake, Wananchi 2,903 walipokea ushauri wa kisheria kutoka kwa maafisa wa Tume, miongoni mwao, wananchi 210 walipata ushauri kuhusu masuala ya mirathi, 900 kuhusu migogoro ya kazi ikiwemo, kutopandishwa vyeo, kuachishwa kazi na mafao, 1750 kuhusu migogoro ya ardhi na 43 kuhusu masuala ya haki jinai ikiwemo utaratibu wa kukata rufaa.

Katika kipindi cha 2015/16, Tume iliendelea na utekelezaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu chini ya mradi wa "***Support for National Human Rights Priorities***" unaotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa ufadhili wa UNDP.

Mradi huu ulikuwa na kazi kuu tatu ambazo ni; kuwajengea wananchi uelewa wa masuala ya utekelezaji wa mpango kazi,ufuatiliaji wa upatikanaji wa haki, kuzijengea taasisi uwezo wa kiutendaji wa kufanya kazi kwa kuzingatia jicho la haki za binadamu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mpango kazi wa kitaifa wa haki za binadamu

Kwa kupitia mradi huu, Tume iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni za Paris-*(Paris Principles)* kwa Kamati ya Tathmini ya Hadhi za Tume za Haki za Binadamu Kimataifa ya Mtandao wa Tume za Haki za Binadamu Duniani (GANHRI) katika Ofisi ya Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa. Tathmini hii hufanyika kwa Tume zote za haki za binadamu kote ulimwenguni na taarifa huwasilishwa kwa Sekretarieti ya Mtandao wa Kidunia kwa Tume za Haki za Binadamu.

Sehemu ya pili yenye sura mbili inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Tume Zanzibar Sura ya nne, inaanza kuelezea ilifanya shughuli mbalimbali za kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Baadhi ya kazi zinazoelezewa ni pamoja na kupokea na kuchunguza malalamiko, kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, uangalizi wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 25, 2015 na ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar .

Kwa upande wa malalamiko, mwaka 2015/2016, Tume ilipokea na kushughulikia malalamiko mapya 20. Aidha, Tume iliendelea na uchunguzi wa malalamiko 162 yaliyopokelewa miaka iliyopita hivyo kufanya idadi ya malalamiko yaliyoshughulikiwa mwaka huo kufikia 182. Kati ya hayo, uchunguzi wa malalamiko 29 ulikamilika na kuhitimishwa. Hadi kufikia mwezi Juni, 2016 idadi ya malalamiko yaliyokuwa yanaendelea kushughulikiwa yalikuwa 153

Malalamiko yaliyopokelewa yalihusu kupigwa na kuteswa, ucheleweshaji upelelezi wa kesi, kubambikizwa kesi, kunyanyaswa, ucheleweshaji wa malipo kutoka hazina, kutotendewa haki, kuzuiwa kufanya kazi na madai mbali mbali. Baadhi ya taasisi zilizolalamikiwa ni pamoja Idara Maalum za SMZ, Jeshi la Polisi, Halmashauri za Wilaya, shehia, hazina, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, mamlaka ya viwanja vya ndege na watu binafsi.

Aidha, Tume ilifuatilia uchaguzi mkuu uliofanyika Octoba 2015 kwa upande wa Zanzibar kuanzia uandikishaji na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kampeni, upigaji kura na hali ilivyokuwa baada ya matokeo. Katika uchaguzi huo vyama vya siasa 14 vilisimamisha wagombea wa kiti cha Urais wa Zanzibar na 22 viliwania viti katika Bunge, Baraza la

Wawakilishi na Udiwani. Aidha, vyama vya CHADEMA, NCCR- Mageuzi, CUF na NLD vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) vilikubaliana kusimamisha mgombea mmoja kwenye uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wawakilishi na Masheha.

Taarifa inaonyesha kuwa mikutano ya kampeni na upigaji kura upigaji ulikuwa ni wa amani. Mapungufu yaliyotaarifiwa ni pamoja na baadhi ya mawakala wa vyama kukosa vitambulisho, matukio ya upigwaji wa watu katika baadhi ya vituo kisiwani Pemba kutokana na kuwepo kwa imani ya kuhofia kuibiwa kura na baadhi ya watu kushindwa kupiga kura kwakuwa hawakuandikishwa kwenye daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutokuwa na vitambulisho vya mzanzibar mkaazi. Hata hivyo matokeo ya uchaguzi yalifutwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) siku ya tatu baada ya upigaji kura. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, matokeo ya yalifutwa kutokana na "ukiukwaji na uvunjaji mkubwa wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.Tume ilitoa mapendekezo ya namna ya kuboresha kasoro au changamoto zilizojitokeza.

Tathmini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora baada ya Uchaguzi ilionyesha kuwepo kwa baadhi matukio ya uharibifu wa mali, mfarakano wa familia, migomo, hujuma, ubaguzi wa kiitikadi na kutoshirikiana katika shughuli za kijamii na huduma za kijamii. Matukio ya uhalifu na uharibifu wa mali, kama vile kukata mazao, na kuchoma moto nyumba

Tume inashauri kuchukuliwa kwa hatua za makusudi na haraka zifanyike kwa Viongozi wa Kitaifa na wa vyama vyote vya siasa vikiwemo CUF na CCM wakae pamoja kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa suluhisho la kudumu litakalozuia matatizo ya uvunjifu wa amani kujirejea. Ushauri pia, unatolewa kwa taasisi zinazosimamia ulinzi na usalama hususan vyombo vya dola ziwe makini katika kufanya kazi zake kwa kufuata misingi ya utawala bora, haki za binadamu na utawala wa sheria ili kuepukana na madhara yasiyotarajiwa katika jamii.

Aidha, Taarifa imejumuisha kwa ufupi taarifa ya tathmini ya haki za binadamu na ustawi iliyofanywa na Tume katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar. Tathimini hiyo inaonyesha kuwa, mapungufu katika upatikanaji wa haki za wanafunzi waliozuiwa katika vyuo vya mafunzo na ustawi wa watumishi wa vyuo hivyo. Uwepo wa matumizi ya mitondoo katika baadhi ya vyuo, kutokuwepo huduma ya usafiri, na afya na mazingira magumu ya kazi na ustawi wa watumishi ni kinyume na mikataba ya kimataifa na kikanda ya haki za binadamu pamoja na sheria za nchi zinazoelekeza uzingatiwaji wa haki za binadamu kwa watu waliozuiwa. Katika Taarifa hii inaambatana na mapendekezo ya kuboresha haki za askari, na wanafunzi na kukamilisha mashauri yao kwa wakati muafaka.

Taarifa pia, inaonyesha utekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa umma lilivyotekelezwa na Ofisi ya Tume Zanzibar.kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kushirikiana na wizara na idara za SMZ, shirika la habari la Zanzibar (ZBC), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) na Club ya Waandishi wa Habari Zanzibar, Kazi hii ilifanyika kwa njia ya vyombo vya habari, kongamano, semina na kutoa mada katika warsha zilizoandaliwa na taasisi nyingine kama vile haki za binadamu na utawala bora, wajibu wa jamii, Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, haki za watoto, mahabusu na wafungwa.

Aidha, Taarifa imeelezea kwa ufupi utekelezaji wa jukumu la Tume la kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wake na watumishi wa Wizara na Idara za Serikali ili kuongeza ufahamu na weledi. Mafunzo hayo yalihusu usuluhishi wa migogoro (Conflict Management), Usawa wa Kijinsia katika utoaji haki (‘*’Gender Equality in the Administration of Justice’’*), uangalizi wa mchakato wa uchaguzi na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu. Aidha, Tume iliendelea kushirikiana na taasisi na wadau mbalimbali katika masuala ya haki zabinadamu namisingi ya utawala bora kwa lengo la kuendeleza utulivu na amani.

Sura ya Tano inayoelezea juu ya changamoto zinazoikumba Tume katika utekelezaji majukumu yake, mapendekezo ya kuboresha changamoto hizo na matarajio ya kwa mwaka unaofuata. Changamoto zinazotaarifiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti ya Tume ukilinganisha na mahitaji yake na kinyume na matakwa ya kanuni za Paris (Paris Principles) zinazozitaka serikali husika kutenga bajeti za kutosha kwa taasisi za kitaifa za haki za binaadamu.

Ufinyu wa bajeti kumepunguza uwezo wa Tume kutekeleza jukumu lake la kulinda na kuhifadhi haki za binadamu nchini kwa viwango vinavyotakiwa. Kutokana na mapungufu hayo, Tume imeshindwa kuwafikia wananchi, kufuatilia mashauri, upungufu wa vitendea kazi na kushiriki katika mikutano muhimu ya kimataifa na kikanda ambayo Tume ni mwanachama.

Taarifa hiyo pia, inaonyesha mikakati ya Tume kukabili changamoto pamoja na mapendekezo ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Tume na haki za binadamu na utawala bora nchini.

Kuendelea kuiomba Serikali ili iweze kuongezewa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba na Kisheria.

- Tume inaomba wadau wa mendeleo kuongeza mchango wao kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Tume, Taaisi za kiserikali na za kiraia kuungana kwa pamoja na kuongeza kasi kutoa elimu ya haki na wajibu ili kudhibiti ukiukwaji wa misingi ya utawala bora miongoni mwa taasisi za umma,
- Kujenga uwezo kwa maafisa wawakilishi “*Focal Persons*” katika Wizara na Idara mbalimbali za Serikali ili kurahisisha mawasiliano kati ya Tume na taasisi hizo kuufanyia maboresho mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko Yanayofikishwa Tume.
- Tume inaishauri serikali kupitia sheria zake ili kuboresha haki za watoto, wazee, walemavu na watu wengine wenye mahitaji maalumu

Taarifa ina hitimisha kwa kuelezea matarajio ya utekelezaji wa majukumu yaTume kwa mwaka 2016/2017. Tume inatarajia kukamilisha malalamiko yanayoendelea na yatakayopokelewa, kutoa elimu ya umma kuhusu masuala ya haki za binadamu, wajibu kwa jamii na misingi ya utawala bora kwa wadau mbalimbali wa Tumekufanya utafiti kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora zinazolenga kuboresha maisha ya wananchi walio kwenye mazingira magumu katika jamii, na kuimarisha utendaji wake katika matawi na kuwepo kwa Vitendea kazi vya kutosha.

# SEHEMU YA PILI

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU NCHINI NA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME KWA TANZANIA BARA

# SURA YA KWANZA

# 1.0 MUUNDO NAMAJUKUMU YA TUME

## 1.1 Historia ya Tume

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni idara huru ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa mwaka 2000[1], na Sheria ya Tume Sura ya 391 ya Sheria za Tanzania, rejea ya 2002) kuhamasisha, kulinda na kutetea hifadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.. Majukumu ya Tume yamefafanuliwa katika Ibara ya 130 ya Katiba na Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391. Dira ya Tume ni ***kujenga jamii inayozingatia haki na utamaduni, ambamo haki za binadamu na misingi ya utawala bora inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na inahifadhiwa nchini Tanzania. Dhima ya Tume ni kukuza na kulinda haki zote za binadamu, misingi ya utawala bora ili kudumisha demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora bila kuingiliwa na mtu au taasisi yeyote.***

THBUB ilianzishwa baada ya kuvunjwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (TKU) mnamo mwaka 2001. TKU kilikuwa ni chombo cha muungano kilichoundwa na Katiba ya Muda ya Tanzania ya mwaka 1965 Ibara ya 67 (1) na Sheria Na. 25 ya mwaka 1966 ambayo iliipa Tume mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yanayohusiana na matumizi mabaya ya madaraka kwa watumishi wa umma.

THBUB ni chombo cha Muungano na ina Ofisi zake Zanzibar ambayo ilifunguliwa kutokana na marekebisho ya Sheria Na 8 ya mwaka 2006, na *Legal Notice* Na 31 ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliridhia Tume kufanya shughuli zake Zanzibar. Tume ilianza kufanya kazi rasmi baada ya Waheshimiwa Makamishna kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Machi, 2002.

## 1.2 Uongozi wa Tume

Tume inaongozwa na Mwenyekiti akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti na Makamishna wengine wasiozidi watano.[2] Uongozi wa Tume uliopo hivi sasa ni wa awamu ya tatu tangu kuanzishwa kwake, na uliteuliwa Januari 2015 na Mhe. Dk Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (Rais wa Awamu ya Nne) ambapo uliungana na Mhe. Kamishna Rajab Alli Hassan aliyebaki kutoka uongozi wa awamu ya pili, ambae alimaliza muda wake mwezi Oktoba 2016. Uongozi uliopo madarakani unatarajia kumaliza kipindi cha kwanza cha miaka mitatu ifikapo Januari mwaka 2018.[3] Kwa mwaka 2015/2016 Makamishna wa Tume walisimamia maeneo ya kazi yafuatayo;

---

[1] Sura ya sita (6), sehemu ya kwanza (1) Ibara ya 129 (1)

[2] Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 129(2) na Sheria ya Tume Na. 7 ya mwaka 2001

[3] Kwa mujibu wa Sheria Na.7/2001 kifungu cha 8(1) Mheshimiwa Kamishna anaweza kuongezewa kipindi kimoja tu cha miaka mitatu baada ya miaka mitatu ya kwanza kumalizika

### 1.2.1 Makamishna na mgawanyo wa usimamizi wa maeneo kazi

Ili kuimarisha na kurahisisha utekelezaji wa kazi za kila siku, Tume imejigawa usimamizi wa maeneo ya kazi ifuatavyo;-

MGAWANYO WA KAZI KWA MAKAMISHNA MWAKA 2015 – 2018

| NA | JINA | CHEO | ENEO LA MAJUKUMU | MASUALA ANAYOSHUGHULIKIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. |  Mhe. Bahame T. Nyanduga | Mwenyekiti | Haki za watu wenye Ulemavu<br>• Masuala ya watu wenye ulemavu wa ngozi<br>• Haki za watu wanaoishi maisha ya asili (Indigenous Peoples Rights)<br>• Haki za vyombo vya habari<br>• Mahusiano na vyama vya Siasa Mwenyekiti | • Utaratibu wa shughuli zote |
| 2. |  Mhe. Iddi R. Mapuri | Makamu Mwenyekiti | • Utawala kwa ujumla na bajeti<br>• Ushirikiano na Taasisi za Serikali kama vile Ikulu, PCCB<br>• Sera na Mipango mbalimbali ya Kitaifa, kukidhi haki za Binadamu<br>• "hifadhi ya jamii kwa watu walio nje au mifuko, haki za wazee | • Masuala yote yanayohusu Mafao |
| 3. | Mhe. Ali H. Rajabu | Kamishna I | Utawala Bora<br>• Maadili katika Utumishi wa Umma<br>• Mahusiano na Asasi za Kiraia | • Masuala yote yanayohusu ajira na nidhamu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4. | <br>Mhe. Mohamed K. Hamad | Kamishna IV Zanzibar | • Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni – hasa mazingira safi,<br>• Haki za binadamu na biashara | • Masuala yote ya haki za binadamu na utawala bora Zanzibar |
| 5. | <br>Mhe. Dr. Kevin Mandopi | Kamishna III | • Utawala wa Sheria<br>• Masuala ya Polisi<br>• Magereza,<br>• Wakimbizi<br>• Mahakama na<br>• Uhuru wa kutoa mawazo na mikusanyiko | • Masuala yote ya haki za Kisiasa na kiraia |
| 6. | <br>Mhe. Rehema M. Ntimizi | Kamishna II | • Masuala ya Ardhi,<br>• Migogoro kati ya makundi mbambali | • Masuala yote yanayohusu matumizi mabaya ya madaraka |
| 7. | Mhe. Salma A. Hassan | Kamishna V | • Haki za makundi maalum wanawake, jinsia na watoto<br>• Haki ya Maji Safi | • Masuala yote ya Makundi Maalum, Mirathi, Maji, Wanawake na Watoto. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| |  | | | |

## 1.2.2 Katibu Mtendaji

Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kinaeleza kuwa, Tume itakuwa na Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriwa na Tume kutokana na watumishi waandamizi wa Serikali. Majukumu ya Katibu Mtendaji ni pamoja na kusimamia shughuli za utawala na utekelezaji wa sera za Tume. Katika kutekeleza majukumu yake, Katibu Mtendaji anasaidiwa na kurugenzi sita ambazo ni; Idara ya Haki za Binadamu, Utawala Bora, Utawala na Rasilimali watu, Huduma za Kisheria, Elimu kwa Umma na Mafunzo, na Utafiti na Nyaraka.



***Mary C. Massay,*** ***Katibu Mtendaji***
Shahada ya Sheria, (1984) Dar es Salaam na Shahada ya Uzamili ya Utawala, (2012) (Dar es Salaam). Ni wakili wa Kujitegemea (1994).Alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Kisheria wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (2004-2010) Kamishna wa Tume ya Usuhishi na Upatanishi (CMA) (2012-2015) Mwanasheria wa Twiga Bankcorp Ltd (1999-2004)

## 1.3 Ofisi za Tume

Tume ina ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam (Makao Makuu) na Zanzibar na matawi katika mikoa ya Mwanza (kwa ajili ya mikoa ya kanda ya ziwa), Lindi (mikoa ya Kusini), na Pemba. Ofisi hizi zimeanzishwa kwa ajili ya kuwafikia wananchi wengi zaidi. Aidha ina mpango wa kufungua matawi katika kanda za Kati, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, na Kaskazini.

## 1.4 Majukumu ya Tume

Kazi za Tume zinatekelezwa kulingana na dira, dhima na malengo ya Tume kama zilivyoainishwa katika Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na katika kifungu cha 6 (1) vifungu vidogo (a) mpaka (o) vya Sheria ya Tume. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

a) Kukuza nchini kinga na hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;
b) Kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa ujumla;
c) Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ;
d) Kufanya utafiti katika, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
e) Inapobidi, kufungua mashauri mahakamani yanayolenga kukomesha ukiukwaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki zinapovunjwa au misingi ya utawala bora inapokiukwa;
f) Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote au taasisi yoyote ambayo vifungu vya sehemu hii vinahusiana navyo katika utaratibu wa kawaida wa kutekeleza kazi za ofisi yake au utendaji wa kazi unaokiuka mamlaka yake;
g) Kupeleleza au kuchunguza malalamiko yanayohusiana na utekelezaji au utendaji wa watu wanaoshikilia ofisi katika utumishi wa Serikali, mamlaka za umma au vyombo vya umma, ikijumuisha taasisi binafsi na watu binafsi ambapo malalamiko hayo yanadaiwa kuwa ni ya matumizi mabaya ya madaraka, huduma za upendeleo kwa mtu yeyote, ikiwa ni mlalamikaji au mtu mwingine, katika kutekeleza kazi zao za kiserikali au umma;
h) Kutembelea Magereza na mahala pengine wanamozuiliwa watu au sehemu zinazofanana kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanaozuiliwa sehemu hizo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hii;
i) Kuchukua hatua za kusaidia kusahihisha, kurekebisha, kuzuia au kukomesha vitendo vilivyotajwa katika vifungu (e), (f), (g) au (h) kutokana na njia za usawa sahihi na haki, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria;
j) Kutoa ushauri kwa Serikali na kwa vyombo vingine vya umma na taasisi za sekta binafsi juu ya mambo maalum yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora;
k) Kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwishatungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakubaliana na haki za binadamu na za misingi ya utawala bora;
l) Kusaidia uridhiaji wa au utiaji saini mikataba au makubaliano yanayohusu haki za binadamu, kuzilinganisha sheria za nchi na kufuatilia na kutathmini utekelezaji ndani ya Jamhuri ya Muungano na Serikali na watu wengine, kwa viwango vya haki za

binadamu vilivyoainishwa kwenye mikataba au makubaliano au chini ya sheria za kawaida za mahusiano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo

m) Kwa kupitia Serikali, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika, Jumuia ya Madola na taasisi nyingine zenye uhusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi za nje ambazo zina uzoefu katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu na utawala bora;
n) Kuchukua hatua zifaazo kwa ajili ya ukuzaji na uendelezaji wa upatanishi na usuluhishi miongoni mwa taasisi na watu mbalimbali ambao hufika au hufikishwa mbele ya Tume;
o) Kufanya kazi nyinginezo zozote kama zinavyoweza kuelezwa katika sheria nyingine.

Aidha, ibara ya 131 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeainisha maeneo ambayo Tume haina mamlaka kuyachunguza kama ifuatavyo.

a) Jambo lolote ambalo liko mbele ya Mahakama au chombo kinginecho cha Kimahakama.
b) Jambo lolote linalohusu uhusiano au mashirikiano kati ya Serikali ya nchi yoyote ya nje au shirika la Kimataifa
c) Jambo linalohusu madaraka ya Rais kutoa msamaha.
d) Jambo jingine lolote lililotajwa na sheria yoyote.

### 1.4.1 Masuala ya Makundi ya Haki (Thematic issues)

Katika kuongeza ufahamu, ufanisi na utendaji kazi wa Watumishi wa Tume, Tume ilibuni na kuanzisha mfumo mpya wa kushughulikia masuala ya "makundi haki" ya haki za binadamu, (Thematic issues) kama ilivyo kwenye tasnia ya haki za binadamu kimataifa, yanayofafanua kwa undani dhana ya haki za kiraia, kisisasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa hiyo Tume ilianzisha na kugawa majukumu ya utekelezaji kwa Watumishi katika makundi haki hayo ambayo ni;

| | **Makundi ya Haki.(Thematic areas)** |
|---|---|
| 1. | Haki za Jamii zinazoishi Maisha ya Asili, (Rights of Indigenous peoples) |
| 2. | Haki za watu Wenye Ulemavu |
| 3. | Haki za Wanawake, Jinsia na watoto |
| 4. | Kupiga vita Biashara haramu ya Binadamu, African Ombudsman and Mediators Aassociation (AOMA) , International Ombudsman Institute.(IOI) |
| 5. | Biashara na Haki za Binadamu (Human Rights and Business), Mahakama ya Jinai ya Kimataifa (International Criminal Court (ICC), Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu (*Office of the High Commissioner for Human Rights (OHCHR*). |
| 6. | Uhuru wa kujieleza, Maoni, na Haki za Wana Habari. (Freedom of Expression and Opinion , Media Rights |
| 7. | Haki ya Elimu na Afya |
| 8. | Masuala ya Ajira, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika (SADC) |
| 9. | Wakimbizi, wakimbizi wa ndani ya nchi (IDPs), Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mtandao wa Taasisi za Haki za Binadamu barani Afrika, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Mtandao wa Kimataifa wa Taasisi za Haki za Binadamu. (GANHRI). |
| 10. | Mahusiano na Taasisi za haki jinai, Kutoweka kwa watu, Mauaji kinyume na sheria (arbitrary and summary executions) mahusiano na Polisi, Magereza, haki za wafungwa na mahabusu, Matendo ya Ukatili, na adhabu ya Kifo. |
| 11. | Wazee na mifuko ya Hifadhi ya Jamii. |
| 12. | Dawati la Watoto |
| 13. | Haki ya Maji na Sheria za Mazingira. |
| 14. | Haki ya Kumiliki mali na nyumba na Haki Ardhi |
| 15. | Maadili na Uwajibikaji, TAKUKURU na Sekretarieti ya Maadili. |
| 16. | Haki za Wakulima na watu wanaofanya kazi vijijini. |

## 1.5 Malengo na Mipango ya Utekelezaji wa Kazi kwa Mwaka 2015/2016

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume imekuwa ikiongozwa na Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa miaka mitano ambao hubeba malengo makuu ya kiutekelezaji na hatimaye kutengenezewa Mpango - Kazi katika Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) pamoja na Mpango Kazi (Action Plan) wa Mwaka husika. Mpango Mkakati wa Tume umezingatia majukumu yake yaliyoainishwa ndani ya Katiba na sheria, Sera ya MKUKUTA (nguzo ya Tatu), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 (Ibara ya 185 (f)), Malengo ya Milenia 2015, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 (lengo la (ii) na (iii), Maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (2030), na Mpango wa Umoja wa Afrika wa Maendeleo ya Afrika mwaka 2063.

### 1.5.1 Mpango mkakati wa Tume (2011/2012 – 2014/2015)

Mpango Mkakati wa Tume umeainisha wazi malengo makuu saba (7) ambayo ni;

a) Kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika,

b) Kujenga uelewa na ufahamu kwa wananchi na wadau wa haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora

c) Kufanya utafiti, ufuatiliaji na kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora

d) Kufanya uchunguzi wa hadharani na ufuatiliaji wa uvunjwaji wa haki za binadamu nchini ili kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora,

e) Kushirikiana kikamilifu na wadau wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala yote ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora

f) Kukagua magereza, vituo vya polisi, mahabusu za watoto, shule ya maadilisho na sehemu nyingine za vizuizi kwa lengo la kutathmini hali ya utekelezaji wa haki za Binadamu katika sehemu hizo na kutoa mapendekezo ya kurekebisha kasoro zitakazojitokeza

g) Kuongeza uwezo wa Tume katika utoaji wa huduma za kisheria kwa kusaidia watu wasio na uwezo wa kupeleka kesi mahakamani.

### 1.5.2 Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013-2017)

Kwa mwaka 2015/2016 Tume iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013-2017) uliozinduliwa Desemba 2013. Mpango Kazi huo unalenga kujenga taifa linaloheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu (*Human Rights Based Approach )* katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali, taasisi za umma, mashirika ya asasi za kiraia na wananchi kwa ujumla ili kuondoa umaskini na kuleta maendeleo sawia kwa wananchi.

Mpango huu pia umelenga katika kujenga jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu (human rights culture) kwa kuzingatia maamuzi na maazimio mbali mbali ya kimataifa ambayo Serikali ya Tanzania imeyakubali. Baadhi ya Maazimio hayo ni Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) unaoisha mwaka 2030, na Mpango wa maendeleo wa Umoja wa Afrika unaojulikana kama Ajenda ya 2063(The African Union Agenda 2063.)

Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo Endelevu unasisitiza malengo 17 ambayo yanatakiwa yafikiwe ifikapo mwaka 2030. Utekelezaji wake utajenga kiwango kikubwa cha ukuaji wa haki za binadamu na utawala bora nchini. Kwa mfano lengo na 2 linahusu kuondoa njaa ambapo haki ya chakula na lishe bora vinahusika. Lengo na 3 litahakikisha ukuaji wa afya njema na ustawi wa watu wote. Lengo namba 4 litahakikisha elimu bora na yenye usawa kwa wote inapatikana. Lengo na 5 linataka uwepo wa usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana wote. Lengo la sita litahakikisha upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kwa wote, na namba nane linalenga kukuzwa kwa ajira bora na ukuaji wa uchumi wenye faida kwa wote. Lengo na kumi linataka kupunguza tofauti baina ya watu katika jamii wakati namba 16 linasisitiza ukuzwaji wa amani, haki sawa kwa wote (*access to justice for all*) na uwepo wa taasisi madhubuti zenye kuwajibika.

Mpango wa Maendeleo wa Afrika, yaani Ajenda ya 2063 umejumuisha malengo yatakayotekeleza haki za binadamu na utawala bora; kwa mfano lengo (*aspiration*) namba 3 linalenga kuwa na Afrika yenye utawala bora, demokrasia, inayoheshimu haki za binadamu, na utawala wa sheria na haki. Mpango wa Kitaifa wa haki za Binadamu unafikia ukomo wake Desemba 2017. Ni matumaini ya Tume kwamba Serikali itafanya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo na kuandaa namna ya kuendeleza mpango mwingine mara tu mpango wa awali wa mwaka 2013 - 2017 utakapo kwisha muda wake. Kwa upande wake Tume ilikwishaanza majadiliano na kuikumbusha Serikali na wadau, hususan Umoja wa Mataifa, umuhimu wa kufanya tathmini. Serikali kwa kushirikiana na Tume ya haki za Binadamu, na Umoja wa Mataifa wameandaa mpango utakaojadiliwa ili mara mpango wa awali utakapokwisha muda wake, upatikane mpango mwingine kwa kipindi kijacho.

# SURA YA PILI

# 2.0 HIFADHI YA HAKI ZA BINADAMU NA MISINGI YA UTAWALA BORA NCHINI

## 2.1 Haki za binadamu na utawala bora

Ibara ya 131 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaagiza Tume kufuatilia utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini na kutayarisha na kuwasilisha taarifa inayoonesha hali ya utekelezaji wa haki za binadamu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa na kikanda ya kulinda haki za binadamu. Mikataba hii imetafsiriwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kuweka nguzo za kusimamia haki za msingi za binadamu. Sura hii inaeleza hali ya hifadhi ya baadhi ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa mwaka 2015/2016. Maelezo ya haki hizi zimegawanywa katika makundi makuu matatu ambayo ni haki za kiraia na kisiasa, haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na haki za makundi yenye mahitaji maalum

Ibara ya 12 hadi ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinatamka haki za binadamu zinazolindwa na Katiba nchini Tanzania. Ibara ya 25 hadi 28 zinatamka wajibu wa kila Mtanzania kwa jamii katika kulinda na kutetea haki za binadamu. Ibara ya 29 and 30 ni masharti ya jumla ya jinsi ya kulinda haki za kila mtu.

Kwa upande wa misingi ya utawala bora, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Tume, namba 7 ya mwaka 2001 na Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Sura 3 ya Sheria za Tanzania kama zilivyorekebeshwa mwaka 2002, hazifafanui maana ya maneno au dhana ya utawala bora. Dhana ya utawala bora inaeleweka kimantiki kwa kuzingatia maandiko ya sheria za utawala na sheria za kikatiba (*Administrative law and Constitutional law*) ambayo imeainisha misingi mikuu ya utawala bora kadhaa ambayo inatambulika ulimwenguni kote, *(universally acceptable pinciples*). Misingi hii inapokiukwa husababisha utawala bora kukosekana.

Kwa mujibu wa Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo-;

(a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wnanchi kwa mujibu wa Katiba hii,
(b) Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi,
(c) Serikali itawajibika kwa wananchi,
(d) Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii”.

Hivyo basi, utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na kufuata utawala wa sheria. Ili kutekeleza dhana ya utawala bora mabo yafuatayo lazima yazingatiwe;

(a) matumizi sahihi ya dola,
(b) matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi,
(c) matumizi mazuri ya madaraka,
(d) watawala kujua na kutambua madaraka waliyonayo na matumizi yake
(e) madaraka yatumike kulingana na mipaka iliyowekwa na katiba na sheria."[4]

Dhana ya utawala bora kwa ujumla inatambua kwamba utawala wa sheria ndiyo msingi wa utawala wa kideomkrasia, na kwamba kila mtu yu sawa mbele ya sheria, na hamna mtu aliyeko juu ya sheria. Dhana ya utawala wa sheria inatambua uwepo wa mihimili mikuu mitatu ya dola na kwamba haki inapatikana kupitia mhimili wa mahakama. Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kwamba Mahakama ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ndiyo mamlaka yenye kauli ya mwisho katika utoaji haki nchini.

## 2.2 Haki ya usawa wa binadamu, na heshima ya utu

Ibara ya 12 ya Katiba inatambua utu wa mtu, kwamba kila mtu amezaliwa huru, kila mtu ni sawa na anastahili heshima na kuthaminiwa utu wake. Haki hii pia inatamkwa kwenye Tamko la Ulimwengu la mwaka 1948 la Haki za Binadamu katika Ibara ya 1 ambalo Tanzania inalitambua.

### 2.2.1 Usawa mbele ya sheria na haki ya kutobaguliwa

Ibara ya 13 inatoa haki ya mtu kulindwa na sheria, na inapiga vita ubaguzi wa aina yeyote kufanywa na mtu au mamlaka yoyote inapotekeleza madaraka yake. Ibara hii inatamka kwamba neno 'kubagua' maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa namna tofauti kati ya watu kulingana na utaifa wao, kabila, pahala anapotokea, maoni ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali ya maisha kwa udhaifu au uduni wao na kuwekewa masharti au vipingamizi ambavyo watu wengine hawatendewi hivyo au kutendewa kwa upendeleo.

#### *2.2.1.1 Haki jinai, haki ya kutoteswa na kutodhalilishwa*

Mateso ni kitendo kinachosababisha madhara ya kiakili au ya kimwili kwa makusudi ambacho hufanywa na chombo cha serikali au mtumishi wa serikali.[5] Baadhi ya watendaji walio katika vyombo vya kutekeleza sheria kama vile Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji, askari wa wanyamapori na mgambo wanatuhumiwa kutesa na kudhalilisha raia kwa ajili ya kupata taarifa au kulazimisha kukiri kosa, kuogopesha au kama adhabu kwa makosa waliyoyafanya. Aidha zipo taratibu za kijamii zenye mifumo ya ulinzi na usalama isiyo rasmi kwa mfano sungusungu ambazo zinalalamikiwa kuendeleza vitendo vya udhalishaji na utesaji katika jamii. Pia, watu binafsi wanatuhumiwa kuvunja haki za raia, kwa kusababisha maumivu au namna nyingine ya utendaji usiokuwa wa kibinadamu, ambayo hutambulika kuwa ni makosa ya jinai kama vile shambulio, kupiga, uvunjaji mkubwa wa heshima na mengine kama hayo ambayo yanapotendwa

[4] Angalia Uk wa 1, Sura ya Kwanza, kijitabu cha Mwongozo wa Utawala Bora, kilichoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Policy Forum, Septemba 2003.

[5] Mkataba Dhidi ya Mateso na Utendeaji au Adhabu Nyingine ya Kikatili Isiyokuwa ya Kibinadamu ya Kudhalilisha (1984) Ibara ya 1

na askari hao, yanastahili kutolewa adhabu ya makosa ya jinai kwa mujibu wa Sheria ya *Kanuni ya Adhabu.*[6]

Matukio ya watu kuteswa na kudhalilishwa yaliripotiwa kufanyika katika sehemu ambazo watuhumiwa wanazuiliwa kwa mujibu wa sheria, hasa katika vituo vya Polisi.[7] Matukio hayo ni pamoja na adhabu ya kuchapwa viboko na kufungiwa kwenye selo za adhabu. [8] Yapo malalamiko yaliyotolewa na mahabusu wakati wa ukaguzi wa Magereza na Vituo vya Jeshi la Polisi yalioashiria kuwepo kwa mateso na vipigo vinavyotolewa na askari polisi kwa mahabusu wakati wa kuwakamata na kuwahoji. [9] Vipigo hivyo ni kinyume ya sheria na utaratibu na ukiukwaji wa haki za binadamu za mahabusu. Pia, kwa wahalifu walio chini ya umri wa miaka 18 kubadilishiwa umri, kuchanganywa na mahabusu watu wazima na baadaye kesi zao kupelekwa katika mahakama za mwanzo kinyume na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009.[10]

Ingawa baadhi ya adhabu hizo zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu[11], adhabu ya kuchapa viboko[12] na Prisons General Orders (PGO). Utekelezaji wa baadhi ya adhabu hizi unakinzana na Mkataba ya kimataifa Kuzuia Adhabu za Kudhalilisha na Kutweza utu wa mtu.[13] Aidha, adhabu ya viboko inatolewa kwa wanafunzi kwa mujibu wa Kanuni za Elimu maarufu kama adhabu ya kuchapa viboko wanafunzi.[14] Adhabu ya kuchapa viboko inatumiwa na walimu ikiwa ni njia ya kufundisha na kuadabisha wanafunzi mashuleni na watoto majumbani. Matumizi ya adhabu hii ya viboko kwa watoto yanaharimishwa na mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda kuhusu haki za watoto ambayo Tanzania tumeridhia.[15] Tume inashauri sheria hizi zifanyiwe marekebisho kwa kuwa utekelezaji wake unavunja haki za binadamu. Kwa maoni ya Tume, sababu zinazoendeleza kuwepo kwa mateso ni pamoja na ;

(i) Serikali kushindwa kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaopinga mateso. (*The Convention Against Torture and other Cruel, Inhuman, Degrading Treatment or Panishment* wa mwaka 1984.

(ii) Kukosekana kwa sheria maalumu inayoharamisha utesaji na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kukamata na kuweka watuhumiwa rumande.

(iii) Kutokuwepo uwajibikaji kwa watu au taasisi zinazodhihirika kuhusika na vitendo vya utesaji kwa wananchi au watuhumiwa.

[6] Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 R.E 2002
[7] Taarifa za Ukaguzi wa Magereza na Vituo vya polisi za mwaka 2011 na 2013
[8] Sheria ya adhabu ya kuchapa viboko Sura ya 17 R.E 2002
[9] THBUB taarifa ya Ufuatiliaji wa Watoto walio Katika Vizuizi mbali mbali 2015/2016
[10] THBUB taarifa ya Ufuatiliaji wa Watoto walio Katika Vizuizi mbali mbali 2014.
[11] Kifungu cha 25 na 26 cha sheria ya Kanuni ya adhabu Sura ya 16
[12] Sheria ya adhabu ya kuchapa viboko Sura ya 17 R.E 2002
[13] Ibara ya 1 ya Mkataba wa kimataifa wa Kuzuia Utesaji (CAT)
[14] Tangazo la Serikali Na. 294/2002 lililotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 60 (o) cha Sheria ya Elimu Sura ya 353.
[15] CRC –Ibara ya 37 na 28 (2) Mtoto ana haki ya kutendewa utu wakati wowote. Haki ya kutoteswa au kuadhibiwa kwa njia katili au isiyo ya kiutu.

(iv) Kutokuwepo na juhudi za kutosha za kufuatilia watu walio vizuizini (hasa rumande za polisi).

(v) Kutokuzingatiwa kwa sheria na taratibu zinazolinda haki za watu wakiwa vizuzini.Udhaifu wa vyombo vya kusimamia sheria katika kupeleleza na hivyo kusababisha matumizi ya nguvu kupita kiasi ili kulazimisha watuhumiwa kukiri au kutoa taarifa.

(vi) Mazingira ya kutweza utu wa mtu yaliyoko katika magereza na rumande za vituo vya polisi.[16]

(vii) Uwezo mdogo wa mbinu za kitaalamu wa vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sheria na upelelezi.

Suala la utesaji pia lilielezwa katika taarifa ya UPR ya 2011, na taarifa ya utekelezaji wake ya mwaka 2012. Serikali ilikubaliana na mapendekezo 107 yaliyotolewa na Baraza la Hakiza Binadamu la Umoja wa Mataifa, ambayo kati ya hayo moja wapo lilikuwa ni kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaozuia Utesaji na Vitendo vyinavyotweza utu wa Mtu (*the Convention against Torture and other Cruel, Inhuman and Degrading Treatment or Punishment (CAT).*[17] Tume inaishauri serikali kuharakisha hatua za kuridhia mkataba huo kwa kushirikisha wadau wa haki za binadamu. Pia Tume inaishauri serikali kuwachukulia hatua zinazostahili wale wote wanaodhihirika kutesa au kutoa adhabu zinazotweza utu wa mtu.

## 2.3 Haki ya Kuishi

Haki ya kuishi imeainishwa katika Ibara ya 14 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kimataifa na ya kikanda ambayo Tanzania imeridhia. Ibara ya 6(1) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa inaeleza kuwa kila binadamu ana haki ya kuishi na kuwa haki hii italindwa kisheria na hakuna atakayenyimwa haki hiyo kiholela. Pamoja na jitihada za serikali katika kuhakikisha haki hii inalindwa, bado kumekuwepo na changamoto zilizojitokeza katika kipindi hiki zilizoondoa haki hii. Uwepo wa adhabu ya kifo katika sheria za Tanzania, na matukio ya mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, mauaji ya wazee husasan wanawake, mauaji ya kujichukulia sheria mkononi, na mauaji yanayofanywa na vyombo vya kutekeleza sheria kama vile polisi, ni kati ya changamoto zilizojitokeza katika uhifadhi wa haki ya kuishi.

### 2.3.1 Vifo kutokea mikononi mwa Polisi

Tume imebaini kuwa tatizo la askari wa Jeshi la Polisi kuuwa watu au watu kufariki wakiwa mikononi mwa Jeshi la Polisi kuwa ni tatizo kubwa na uwajibikaji wa Jeshi la Polisi katika

---

[16] NANHRI, The Role of Southern African NHRIs in Torture Prevention, p.3

[17] A/HRC/19/4/Add. of 12th March 2012 on "Views on conclusions and/or recommendations, voluntary commitments and replies presented by the State under review (Tanzania)"

kushughulikia malalamiko haya ni hafifu. Katika kipindi hiki Tume ilipokea malalamiko toka kwa wananchi kuhusu vifo vilivyotokea au kusababishwa na askari wa Jeshi la Polisi. Tume iliwasiliana na Jeshi la Polisi kuhusu malalamiko hayo, lakini matendo hayo bado yanaendelea kujitokeza . Jeshi la Polisi ni chombo cha kutenda haki katika mfumo wa haki Jinai, kwani lina jukumu la kulinda raia na mali zao.

Inapotokea kuwa askari wa Jeshi la Polisi wanatuhumiwa kuhusika na mauaji ya raia, au matumizi ya nguvu kupita kiasi, na bado Jeshi la Polisi halionekani kuchukua hatua za kulinda haki za raia au marehemu, Tume inaona kuwa kuna mushkeli mkubwa katika namna Jeshi la Polisi linavyoshughulikia malalamiko ya aina hii, kwani inakuwa kana kwamba Jeshi la Polisi linawalinda wahalifu miongoni mwao. Tume iliendelea kufuatilia suala hili na kushauriana na vyombo husika juu ya utekelezaji wa haki hii .Tume inaendelea kufuatilia ili kupata taarifa sahihi ya hatua ambazo Jeshi la Polisi linachukua ili kukomesha mauaji kama hayo;

(i) Jalada HB/S/185/09/10/POLISI/DSM. Marehemu alikuwa taxi dereva alikamatwa na Polisi wa Kituo cha Chang'ombe, Wilaya ya Temeke tarehe 8/3/2010 na kufungukiwa jalada CHA.IR/1688/2010 na kuhusishwa na unyang'anyi wa kutumia silaha. Ndugu zake walifika kituoni usiku wa tarehe hiyo na wakashuhudia akichukuliwa na askari kikosi cha tembo 42. Ndugu zake hawakumwona tena mpaka tarehe 10/03/2010 akiwa amefariki na kupelekwa Hospitali ya Temeke ambako uchunguzi wa daktari ulionyesha alifariki kwa "suffocation". Uchunguzi wa Mkemia ulionyesha alipewa chakula chenye sumu ya 'diazon' Majibu ya Polisi yaliku watu kwamba hali ya marehemu ilibadilika ghafla tarehe 10/3/2010.

(ii) Jalada HB/S/850/14/15/POLISI. Marehemu alikamatwa tarehe 17/6/2015 na kufikishwa kituo cha Wazo Hill. Akikabiliwa na tuhuma za wizi wa magari matatu.Tarehe 01/06/2015 alipelekwa mahakamani na kusomewa mashtaka na kurudishwa Kituo cha Oysterbay, ambako alifariki tarehe 02/6/2015. Taarifa ya uchunguzi wa daktari ulionyesha alifariki kwa 'septic shock' Shahidi (mshatakiwa mwenza) aliyehojiwa na Tume alieleza kuwa yeye pamoja na marehemu wakiwa chini ya ulinzi wa Polisi waliteswa kituo cha Boko, Kawe na Oysterbay. Baada ya kupelekewa taarifa ya uchunguzi wa Tume, imeendela kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake.

(iii) Jalada HB/S/630/15/16/POLISI/DSM, Taarifa iliifikia Tume tarehe 30/6/2016 kwamba kuna watuhumiwa walikuwa kituo cha kati Dar es salaam wakiwa wamefanyiwa ukatili na kuvunjwa miguu wakiwa chini ya ulinzi wa Polisi bila kupelekwa hospitali. Tume ilifuatilia na kufanya ukaguzi, Tarehe 1/7/2016 Tume iliandikia jeshi kutaka kufanya uchunguzi na haikupewa kibali hicho mpaka tarehe 21/7/2016 na mapaka Tume inafika mahabusu hao walishaondolewa na haikujulikana wamepelekwa wapi. Jeshi la Polisi halikutoa ushirikino kama Kifungu 14(2) cha Sheria ya Tume namba 7/2001 kinavyoagiza.

### 2.3.2 Adhabu ya Kifo

Adhabu ya kifo inatolewa kwa mujibu wa Kifungu 197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu ( The Penal Code, Cap 16 R.E.2002] nchini. Adhabu hii inatolewa na mahakama kwa makosa ya mauaji, uhaini na mengine ya kijeshi. Kwa kipindi cha miaka 23 adhabu hii haijatekelezwa (defacto moratorium) kwani kwa mara ya mwisho ilitekelezwa mwaka 1994.

Adhabu ya Kifo iliingizwa kwa mara ya kwanza katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu (*Penal Code*) mwaka 1945. Hadi kufikia mwaka 2015 idadi ya wafungwa wa kunyongwa ilikuwa ni 465, ambapo wanaume walikuwa 445 na wanawake 20.[18] Kwa vile adhabu hii haijatekelezwa kwa muda mrefu na pia ni kinyume na Ibara ya 14 ya Katiba na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu, Tume inashauri kufutwa kwa adhabu hii au kutolewa kwa adhabu mbadala ya kifungo cha maisha badala ya adhabu ya kifo. Pamoja na ushauri wa Tume, yapo mashauri yaliyofunguliwa kupinga hukumu ya kifo katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, mjini Arusha .[19]

Katika taarifa ya kujitathmini (Universal Periodic Review) iliyowasilishwa kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mwezi Mei 2016, (*United Nations Human Rights Council*) Serikali ilitamka kwamba, *"*Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Ukatili na Adhabu za Kutweza na Kudhalilisha Utu wa Mtu *(The Convention Against Torture and other Cruel, Inhuman, and Degrading Treatment of Punishment 1984) haujaridhiwa na serikali na bado hukumu ya kifo imeendelea kutolewa na mahakama. …"* Katika maelezo ya ziada serikali inasema kuwa *"Currently the Constitution of theUnited Republic of Tanzania, 1977 prohibits torture and remedies for victims of torture are available through the Basic Rights and Duties Enforcement Act, CAP 3 and the Commission for Human Rights and Good Governance."*[20]

Kwa ufupi serikali inasema kuwa haijaridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Ukatili na Adhabu za Kutweza na Kudhalilisha Utu wa Mtu wa mwaka 1984 ikiwemo adhabu ya kifo, na kwa kuwa Katiba ya mwaka 1977 inazuia adhabu hizo. Serikali inasema pia kwamba kwa kuwa haki za binadamu zinalindwa kwa mujibu wa Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania, na pia Tume ina mamlaka ya kupokea na kusikiliza malalamiko kuhusu adhabu za kutweza na mateso hivyo kuna ulinzi wa kutosha ndani ya katiba na sheria dhidi ya adhabu ya kifo.pamoja na maelekezo yaliyotolewa na serikali, Tume inaiomba serikali kuangalia upya suala la utekelezaji wa adhabu ya kifo Tume inaishauri Serikali kuridhia Mkataba wa Kupinga matendo na adhabu za Mateso wa mwaka `1984 na Itifaki ya Pili ya Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1989 inayozitaka nchi wanachama kufuta adhabu ya kifo.

Tume kwa kushirikiana na mabalozi wanaowakilisha nchi 11 za Umoja wa Ulaya mnamo tarehe 10 Oktoba 2015 ilishiriki katika kampeni ya Siku ya Kimataifa kupinga adhabu ya kifo duniani kwa kutembelea na kukagua hali ya wafungwa wa kunyongwa katika Gereza Kuu la Ukonga. Katika risala yao ya kuadhimisha siku hiyo, wafungwa waliohukumiwa kunyongwa waliiomba serikali kubadilisha hukumu yao na kufutwa kwa adhabu ya kifo kuwa kifungo cha maisha.

[18] Taarifa ya UPR ya mwaka 2016

[19] Angalia Ripoti ya mwaka 2016 ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika, ya tarehe 1 Januari hadi 31 Desemba, 2016; Maombi na. 001/2015 Amand Guehi v Tanzania, Maombi na. 007/2015 Ally Rajab v Tanzania, Maombi na. 003/2006 John Lazaro v Tanzania, Maombi 004/2016 Evodius Rutachura v Tanzania, Maombi na. 015/2016 Habiyalimana Augustino and Another, v Tanzania, Maombi na. 017/2016 Deogratius Nicolaus Jeshi v Tanzania, na Maombi na 018/2016 Cosma Faustine, Maombi na 021/2016 Josweph Mukwano v Tanzania, Maombi na 024/2016 Amini Juma v Tanzania yaliyofikishwa kwenye mahakama hiyo. Kulingana na Ripoti hiyo Tanzania haikutekeleza amri ya Mahakama ya kusistisha adhabu hizo wakati maombi hayo yakisikilizwa na Mahakama ya Afrika, ingawaje taarifa zinadai kwamba serikali haijawahi kutekeleza hukumu hizo na maombi hayo bado yanaendelea.

[20] Anagalia Ripoti ya Tanzania A/HRC/WG.6/25/TZA/1 ya tarehe 10 February 2016, paragraph 30 na footnote 22 kwenye www.ohchr.org/EN/HRBodies/UP.

Washiriki wa kampeni hiyo waliendelea kuisisitiza serikali kuiondoa adhabu ya kifo katika sheria zake, kwa sababu ni adhabu ambayo haifundishi wala kumaliza makosa ya mauaji




***Ujumbe wa mabalozi 11 wa Jumuiya ya Ulaya na Mkurugenzi wa Haki za Binadamu, Bw. Francis Nzuki ulipowatembelea wafungwa waliohukumiwa kunyongwa walioko katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam katika Kampeni ya siku ya kupinga adhabu ya kifo duniani tarehe 10 Oktoba 2015***

## 2.4 Haki ya uhuru wa mtu binafsi

Ibara ya 15 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka haki ya kuishi kwa uhuru na inakataza mtu kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyanganywa uhuru wake isipokuwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kisheria au katika kutekeleza sheria, au kunyimwa uhuru wake kwa ajili ya kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama.

Ibara ya 9(4) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia wa mwaka 1966 inaeleza kwamba mtu anaponyimwa uhuru Mahakama inawajibika kusikiliza shauri lake na kulitolea maamuzi bila kuchelewa. Ukaguzi uliofanywa na Tume katika Magereza 41 nchini kwa mwaka 2016 unaonyesha kuwepo kwa watuhumiwa waliokaa muda mrefu bila mashauri yao kukamilika. Ilibainika kuwa kesi za mauaji, uhalifu wa kutumia silaha, kesi ya madawa ya kulevya, ugaidi na ubakaji huchukua muda mrefu kukamilika. Kwa mfano, katika ukaguzi huo, Tume ilibaini mahabusu mmoja katika Gereza la Segerea amekaa miaka tisa akisubiri kesi yake kukamilika.[21] Maelezo yaliyotolewa kwa kuchelewa kwa kesi hizo ni aina ya kesi kuhitaji uchunguzi wa kina, kutokamilika kwa upelelezi kwa wakati, kucheleweshwa kwa majibu ya ushahidi toka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, na upungufu wa rasilimali watu (Majaji) na fedha, na urasimu katika baadhi ya idara zinazoshughulikia haki jinai.

Hali hii ya kutokamilika kwa kesi kwa muda unaotakiwa ni uvunjifu wa haki za watuhumiwa na pia ni kinyume na Ibara ya 9(4) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. Tume inashauri vyombo vya haki jinai kama vile Mahakama, Polisi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa na mpango mkakati ambao utakaowezesha kesi kukamilishwa kwa wakati.

---

[21] Taarifa ya ukaguzi 2016/17

## 2.5 Haki ya faragha, usalama wa mtu

Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua haki na stahili ya mtu kupewa heshima na kupata hifadhi ya nafsi yake, maisha yake binafsi, familia yake, unyumba wake na heshima ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi. Ibara hii inafafanua jinsi ya kuhakikisha uhifadhi wa haki hii unavyotekelezwa kwa kuweka sheria kuhusu, faragha na usalama wa mtu binafsi utakavyo hifadhiwa.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 haijaainisha wazi kuhusu haki ya mtu kuwa na makazi bora. Hata hivyo Ibara ya 8(1) (b) ya Katiba inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa jamii. Ustawi wa jamii kwa tafsiri rahisi unajumuisha kuhakikisha kuwa wananchi wanaishi maisha mazuri, ikiwemo kupata ulinzi dhidi ya maisha yao, afya yao na makazi. Kwa mujibu wa Ibara ya 9(a) ya Katiba, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa utu na haki nyinginezo za binadamu zinaheshimiwa. Kwa mantiki hii, haki ya makazi bora ni mojawapo ya haki hizi. Uchunguzi wa Tume ulibaini kuwa haki ya hifadhi ya faragha ya mtu na maisha ya familia, na heshima ya makazi, hata kama ni makazi duni, imekuwa ikikiukwa kutokana na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo bila hata ya waathirika kulipwa fidia au kupewa makazi mbadala

Kwa mwaka huu, Tume ilipokea malalamiko yanayohusu bomobomoa zililosababisha watu kukosa makazi na kuishi nje kwa siku kadhaa katika bonde la Mto Msimbazi. Matukio ya watu kubomolewa makazi yao yalijitokeza katika hifadhi ya Reli, hifadhi ya barabara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na katika maeneo ya wazi pasipo kulipwa fidia. Malalamiko haya yanaonesha kwamba kimsingi nyumba zilivunjwa pasipo kufuatwa utaratibu wa sheria na kuheshimu utu wa binadamu. Sheria zinaruhusu Serikali kutwaa ardhi ya mtu kwa ajili ya manufaa ya umma au kuwaondoa sehemu zilizovamiwa kwa kutumia utaratibu uliowekwa.[22]

Zoezi la kuwaondoa kwa nguvu (*forced eviction)* watu katika makazi yaliyokuwa mabondeni limesababisha uvunjifu wa haki za binadamu na kuwaacha watu bila kuwa na makazi na hivyo kuhatarisha ustawi wao wa kiafya na hata kuhatarisha maisha yao.

[22] Sheria ya Ardhi; Sura ya 118 ; Utwaaji - kifungu 3 Mamlaka kwa Rais kutwaa ardhi; 11 kulipia fidia



***Ubomoaji wa nyumba katika bonde Msimbazi Dar es Salaam na uharibifu wa mali zilizokuwemo ndani wakati wa zoezi la bomoabomoa ambapo watu walikosa makazi na mali kuharibiwa.***

Kubomoa nyumba za watu bila kuwapa makazi mbadala kunakinzana na Maoni Na. 4 *(UN Human Rights Committee General Comment)* ya Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Mkataba wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni inayooanisha haki ya kupata makazi bora na haki ya kuishi. Aidha, uchunguzi wa awali wa Tume unaona kuwa kubomoa makazi ya mtu bila kumtafutia makazi mengine ni kinyume na Maoni Na.7 ya Kamati ya Mkataba huu inayobainisha kuwa kila mtu ana haki ya kufurahia haki za makazi yake bila kuondolewa kwa nguvu kwani kufanya hivyo kunasababisha uvunjifu wa haki nyingine kama haki ya kuishi, haki ya ulinzi wa mtu, haki ya kutoingiliwa faragha, haki ya kuwa na familia na haki ya kumiliki mali bila ya bugudha.[23]

Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa katika Maoni yake ya Jumla Na. 16, Tume inashauri kuwa kuingiliwa kwa makazi ya mtu kunaweza kufanyika pale tu inapolazimu na kwa kuzingatia sheria. Aidha, ni muhimu kufuata sheria na utaratibu madhubuti kabla ya kuwaondoa watu kwenye makazi wanayoishi ikiwa ni pamoja na kuwatafutia waathirika makazi mbadala, kuwalipa fidia na kuwapa misaada itakayowawezesha kupata makazi mbadala.

Hata hivyo wakati Tume inatayarisha taarifa hii (2015/2016) ilikuwa inaendelea na uchunguzi wa wa ubomoaji wa makazi haya hivyo taarifa kamili yenye mapendekezo itajumuishwa kwenye taarifa ya Tume ya mwaka 2016/2017

[23] Aya ya 4 ya Maoni Na 7 ya Mkataba wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, pia Taarifa ya Mtaalamu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Makazi Bora, Ndugu Leilani Farha iliwasilishwa kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 8 Agosti, 2016

## 2.6 Uhuru wa Mawazo, habari na mawasiliano

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatoa uhuru wa fikra, habari, uhuru wa kujieleza, na haki ya kupata habari bila ya kujali mipaka ya nchi, uhuru wa mawasiliano bila kuingiliwa, na haki ya kupewa taarifa kuhusu matukio muhimu, maisha na shughuli za wananchi, na masuala ya kijamii. Hii ni haki ya msingi katika jamii yoyote inayoheshimu misingi ya kidemokrasia na utawala bora

Aidha, kwa pamoja, Ibara ya 19 ya Tamko (au Azimio) la Dunia la Haki za Binadamu Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na za Kisiasa, na Ibara ya 19 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981, kwa pamoja zinatambua haki ya uhuru wa kuwa na mawazo na wa kujieleza bila kungiliwa. Aidha, Kifungu cha 1 cha *Tamko la* Misingi ya Uhuru wa Kujieleza katika Afrika la mwaka 2002 kinasisitiza kuwa uhuru wa kujieleza na wa kupata habari ni haki ya binadamu ya msingi na isiyoweza kuondolewa na ni sehemu ya demokrasia.

Katiba ya nchi haijaweka mipaka au kufunga haki hii ingawaje haki hii imeathirika sana kutokana na sheria zilizotungwa, au maamuzi mbalimbali ya Serikali. Utekelezaji wa haki hizi kwa vitendo ulikabiliana na changamoto za kuwepo kwa baadhi ya vipengele vinavyonyang'anya haki hizo katika sheria zinazoweka masharti kuhusu uhuru wa kujieleza, wa maoni na uhuru wa kupata habari. Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015 na Sheria ya Huduma ya Habari ya mwaka 2016 zimetungwa na ni sheria ambazo zina vipengele vinavyokinzana na haki hii inayolindwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Hapo awali Kifungu cha 25 (1) cha Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 kilimpa mamlaka Waziri mwenye dhamana kuzuia uchapishwaji wa gazeti kupitia amri katika Gazeti la Serikali endapo Waziri atakuwa na maoni kuwa uzuiaji huo ni kwa manufaa ya umma au kuimarisha amani na utulivu katika jamii. Kifungu cha 55 cha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 pia kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana kuzuia uchapishaji au utangazaji wa maudhui yanayohatarisha usalama wa taifa au jamii.

Kupitia kifungu hicho Serikali ilifungia Gazeti la Mwanahalisi ambalo lilifunguliwa baada ya kupeleka hoja ya Kikatiba Mahakama Kuu ya Tanzania na kushinda kesi. Aidha, mwezi Januari mwaka 2016, Serikali ililifungia gazeti la Mawio kuchapisha na kusambaza nakala zake kupitia tangazo kwenye gazeti la Serikali na 55 la tarehe 15/01/2016 chini ya kifungu cha Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Sheria ya Mawasiliano ya mwaka 2010.

Vifungu vya 35 na 36 vya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 vinakinzana na haki ya uhuru wa maoni na kujieleza kama ulivyoainishwa katika Katiba ya nchi. Vifungu hivi vinafanya makosa yanayohusiana na kashfa za kisiasa kuwa makosa ya jinai ambayo kwa kawaida ni makosa ya madai ya uvunjifu wa sifa (*defamation).*

Kwa kupitia Sheria hii baadhi ya wanasiasa walihojiwa na polisi kwa kutoa maoni yao katika mikutano na midahalo ya kitaaluma kwa tuhuma za kutoa kauli zenye kuleta uchochezi kwa jamii.

Katika hatua nyingine, kuanzia Januari 2016, Serikali ilizuia vyombo vingine vya habari kurusha matangazo ya moja kwa moja ya vikao vya Bunge na kuanzisha idara maalum ya Bunge ya kurusha matangazo hayo moja kwa moja kwa baadhi ya vikao na kuhariri sehemu ya matangazo hayo ambayo yalirushwa baadae saa tatu usiku kupitia TBC1.[24] Waziri wa Habari, Utamaduni, Michezo na Sanaa, Nnape Nnauye alitangaza kusitishwa kwa matangazo ya Bunge mubashara akieleza kuwa kumetokana na gharama kubwa za urushwaji wa matangazo. Uamuzi huo wa Serikali ulileta mgongano wa kimawazo na kupokelewa kwa hisia tofauti na wananchi baadhi yao wakilaumu serikali kwa hatua hiyo. Kutokana na kusitishwa kwa matangazo ya moja kwa moja ya Bunge, baadhi ya Taasisi zilijitolea kulipia gharama za matangazo hayo lakini ilishindikana.[25]

Haki ya uhuru wa maoni na kupashana habari ni moja ya haki za msingi zinazowezesha uwepo wa demokrasia ya vyama vingi hapa Tanzania tangu mwaka 1992. Mfumo wa vyama vingi kikatiba unaruhusu uwepo wa maoni tofauti, kwa hiyo maoni yaliyo tofauti na sera za serikali yasionekane kuwa ni makosa ya jinai.

Tume inavishauri vyombo vya vya usimamizi wa sheria kuheshimu katiba na sheria za nchi zinazotoa uhuru na haki hii. Haki hii ni ya msingi kwakuwa inatoa nafasi kwa wananchi kuchangia mawazo yao katika shughuli za maendeleo na kutekeleza wajibu wao wa kuishauri serikali juu vya vyombo na utendaji wake.

## 2.7 Uhuru wa kukusanyika na kuungana katika vikundi mbalimbali

Ibara ya 20 ya Katiba ya nchi inatambua uhuru wa mtu kukusanyika na kukutana na watu wengine kwa hiari na kushirikiana, na kutoa mawazo yao hadharani, kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika mbalimbali kwa kuendeleza imani au maslahi ya pamoja. Uhuru wa kukusanyika na haki hiyo, ndiyo msingi wa kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa. Ibara hii ndiyo inayoweka misingi muhimu ya Utaifa katika kuendesha siasa za vyama vingi nchini Tanzania. Uhuru wa kujumuika pia unalindwa na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322[R.E 2002][26] na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992. Sheria hizi hudhibiti mienendo ya kukusanyika kisheria kwa kuweka taratibu za kufuata pindi panapokuwa na ulazima wa watu kukusanyika.

Upatikanaji wa haki hii ulikumbwa na changamoto mbalimbali hasa kuhusiana na mkanganyiko katika tafsiri ya majukumu na mamlaka ya Jeshi la polisi katika ulinzi na usalama wa wananchi

---

[24] Media Council of Tanzania; Report of the investigation on the Cessation of Live Coverage of Parliamentary Sessions; September 2016

[25] Mwananchi; TMF yajitolea kuilipa TBC irushe Bunge 'live' Ijumaa, Februari 26,2016; http://www.mwananchi.co.tz/habari/Kitaifa/TMF-yajitolea-kuilipa-TBC-irushe-Bunge--live-/1597296-3093270-mt6kp6/index.html

[26] Kifungu cha 43 na 44 cha Sheria ya Jeshi la Polisi

wanapokusanyika. Kwa mfano Jeshi la Polisi limekuwa likitumia vibaya mamlaka yake kisheria kwa kupiga marufuku mikusanyiko mbalimbali kwa dhana kwamba mikusanyiko hiyo inaweza kuvunja amani au kuvuruga usalama wa umma. Kuna baadhi ya matukio yaliyozuia upatikanaji wa haki hii ikiwa ni pamoja na tamko la Jeshi la Polisi la tarehe 7 Juni 2016 lililozuia mikutano ya kisiasa nchi nzima.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilijulisha Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali maoni na ushauri wake kwamba zuio la Jeshi la Polisi halikukidhi matakwa ya Sheria na Katiba ya nchi. Hivyo zuio hilo liliwanyima wananchi na vyama vya siasa haki na uhuru wa kushiriki katika shughuli za kisiasa. Wajibu wa Jeshi la Polisi kutoa ulinzi kwa wananchi hasa wakati wa mikusanyiko ili kuhakikisha wanafurahia uhuru na haki zao zilizoko ndani ya Katiba na Mikataba ambayo Serikali imeiridhia. Pamoja na ushauri wa Tume kuhusu uhalali wa zuio hilo limeendelea kutekelezwa kinyume na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 20 inayotoa haki ya kukusanyika. Kwa mfano Jeshi la Polisi lilitumia madaraka yake kuzuia mikusanyiko hata wakati wa mazishi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza alitoa zuio la kukusanyika kwa ndugu, familia, marafiki na wafuasi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo kushiriki katika mazishi ya kada na kiongozi wa CHADEMA marehemu Alphonce Mawazo aliyeuawa kikatili na watu wasiojulikana. Familia na wanachama wa Chadema walipanga kuaga mwili wa ndugu yao ambazo zilipangwa kufanyika katika viwanja vya Furahisha Mwanza lakini Kamanda wa Polisi alipiga marufuku mkusanyiko huo kwa maelezo ya kuwepo ugonjwa wa kipindupindu jijini Mwanza[27]. Hata hivyo taratibu za mazishi hayo ziliendelea baada ya hukumu ya mahakama kuruhusu

## 2.8 Uhuru wa kushiriki shughuli za umma na utawala wa nchi

Ibara ya 25 (a) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 inaeleza haki ya kila raia ya kushiriki katika shughuli za umma ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa hiari. Pia, Ibara ya 25 (b) inaeleza haki ya kupiga kura au kuchaguliwa katika chaguzi za vipindi mbalimbali ambazo ni za huru na haki. Aidha, haki hii imeelezwa pia katika Ibara ya 21 ya Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948 na Ibara ya 13 (1) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.

Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inatamka haki ya raia ya uhuru wa kushiriki katika utawala wa nchi moja kwa moja au kupitia wawakilishi kwa hiari, kwa kuchagua au kuchaguliwa, kuteua au kuteuliwa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria. Kila raia ana haki na uhuru wa kushiriki kwa kikamilifu katika kufikia maamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake na yanayolihusu taifa.

Katika kuhakikisha kuwa kila raia mwenye sifa za kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kuratibu chaguzi mbalimbali nchini.[28] Katika

[27] Mwananchi "Polisi marufuku kukusanyika kuaga mwili wa Mawazo" tarehe 21 Novemba 2015
[28] Ibara 74 (6) (a-e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kuhakikisha kuwa zoezi la uchaguzi linafanyika Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliendesha shughuli za uboreshaji wa daftari la wapiga kura, kuratibu mikutano ya kampeni na uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka 2015.

Tume ilifuatilia taratibu za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kuanzia uboreshaji wa daftari la wapiga kura, mikutano ya kampeni za wagombea, upigaji na kuhesabu kura na kutangazwa kwa matokeo. Uangalizi wa Tume ulipima utekelezaji wa vigezo mbalimbali vya maadili ya uchaguzi vilivyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika tangazo la Serikali Na. 294 la tarehe 27 Julai 2015 chini ya Kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Sera ya Habari na Utangazaji 2003 Toleo la pili 2006.Aidha, Tume ilipima uzingatiwaji wa Miongozo na Misingi kwa ajili ya Matangazo ya Uchaguzi katika Ukanda wa SADC (*Guidelines and Principles for Coverage of Elections in the SADC Region*), Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Penal Code cap 16), Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (2010), Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia 1966, Mkataba wa Kimataifa wa Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (1966), Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu 2006, Misingi na Mwongozo wa SADC zinazosimamia Uchaguzi wa Kidemokrasia.

### 2.8.1 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Daftari la kudumu la wapiga kura liliboreshwa kwa kutumia Mfumo wa Teknolojia mpya ya Uandikishaji *Biometric Voter Registration (*BVR) tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.[29] Zoezi hili lilifanyika kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza ilikuwa ya majaribio na awamu ya pili ilikuwa ya uandikishaji wa wapiga kura kwa nchi nzima. Changamoto mbalimbali zilijitokeza katika zoezi hili ikiwa ni pamoja na;


a) **Wananchi kujiandikisha zaidi ya mara moja**
Vyombo vya habari viliripoti kuwa baadhi ya wananchi walijiandikisha mara mbili. Kwa mfano jumla ya wananchi 152 walibainika kujiandisha mara mbili katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa na Njombe.[30]

b) **Waandikishaji BVR kutolipwa posho zao kwa wakati**
Pamoja na kufanya kazi katika mazingira magumu, ililalamikiwa kuwa waandikishaji wa BVR hawakulipwa posho zao kwa wakati kama inavyostahili. Kwa mfano waandikishaji 140 wilayani Chunya walicheleweshewa posho zao jambo ambalo liliwafanya waache kazi na kuizingira ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na kutishia kulala ofisini hapo hadi hapo watakapolipwa stahili zao.

c) **Utendaji wa mashine na waandikishaji**

[29] Kwa mujibu wa Ibara ya 5(3) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977*, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina dhamana ya kutayarisha na kutunza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lenye kuandikisha kila raia mwenye sifa za kupiga kura na kutunza taarifa zake. Tume ya Uchaguzi imepewa jukumu hilo kupitia Ibara ya 5 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na vifungu vya 11, 12 na 15 (5) vya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa Sura ya 343, na kwa Uchaguzi wa Madiwani kupitia vifungu vya 15 B na 21 vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.
[30] Gazeti la Nipashe Juni 10, 2015 ukurasa 25

Ilibainika kuwa pamoja na matatizo ya mashine baadhi ya waandikishaji hawakuwa na uelewa wa kutosha kutumia mashine hizo. Walipohojiwa baadhi walikiri kwamba wamepewa mafunzo siku moja kabla ya kuanza uandikishaji huku wakiwa hawajawahi kutumia kompyuta wala kuwa na ujuzi wa TEHAMA (ICT). Hali hii ilisababisha uandikishaji wa wapiga kura kuchukua muda mrefu katika baadhi ya vituo hivyo kuathiri makundi ya watu wenye mahitaji maalum. Aidha, kutokana na mapungufu ya utaalam wa kutumia mashine hizo, baadhi ya vitambulisho vilikosewa wakati mwingine kusajili mwananchi kwa kutumia jina au utambulisho wa jinsia kuwa tofauti na picha ya mwenye kitambulisho.




***Picha ya kitambulisho cha mpiga kura inayonyesha sura ya mwanaume ikiwa na jina la mwanamke (Hadija)***

### 2.8.2 Uchaguzi mkuu wa 2015

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ulihusisha vyama 18 kwenye nafasi za ubunge na vyama 8 katika nafasi ya Rais wa Jamhuri wa Muungano ambapo zaidi ya Watanzania milioni 23 walijiandikisha kupiga kura. Vyama vilivyoshiriki ni pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Civic United Front (CUF), *National Convention for Construction and Reform* Mageuzi (NCCR-Mageuzi), ACT Wazalendo, UPDP, *Tanzania Labour Party (TLP), United Democratic Party (UDP), Chama cha Ukombozi wa Umma (*CHAUMA), National Reconstuction Alliance (NRA) na ACT Wazalendo. Hata hivyo vyama vinne vilivyoamua kushirikiana na kujinadi kama Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) viliungana na kumsimamisha mgombea mmoja wa Urais. Vyama hivyo ni pamoja na CHADEMA, CUF, NCCR Mageuzi na NLD.

#### *2.8.2.1 Kampeni za Uchaguzi*

Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, Sheria ya Gharama za Uchaguzi, ya mwaka 2010 na Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zinatoa maelekezo kuhusu masuala mbalimbali ya uchaguzi nchini.Kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 zilichukua siku 64 ambazo wagombea walijinadi kabla ya siku ya Uchaguzi tarehe 25 Oktoba, 2015. Suala la kulinda usalama wa raia

na mali zao ni jukumu la Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi sura ya 322. Kuwepo kwa vikundi vya ulinzi vya vyama kunawezesha mazingira ya kutokea kwa vurugu hasa pale vikundi hivi vinapoamua kushambulia vikundi vya vyama vingine kwa madai ya kulinda vyama vyao. Jeshi la Polisi lilifanya kazi na kuhakikisha mikutano mingi hasa ya wagombea wa Urais iliyokusanya watu wengi ilikwisha bila vurugu.

i. Kulikuwa na ratiba ya kampeni za wagombea urais ambayo ilizingatiwa na vyama vingi. Hata hivyo kuna wakati ilifanyiwa marekebisho ya hapa na pale;
ii. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa matamko ya mara kwa mara kwa lengo la kuonya pale kanuni zilipokiukwa na maadili na wakati mwingine kutoa ufafanuzi pale walipohitajika.
iii. Jeshi la Polisi lilishiriki kikamilifu katika kulinda usalama wakati wa kampeni na katika uchaguzi

Changamoto mbalimbali zilijitokeza ikiwa ni pamoja baadhi ya wagombea kutumia lugha za kejeli, vijembe na matusi katika majukwaa hivyo kupewa onyo na Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwa kushauri vyama vya siasa kuzingatia maadili ya uchaguzi.[31] Hali kadhalika ilionekana baadhi ya vyama vilikiuka kanuni za maadili ya uchaguzi zinazo simamia muda wa kuanza na kukamilisha kampeni .

***2.8.2.2 Kupiga kura, hesabu na kutangaza matokeo***

Taasisi mbali mbali za nje na ndani ya nchi zilijitokeza kuwa waangalizi na wafuatiliaji wa uchaguzi huo kwa mujibu wa sheria za ndani zinazosimamia uchaguzi na makubaliano ya kikanda na kimataifa.[32] Tume ilikishirikiana na Mtandao wa Asasi za Kiraia uitwao Policy Forumkama taasisi za ndani kufuatlia uchaguzi huo katika vituo 576 vya kupigia kura katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mwanza.[33] Kwa mujibu wa taarifa ya ufuatiliaji upigaji kura ulikuwa shwari kwa vituo vya kufunguliwa kwa muda uliopangwa, kuwepo vifaa vya kupigia kura, ulinzi na amani na wapiga kura kujitokeza kwa idadi kubwa. Hata hivyo mapungufu kama vile baadhi ya vituo kuchelewa kufunguliwa, na vingine havikufunguliwa kabisa kutokana na kutokuwepo kwa vifaa au wasimamizi wa vituo kutofika kwa wakati kuliathiri zoezi la upigaji kura kutofanyika kwa muda muafaka katika baadhi ya maeneo.[34]

Taratibu za kuhesabu kura zilianza baada ya kufungwa kwa vituo na matoleo yalianza kutolewa baada ya kumalizika kujaza fomu muhimu zilizokuwepo vituoni. Matokeo yaliendelea kutolewa ingawa kulikuwa na kucheleweshwa katika baadhi ya majimbo. Kwa mfano katika mkoa wa Dare Salaam, matokeo katika majimbo ya Segerea, Kawe, Mbagala, Ilala, Kinondoni, na Mbagala, yalichelelewa hivyo kusababishwa vurugu za hapa na pale japo zilidhibitiwa.

Pamoja na kuwa baadhi ya sheria zinazoruhusu mfumo wa kidemokrasia, Tume ilibaini kuwa mfumo wa sheria uliopo una mapungufu yanayozuia wananchi kutumia haki zao za kidemokrasia kwa ukamilifu. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni pamoja na:

[31] *Sheria ya Kanuni ya Adhabu, (Penal Code Cap 16), na Maadili ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani ya mwaka 2015, chini ya kifungu cha 124A cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 vinakataza matumizi ya lugha za kuudhi na kudhalilisha watu wengine kwa namna yeyote ile.*

[32] Waangalizi walitoka kwenye jumuiya za SADC, EU, EAC,AU

[33] Kifungu cha 6(1) (m) cha Sheria Na. 7/2001 kinairuhusu Tume kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali na zisizo za serikali.

[34] Vituo vya EDP Royal katika Jimbo la Kibamba mkoa wa Dar es Salaam.

1. Kutoruhusiwa wagombea binafsi katika ngazi zote za uchaguzi kinyume na sheria [35]
2. Kutoruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani;[36]
3. Uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi unaweza kuathiriwa kutokana na namna wajumbe wake na viongozi na watendaji wakuu wa Tume hiyo wanavyoteuliwa. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, wajumbe, na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
4. Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri za Wilaya, ambao ni watendaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa wasimamizi wa uchaguzi kwenye wilaya. Hawa ni watendaji ambao kiutawala ni watumishi wa dola, na hawajibiki moja kwa moja kwa
5. Tume ya Uchaguzi Makundi ya watu wenye ulemavu walilalamika kutotendewa haki na kupewa fursa sawa na watu wasio na ulemavu. Kwa mfano baadhi ya mikutano ya wagombea haikuwa na wakalimani wa lugha za alama, jambo ambalo liliwafanya watu wenye ulemavu wa kusikia washindwe kusikiliza sera za wagombea.

Baada ya kufanya uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa katika ufuatiliaji, Tume inatoa mapendekezo yafuatayo:-

i. Viongozi wa vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine wote wa uchaguzi kuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi katika kipindi chote cha uchaguzi kutotumia lugha zinazoweza kusababisha uvunjwaji wa haki za binadamu.
ii. Mfumo wa Sheria za uchaguzi upitiwe ili kuruhusu uwepo wa wagombea binafsi katika ngazi zote.
iii. Mfumo wa sheria za uchaguzi uruhusu matokeo ya urais kupingwa mahakamani.
iv. Utaratibu wa uteuzi wa viongozi na watendaji wakuu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ushirikishe wadau wa uchaguzi kama vile serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia na mashirika ya dini ili kuongeza imani ya wadau hao kuhusu uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Aidha, kinga ya viongozi na watendaji wakuu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi iwe kama ya Majaji ili kuongeza uhuru wao katika utendaji.
v. Vyama vya siasa na wadau wngine wa uchaguzi washirikishwe katika kupanga na kutoa vibali vya mikutano ya kampeni, ili kuepusha migongano kati ya vyama, wanachama na washabiki wa vyama.
vi. Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali na binafsi, iongeze muda na rasilimali katika kutoa elimu ya mpiga kura kama njia ya kuboresha demokrasia.

## 2.9 Haki ya Kufanya kazi

Ibara ya 22 na ya 23 zinatambua haki ya kila mtu kufanya kazi na kupata ujira unaolingana na kazi yake. Aidha kila raia anastahili fursa na haki sawa kwa masharti ya usawa kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi. Haki hii inasomwa pamoja na

[35]Ibara ya 39(2) na 67(1) (b) za *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* na Kifungu cha 39(1) (f) cha *Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa*, ili mwananchi atekeleze haki yake ya kupigiwa kura kama Rais, Mbunge au Diwani anatakiwa awe ni mwananchama wa chama cha siasa na awe amependekezwa na chama chake kuwa mgombea wa nafasi husika

[36] Ibara ya 41(7) ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania*, ya mwaka 1977

haki zilizoko katika Ibara 13 inazotoa haki ya utu, usawa na kutobaguliwa, kutofanyishwa kazi za kutweza au utumwa.

Ibara hizo ndiyo msingi wa kupatikana haki ya ustawi wa jamii na hifadhi ya jamii, kama zilivyotungwa katka sheria za kazi, na Sheria za Mifuko ya Jamii. Kwa mantiki hiyo Tume imefuatilia malalamiko ya wafanyakazi katika taasisi mbalimbali kuhusu kuvunjiwa haki zao za kiutumishi na kutowasilishwa kwa michango na ucheleweshaji wa malipo katika mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii. Tume ilipokea malalamiko mbalimbali ya wananchi kuhusu ukiukwaji wa taratibu za ajira zinazofanywa na waajiri ambapo kati ya malalamiko **1,538**, yaliyoshugulikiwa na Tume, malalamiko **370 (24.05%)** yalihusu ajira na nidhamu. Malalamiko hayo ni pamoja na kusimamishwa kazi kionevu, kutolipwa mapunjo ya mishahara, kuvuliwa madaraka, kunyimwa stahili, kutopandishwa vyeo, na kutorudishwa kazini.

Tume inatoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha haki hii ya kufanya kazi.

1) Serikali na vyombo au Taasisi zake ziandae mazingira ambayo yatamuwezesha mwaajiriwa aweze kutimiza wajibu wake kwa kadiri ya ujuzi na uelewa wa fani ya mhusika, masuala ya mikataba, mishahara, likizo na uchangiaji kwenye mifuko ya jamii uwekwe uwazi ili mwanachama ahamasike kujiunga.

2) Mifuko ya jamii ihakikishe mnufaika wa kwanza katika mifuko hii ni mwanachama kwanza na shughuli nyingine ziangalie vipaumbele vya mfuko husika.

3) Kuwapo na utoaji mikopo yenye riba nafuu kwa mwanachama ili kila mwanachama aweze kuwekeza wakati bado ana nguvu za uzalishaji.

4) Mafao ya wastaafu yatolewe kwa wakati pindi mfanyakazi anapofikia kikomo ya muda wa kuendelea kufanya kazi kwa sasa imekuwa ni usumbufu kwa vile mstaafu anaweza kukaa zaidi ya miezi nane 8 hajapata mafao yake. Hali hii inaweza kudhalilisha utu wa mtumishi aliyetumikia Serikali kwa kipindi chote cha maisha yake wakati akiwa na nguvu za kuzalisha kwa tija.

5) Serikali na wadau wa sekta binafsi waandae mazingira rafiki ya kuwaajiri watu wenye ulemavu kulingana na ujuzi na fani walizosomea. Na hii ilitiliwa mkazo kuzignatia Sera na Sheria ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010, ambayo imetumika wazi kila mwaajiri atenge nafasi kadhaa kwa watu wenye ulemavu endapo watajitokeza kuomba kazi na sifa wanazo waajiriwe.

6) Elimu ya Sheria ya kazi itolewe kwa viongozi, watendaji wakuu na wafanyakazi ili kila mmoja awajibike kwa nafasi yake katika kuchukua hatua stahiki kwa mtumishi anayetakiwa kupatiwa haki yake au adhabu kwa mujibu wa sheria.

## 2.10 Haki ya kumiliki mali

Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali ya kila mtu kwa mujibu wa sheria. Ibara pia inapiga marufuku mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengine bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili.

Tume ilifuatilia kwa ukaribu migogoro inayojitokeza katika miliki na matumizi ya ardhi katika maeneo mbali mbali nchini. Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaeleza kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria. Haki hizi zinahusu matumizi na umiliki wa ardhi. Mwaka 2015/2016 kulikuwepo na taarifa za migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini yakihusisha; wananchi na wawekezaji, wakulima na wafugaji, wananchi na taasisi mbalimbali na malalamiko ya wananchi na serikali pale maeneo yanapotwaliwa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa maoni ya Tume migogoro ya ardhi nchini inasababishwa na mambo makuu yafuatayo;-

### 2.10.1 Matumizi mabaya ya madaraka katika mgawanyo wa umiliki wa ardhi

Uchunguzi wa Tume ulibaini kuwa migogoro ya Umiliki na matumizi ya ardhi unatokana na matumizi mabaya ya mamlaka waliyopewa baadhi ya watendaji. Baadhi ya watendaji hao wamechukuwa maeneo ya wananchi bila ridhaa, bila kulipa au kwa fidia ndogo na kubadilisha matumizi ya ardhi bila kushirikisha wananchi.

**Lalamiko Na. UB/S/2012/05/06/2012**

Lalamiko hili lililetwa dhidi ya Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Mlalamikaji aliyedai kutolipwa fidia stahiki ya eneo lake la ukubwa wa hekari 2.6 badala ya hekari 0.8 ambazo serikali ilidai kuwa ndilo eneo lake, katika Kiwanja na 192, Kitalu 2 Mradi wa Viwanja 20,000, Mwanagati, Kitunda, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam. Mlalamikaji pia alilalamika kuwa mmoja wa watendaji wa Wizara alijipatia viwanja katika eneo lake, kwa kutumia wadhifa wake, eneo ambalo awali liliotengwa kuwa shule ya sekondari, akaliuza kwa mwekezaji bila kufuata taratibu, na baadaye lilijengwa nyumba za kupangisha kinyume na matumizi ya kujengwa shule. Aidha, mlalamikaji alidai kuwa mtendaji huyo alitumia madaraka yake vibaya kwa kumbambikizia kesi ya jinai na kuvunja nyumba yake, mambo ambayo mtendaji huyo aliyafanya ili kumwezesha kuchuka eneo la shule ambalo awali lilikuwa eneo la mlalamikaji.

Uchunguzi wa Tume uliokamilishwa tarehe 11/12/2015 ulibaini kwamba eneo la Mlalamikaji lilikuwa heka 2.6 na si hekari 0.8. Kwa hiyo Mlalamikaji alistahili fidia ya kiasi ambacho hakulipwa na serikali cha hekari 1.8. Kuhusu madai ya matumizi mabaya

ya madaraka Tume iliishauri Wizara imchukulie hatua mtendaji husika kwa kutumia madaraka yake vibaya na kufuta hati miliki ya kiwanja alichokiuza. Tume haijajulishwa na Wizara iwapo mapendekezo hayo yalitekelezwa.

**Lalamiko 00830/2014/15:**

Mgogoro mwingine uliosababishwa namatumizi mabaya ya madaraka ni mgogoro wa Kijiji cha Mabwegere, wilaya ya Kilosa katika mkoa wa Morogoro. Katika mgogoro huu mlalamikaji analalamikia uongozi wa Wilaya ya Kilosa na mkoa wa Morogoro kushindwa kutekeleza amri ya Mahakama ya Rufaa katika Shauri Na. 53/2010 iliyotambua uhalali wa Kijiji cha Mabwegere na wajibu wa Wilaya ya Kilosa kutambua mipaka ya kijiji hicho.

Huu ni mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Mabwegere na Vijiji vya Mbigiri, Mfulu na Mabengwa wilayani Kilosa, mkoani Morogoro.Uchunguzi ulifanyika kati ya tarehe 24/08/2015 na 12/08/2016. Kiini cha mgogoro huu ni ugomvi wa matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, ugomvi ambao ulisababisha mapigano na uvunjifu wa amani, uharibifu wa mali za wananchi na hata tuhuma za kubakwa wanawake wa jamii ya wafugaji mara kadhaa. Katika mgogoro huo pia viongozi wa wilaya na mkoa wanatuhumiwa kwa kushindwa kutekeleza amri ya Mahakama ya Rufaa katika Shauri Na 53/2010 iliyotambua uhalali wa Kijiji cha Mabwegere na wajibu wa Wilaya ya Kilosa kutambua mipaka ya kijiji hicho cha wafugaji.

Aidha Tume ilipendekeza umuhimu wa kuheshimu hukumu ya mahakama ya Rufaa ambayo ndiyo mahakama ya juu nchini, na kuwepo mpango endelevu wa matumizi ya ardhi katika vijiji hivyo. Pamoja na mapendekezo hayo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliunda Tume nyingine kuchunguza mgogoro huo.

### 2.10.2 Kutokuwepo kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi na uwekezaji

Tume ilibaini kuwa ongezeko la migogoro ya matumizi na umiliki wa ardhi nchini kati ya wakulima na wafugaji ni kutokana na ukweli kwamba wote wanahitaji ardhi kwa maendeleo ya kiuchumi. Uhitaji na kukosekana kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi kumezaa kutoaminiana miongoni mwao na hivyo kila kundi kuliona kundi pinzani kama mvamizi wa ardhi na halina haki kimsingi kuendelea kutumia ardhi inayogombaniwa. Wakati wakulima wakihitaji maeneo zaidi kwa kilimo, wafugaji wanahitaji maeneo zaidi ya kulisha mifugo yao. Pia, wafugaji wamekuwa wakihama hama kutafuta malisho ya mifugo yao kutokana na ardhi kubadilishwa matumizi kwa ajili ya upanuzi wa hifadhi na shughuli za uwekezaji, pamoja na mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri upatikanaji wa malisho na maji.

Aidha, kumekuwa na matukio yanayohusu watu kunyanganywa mali kwa madhumuni ya shughuli za maendeleo pasipo kulipwa fidia na ushirikishwaji wa jamii husika ambapo baadhi ya malalamiko yalipokelewa Tume kuhusu uvunjwaji wa haki hii. Kwa mfano migogoro ya

umiliki na matumizi ya ardhi na ubomoaji wa nyumba za wananchi kupisha miradi ya maendeleo.

**Mgogoro wa Ardhi katika wilaya ya Karatu:**
Uchunguzi wa hadharani (public inquiry) ulifanyika wilaya ya Karatu katika vijiji vya Qangdeng, na Endamaghan kati ya tarehe 25 na 28 Agosti 2015. Mgogoro katika vijiji hivi ulihusu malalamiko ya jamii ya Wahadzabe dhidi ya wakulima wa vitunguu na wafugaji waliovamia maeneo yao ya asili. Mgogoro mwingine ulikuwa baina ya Wahadzabe na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Area Authority), na pia wakulima wa vijiji vya Tloma na Ayalabe na hifadhi ya Ngorongoro waliodaiwa kupanua mipaka ya hifadhi bila ya kuwashirikisha na kutowalipa fidia ya uharabifu wa mazao yao kutokana na wanyama. Tume ilipendekeza kwa mamlaka kuwa itenge eneo la jamii ya Wahdzabe kwa kuwapa hati miliki ya jamii ili eneo lao lilindwe kisheria, na mgogoro wa mipaka ya Kijiji cha Endhamaghan na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro utatuliwe. Kuhusu migogoro inayohusu wakulima ilipendekezwa kuwa mipango ya matumizi bora ya ardhi iandaliwe na mipaka iheshimiwe na pande zote zinazohusika. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iwalipe fidia wakulima wanapoathirika kutokana na wanyama kuharibu mazao yao.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ya Sheria za Tanzania toleo la 2002, ardhi ni mali ya umma. Hata hivyo Ibara ya 24(1) ya Katiba ikisomwa pamoja na Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Ardhi vinaainisha kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki ardhi na haki ya hifadhi ya ardhi anayomiliki kwa mujibu wa sheria. Aidha, Ibara ya 24 (2) inakataza mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kutaifisha au madhumuni mengine kinyume na sheria na bila kulipwa fidia.

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Sura ya 118 ya Sheria za Tanzania (2002) kimempa Rais wa Jamhuri madaraka ya kutwaa au kuhaulisha ardhi kwa manufaa ya umma. Kifungu cha 11 cha Sheria hii kinaeleza kuwa kila mtu ambaye ardhi yake imetwaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 anatakiwa kulipwa fidia. Aidha kifungu cha 13(2) na (3) cha Kanuni za Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa Ajili ya Fidia) 2001 vinahitaji malipo ya fidia kufanyika ndani ya miezi sita tangu ardhi itangazwe kutwaliwa na kwamba iwapo fidia hiyo haitalipwa ndani ya muda huo, itabidi malipo hayo yafanyike pamoja na riba.
Hivyo kutokana na vifungu hivyo utwaaji wa ardhi ya wananchi pasipo kuwalipa fidia ni ukiukwaji wa haki za kumiliki mali.

### 2.10.3 Jamii kutokutimiza wajibu wake wa kulinda rasilimali za Taifa
Tume inapenda kusisitiza kuwa haki na wajibu ni sehemu mbili za shilingi. Hakuna haki isiyo na wajibu. Wajibu wa jamii umeainishwa katika Ibara ya 25 hadi ya 28 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara ya 25 ya Katiba inazungumzia umuhimu wa kila mtu kufanya kazi kwa ajili ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii, kwa kuwa kazi ndiyo msingi na kipimo cha utu.

Tume imeona pia idadi ya raia (makundi na raia mmoja mmoja wanaokiuka sheria na taratibu na kuvamia au kujitwalia ardhi inaongezeka. Aidha, wakulima wamekuwa wakivamia maeneo

yaliyozuiwa kisheria kama vile hifadhi za taifa, vyanzo vya maji, maeneo yaliyotengwa kwa shughuli nyingine  kwa ajili ya kilimo. Hali kadhalika wafugaji wamekuwa wakivamia na kuingiza mifugo yao katika maeneo yaliyozuiliwa kisheria. Wafanya biashara nao wanavamia misitu na maeneo yaliyozuiwa kwa sheria na kuvuna mazao(mbao na miti), uwindaji na uchimbaji madini haramu. Katika maeneo ya mijini, uvamizi wa maeneo ya wazi, viwanja wa taasisi na mradi ya maendeleo (kama vile kando ya barabara), maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji, vyanzo vya maji na maeneo yaliyotamkwa kama hatarishi

Tume inasisitiza kuwa ni wajibu wa kila raia kulinda na kutii Katiba na sheria za nchi kulinda rasilimali za taifa, mali za mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [37].Ni wajibu wa wananchi wote waishio nchini kuheshimu mali binafsi, na kupiga vita uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi kwa faida ya wote. Katika misingi hiyo utii wa sheria, vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, uharibifu wa mali na rasilimali za taifa na ufisadi ni jukumu la kila mtu.[38]

## 2.11 Wajibu wa jamii katika kulinda usalama na amani

Katiba pia inatoa wajibu kwa raia kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa taifa, na mamlaka ya Bunge kutunga sheria zitakazowawezesha wananchi kutumikia katika majeshi ya ulinzi wa taifa. Pia Ibara hii inasisitiza ulinzi wananchi dhidi ya uvamizi na haki ya raia kupigana vita na kulinda taifa na kutamka kuhusu kosa la uhaini kuwa ni kosa la juu kabisa kwa mujibu wa sheria ya nchi.

Pamoja na uwepo wa ibara hizi muhimu ambazo zinatoa wajibu kwa raia wa Tanzania, bado kuna changamoto mbalimbali zilizojitokeza zilizoonesha kuwa baadhi ya raia hawakutekeleza wajibu wao kwa mfano kuvamia vituo vya polisi, kujenga/kuharibu vianzo vya maji, ujangili, mauaji ya watu wenye ualbino

Moja ya majukumu ya Jeshi la Polisi nchini ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo usalama kwa askari uliathiriwa na matukio mbalimbali ya kuvamiwa kwa vituo vya polisi, kuua askari pamoja na kuporwa silaha. Katika kipindi hiki kulikuwa na matukio sita ambapo jumla ya askari wanne na raia mmoja waliuawa ambapo silaha 22 na risasi 273 ziliporwa katika vituo. Jeshi la Polisi limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 17[39] waliohusika na uvamizi wa vituo na kupata silaha zote zilizoporwa katika vituo vya Stakishari, Tanga na Ikwiriri. Katika tukio la Stakishari silaha 14 zilizoporwa zilikamatwa ambapo watuhumiwa 13 walikamatwa walifikishwa mahakamani. Katika tukio lililotokea Tanga silaha mbili zilizoporwa zote zilikamatwa ambapo mtuhumiwa mmoja alikamatwa na kufikishwa mahakamani. Aidha, katika tukio la Ikwiriri silaha 6 na risasi 273 zilizoporwa zote zilikamatwa na watuhumiwa watatu walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Matukio yanayoendelea ya walinzi kuvamiwa wao binafsi na kuporwa silaha siyo dalili njema kwa amani ya nchi na usalama wa raia wenyewe. Pamoja na Tume kulaani vitendo hivi vya kuvamia vituo vya polisi ambavyo vinaambatana na uvunjifu wa haki za binadamu pia, inawakumbusha raia wajibu wao wa kutoa taarifa pale wanapoona dalili au vitendo hivi kwa ajili kudumisha hali ya ulinzi na usalama nchini. Aidha ushauri unatolewa kwa Jeshi la Polisi

[37] Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977
[38] Ibara ya 27 ya Katiba
[39] Taarifa ya waziri wa mambo ya ndani alipokuwa akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017

kuendelea kushirikiana na wananchi katika maeneo mbalimbali ili kupata taarifa za awali za uvamizi huu na kuficha siri za raia wema wanaotoa taarifa kuzia uhalifu usitokee katika maeneo yao. Jeshi pia lifanye uchunguzi wa kina kujua sababu za vamizi hizi na kufanyia kazi matokeo ya tafiti hizo badala ya kuendelea kutoa vitisho ambavyo vinachangia uadui kati ya polisi na jamii katika maeneo husika.

## 2.12 Hifadhi ya Haki za Makundi Maalum

Makundi maalum kwa mtazamo wa haki za binadamu, ni makundi ambayo kwa sababu ya nafasi zao kijamii, kiuchumi au kimwili wanaweza kuwa waathiriwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu hivyo haki zake zinahitaji kupewa kipaumbele. Makundi hayo ni pamoja na wanawake na wasichana, watoto, wakimbizi, watu waliopoteza makazi nchini mwao (internally displaced persons- IDPs), watu wasiokuwa na uraia, watu wanaoishi maisha ya asili, wafanyakazi wahamiaji (migrant workers), watu wenye ulemavu, wazee na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.[40] Nchini Tanzania, haki za makundi maalum zinalindwa na sera, sheria na mipango ya maendeleo kwa kundi husika.

### 2.12.2 Haki za Wanawake

Haki za wanawake zinalindwa kupitia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, Kikanda ambayo Tanzania imeridhia[41]. Mipango na maazimio ya Kimataifa kama vile "*The Beijing Declaration and Plan of Action ya mwaka 1995*[42] na "Solemn Declaration on Gender Equality"[43] ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2004 yote yanazitaka nchi wanachama, ikiwemo Tanzania, kuhakikisha haki sawa kwa wanawake, kwa kuchukua hatua zinazohakikisha haki hizo.

Kitaifa ulinzi wa haki za wanawake zimeainishwa katika Katiba[44], Sheria kama vile Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya Mwaka 1998, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini 2004 na Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Aidha zipo Sera na Mipango mbalimbali kama vile **Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000;**

---

[40] *Guide to international Procedures available in cases of Human Rights Vilations in Africa*

[41] *Baadhi ya nyaraka hizo ni pamoja na; Tamko la Dunia juu ya Haki za Binadamu, la mwaka 1948, Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Uangamizaji wa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, wa mwaka 1978, Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na za Kisiasa 1966 na Mkataba wa Kimataifa juu ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, wa mwaka 1966. Katika ngazi ya kanda, Umoja wa Afrika nao uliandaa Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Haki za Raia, wa mwaka 1981, ambao kwa mujibu wa Kifungu cha 4 unataka iwepo haki ya kuheshimu maisha ya mtu na hadhi yake. Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Haki za Kiraia, juu ya Haki za Wanawake katika Afrika, 2003ambapo kifungu cha 5 kinataka uangamizaji wa aina zote za vitendo vinavyoathiri haki za wanawake katika Afrika, na Mkataba wa Nyongeza kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika juu ya Jinsia na Maendeleo, wa mwaka 2009.*

[42] *Azimio na Mpango Kazi wa Beijing wa mwaka 1995; Ibara ya 58 ilizungumzia kuhusu umuhimu wa serikali kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika kutekeleza sera za nchi kupiga vita umaskini( full and equal paticpation in macroeconomic and social policies) Ibara ya 80 ilisistiza kuhusu kushiriki wanawake bila ubaguzi katika elimu na kuondoa tofauti za kijinsia katika elimu( equal access to education0 na ibara ya 106 kuhakikisha haki ya wanawake kuwa na afya bora kimwili na kiakili ( highest attainable standard of physical and mental health).*

[43] *Ibara ya 5, 6 na 7 ya Tamko hilo zinasistiza, usawa wa jinsia (gender parity principle) katika uongozi wa vyama, bunge na serikali katika nchi, haki za wanawake kupata maendeleo kisheria (right to development by legislation)na haki ya kumiliki mali na kurithi, (right to land, property and inheritance, etc,) na haki ya elimu kwa wasichana na wasichana mijini na vijijini( education for girls and literacy for women,especially in rural areas.).*

[44] *Ibara ya 12 na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977*

inayolenga kushughulikia kwa usawa kati ya wanaume na wanawake kwa kuhusisha suala la rasilimali, umaskini wa vipato na kuupa thamani mchango wa wanawake katika maendeleo ya Taifa.

Pia iliandaliwa Mipango kadhaa inayolinda haki za wanawake nchini. Mipango hiyo ni pamoja na Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2016/2017-2021/2022 wenye lengo la kutokomeza ubaguzi na unyonyaji wa kisheria, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa unaoathiri wanawake na watoto. Aidha Mpango huu pia unalenga kuongeza juhudi za Serikali kwa kushirikiana na wadau kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuhakikisha usawa na haki kati ya wanawake na wanaume nchini Tanzania.

Pia Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa Mwaka (2013-2017) ambao unalenga katika kuhakikisha kwamba kunakuwepo na haki sawa, mipango na sera zinazomwezesha mwanamke kushiriki kikamilifu katika masuala ya kiuchumi kisiasa na kijamii.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sheria, Sera na Mipango mbalimbali kama vile kuanzishwa kwa madawati ya Wanawake na watoto katika vituo vya polisi, kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya kisera na maamuzi, bado haki za wanawake zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na baadhi ya mifumo ya kijamii, mila, desturi na tamaduni ambazo ni kandamizi. Mifumo hiyo huchangia uvunjifu wa haki za wanawake kutokana na matukio kama vile kupigwa, ukeketaji, unyanyapaa, unyanyasaji, mauaji ya wanawake wazee kwa imani za kishirikina, kubakwa na wakati mwingine kukosa fursa za elimu kutokana na kupata mimba katika umri mdogo na ndoa za utotoni. Hali hii ni kinyume na Ibara ya katiba inayoainisha Haki ya Usawa na heshima ya utu.

Taarifa za utafiti wa Kidemografia *na afya* kwa mwaka 2015/2016 zinaonesha kuwa wanawake wanaofanyiwa vitendo vya ukatili bado ni wengi hasa katika maeneo ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria hususani katika mikoa ya Mara na Shinyanga.[45] Ukatili huo hufanywa na ndugu wa karibu hasa waume na wapenzi wao unajumuisha vipigo, ukatili wa kingono *(sexual violence*) na ukatili unofanywa na mume (*spousal violence*)

**Jedwali Na. 2 Ukatili dhidi ya wanawake miaka 15 – 49**

| **Aina ya Ukatili** | **Asilimia** |
|---|---|
| Vipigo | 40% wanawake umri miaka 15<br>22% ya wanawake walipata vipigo ndani ya miezi 12 iliyopita 2015-16 ambapo 8% ni vipigo wakati wa ujauzito. |
| Ukatili kingono | 17% ya wanawake walifanyiwa ukatili huu<br>9% ya wanawake walifanyiwa ukatili wa kingono ndani ya miezi 12 iliyopita 2015-16, Hasa katika kanda ya Mangaribi na ya Ziwa. |
| Ukatili wa mume (Spousal Violence) | 50% ya wanawake walioolewa wanakumbana na ukatili huu (vipigo, na mateso katika ndoa )<br>38% ya wanawake walipata ukatili huu ndani ya miezi 12 iliyopita |

[45] *Taarifa za Utafiti Wa Kidemografia na Afya Tanzania (Tanzania Degraphic and Health Survey) ya mwaka 2015/2016 iliyotolewa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa(National Bureau of Statistics 2015-16 P.369*

| | |
|---|---|
| | 2015-16<br>Kupiga, kuchomwa moto, kulazimishwa kufanya mapenzi,na kupiga kwa kutumia silaha,Hasa katika kanda ya Mikoa ya kanda ya Ziwa, Mara and Shinyanga kwa 78% |

Chanzo: TDHS-MIS 2015-16

Kutokana na ukubwa wa tatizo hili la ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike, nguvu za pamoja zinahitajika kutoka katika jamii, serikali na asasi za kiraia katika kutoa elimu katika jamii zenye kuendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuachana na mila potofu na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kujipatia maendeleo.

### 2.12.3 Haki za Watoto

Haki za watoto zinalindwa kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda ambayo Tanzania iliridhia.[46] Kisheria ulinzi na ustawi wa mtoto umeaninishwa katika Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004). Kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kinaeleza kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane (18). Aidha ulinzi wa haki za mtoto umeainishwa katika Sera ya Mtoto (2008); Sera ya Afya (1990/2002) yenye nia ya kuwalinda kinamama na watoto kwa kupitia upunguzaji wa kiasi cha vifo vya mama na mtoto na Sera ya Ajira (2004) inayoshughulikia masuala ya ajira ya watoto kulingana na masharti ya Shirika la Kazi Duniani.

Upatikanaji wa haki na ustawi wa mtoto umezingatiwa katika baadhi ya mipango na miongozo kama vile Mpango mkakati wa haki za Mtoto (*Child Justice Strategy)* 2013-2016 wenye lengo la kuhakikishwa upatikanaji wa haki sawa na kwa haraka kwa watoto walio katika mkinzano na sheria, na Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2016/2017-2021/2022) wenye lengo la kutokomeza ubaguzi na unyonyaji wa kisheria, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa unaoathiri wanawake na watoto.

Pamoja na kuwepo mifumo thabiti ya kulinda haki za mtoto na mafanikio yaliyojitokeza kama vile kuongezeka kwa wanafunzi kutokana na suala la elimu kuwa bure, bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokabili ulinzi na utekelezaji wa haki za mtoto nchini. Changamoto hizo ni pamoja na; kukinzana kwa sheria, ukatili, ndoa za utotoni, mimba katika umri mdogo na ukeketaji.

Imekuwa ni vigumu kupata takwimu halisi za ukatili wanaofanyiwa watoto hasa kwa maeneo ya vijijini. Ukatili mwingine umeishia kwenye vyombo vya sheria, kuhalalishwa au suluhu katika vyombo visivyo rasmi (Kama vile familia, koo na mabaraza ya kimila), na mengine yamefichwa au kunyaziwa baada ya familia au watendewa kutishiwa, kukosa mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao au hofu za kutengwa au kuona aibu. Aidha, takwimu za malalamiko ya ukatili kwa watoto yanakosekana kutokana na mapungufu katika mifumo ya kukusanya na kufuatilia malalamiko na haki za watoto nchini. Tume imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali ya ukiukwaji wa haki za watoto kutoka kwa wazazi kwa niaba ya watoto na mengine kutoka wadau

[46] Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) NA Mkataba wa Afrika kuhusu haki na Ustawi wa Mtoto.

mbalimbali wanaoshughulikia masuala ya haki za watoto. Kwa mwaka 2015/2016, Tume ilipokea malalamiko 16 kuhusu uvunjwaji wa haki za watoto. Malalamiko hayo yalihusu matunzo ya watoto, watoto kutelekezwa, kubakwa, kulawitiwa na vipigo.

### *2.12.3.1 Kukinzana kwa baadhi sheria zinazolinda haki za watoto*

Pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, bado kuna tatizo la kukinzana kwa sheria zinazotambua haki za mtoto. Kwa mfano wakati sheria ya mtoto ikimtambua mtoto ni mtu mwenye umri wa miaka 18, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inatambua ndoa za watoto katika umri wa wa miaka 14 kwa ridhaa ya mahakama na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi.[47] Kukinzana kwa sheria hizi kunapelekea watoto kuolewa katika umri mdogo na kukosa haki zao nyingine kama vile haki ya elimu.

Kutokana na mapungufu yaliyoko kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, mwaka 1994, Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania ilishauri marekebisho ya Sheria kuongeza umri wa kuolewa kuwa miaka 21 kwa watoto wa kike na kiume. THBUB inaishauri serikali ifanyiwe marekebisho Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 hususan kifungu cha 13 na 17 ili iweze kukidhi matakwa ya sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

### *2.12.3.2 Ukatili dhidi ya Watoto*

Taarifa ya utafiti uliofanywa na UNICEF kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwaka 2009 ilionesha kuwa watoto ni waathiriwa wa ukatili, utumikishwaji wa watoto, ubakaji na ulawiti, ndoa za lazima katika umri mdogo, ukeketaji, mateso, na unyama kwa watoto.[48] Kwa mujibu wa taarifa za Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) nchini Tanzania, matukio haya ya ukatili dhidi ya watoto yameendelea kuwepo hata katika kipindi hiki cha taarifa.[49] Kwa upande wa matukio ya ukatili wa ukeketaji yanataarifiwa kufanyika ambapo asilimia 35 walikeketwa wakiwa na umri wa mwaka mmoja na asilimia 28 katika umri wa miaka 13 ua umri mkubwa.[50] Takwimu zinabainisha kuwa mikoa inayoongoza kwa ukeketaji ni Manyara (58%), Dodoma (47%), Arusha (41%) Mara (32%) na Singida (31%).[51]

### *2.12.3.3 Ndoa na Mimba katika umri mdogo*

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inatoa mwanya wa kuruhusu ndoa kwa wasichana kwa miaka 14 na 15.[52] Uwepo wa vipengele hivi katika sheria umekuwa ukichangia watoto kuolewa wakiwa katika umri mdogo kinyume na sheria ya mtoto inayotambua umri wa mtoto kuwa chini ya miaka 18. Utafiti wa Demografia na Afya Tanzania wa 2016 (TDHS) unaonyesha kwamba asilimia 36 ya wasichana wenye umri wa kati ya miaka 20 na 24 waliolewa kabla ya kufikia umri wa miaka 18.[53]

---

[47] Kifungu cha 13 na 17
[48] *Taarifa Kuhusu Ukatili dhidi ya watoto ya mwaka 2009 iliyoratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na watoto.*
[49] *TDHS-MIS 2015-16*
[50] *Kama hapo awali*
[51] *Kama hapo awali*
[52] Kifungu cha 13 na 17
[53] *TDHS-MIS 2015-16*

Katika kukabiliana na mapungufu ya kisheria yanayosababisha uvunjifu wa haki za mtoto wa kike, taasisi ya Msichana Initiative ilifungua kesi Mahakama Kuu  kupinga umri wa mtoto kuolewa.[54]

***Januari 2016, Msichana Initiative, asasi isiyokuwa ya kiserikali inayosimamia haki za watoto wa kike ilipeleka shauri la Kikatiba Mahakama Kuu ya Tanzania[55] kupinga vipengele vinavyoruhusu watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo. Katika maamuzi ya kihistoria, Mahakama Kuu ya Tanzania ilitoa hukumu iliyotamka kwamba vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 vinakiuka Katiba na kumuagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kurekebisha sheria hiyo  na kuongeza umri  unaofaa kwa ndoa kwa wanaume na wanawake kuwa miaka 18.[56]***

### *2.12.3.4 Watoto walio katika Mkinzano na Sheria*

Watoto walio katika mkinzano na sheria ni kundi ambalo ulinzi na uhifadhi wa haki zao unahitaji kupewa kipaumbele. Haki za kundi hili zinalindwa kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda.[57] Kitaifa haki za watoto walio katika mkinzano na sheria, zinalindwa na *Sheria* ya Mtoto ya mwaka 2009.[58] Sheria hii pamoja na kanuni zake imeanzisha mahakama za watoto, kusimamia mahabusu za watoto na shule ya Maadilisho na kuweka ulinzi thabiti kwa watoto tangu kukamatwa kwao, dhamana, usikilizaji na uendeshaji wa mashauri ya watoto, hukumu zao na wapi wawekwe wakati wanasubiri kusikiliza kesi zao. Aidha Sheria ya Mtoto imevifanyia marekebisho baadhi ya vipengele vya *Kanuni za Adhabu* na *Sheria ya Taratibu za Jinai* ili yawepo maslahi mazuri zaidi ya watoto katika kutoa haki.

Tafiti na kaguzi mbalimbali zilizofanywa na Tume katika magereza na vituo mbalimbali nchini kwa nyakati tofauti zinaonesha kuwa  watoto bado wameendelea kushikiliwa  na kutumikia adhabu za vifungo katika magereza  ya watu wazima, kuchanganywa na wahalifu watu wazima na wakati mwingine kutopatiwa msaada wa kisheria katika kesi zao. [59]

---

[54]*Miscellaneous Civil case No. 5 of 2016 in the matter of a petition to challenge the Contutionality of Section 13 and 17 of  LMA Cap 29 (R.E 2002) between Rebeca Z. Gyumi Vs Atorney General*
54 *Rebeca Z. Gyumi v The Attorney General*, Mahakama Kuu ya Tanzania, Miscellaneous Civil Cause No. 5 of 2016, Judgment, July 08, 2016, http://las.or.tz/wp-content/uploads/2016/07/REBECA-Z.-GYUMI-vs-A.G_Misc-Civil-Cause-No.5-of-2016.compressed.pdf.
[55] *Miscellaneous Civil case No. 5 of 2016 in the matter of a petition to challenge the Contutionality of Section 13 and 17 of  LMA Cap 29 (R.E 2002) between Rebeca Z. Gyumi Vs Atorney General*
56 *Rebeca Z. Gyumi v The Attorney General*, Mahakama Kuu ya Tanzania, Miscellaneous Civil Cause No. 5 of 2016, Judgment, July 08, 2016, http://las.or.tz/wp-content/uploads/2016/07/REBECA-Z.-GYUMI-vs-A.G_Misc-Civil-Cause-No.5-of-2016.compressed.pdf.
[57] Mkataba wa Umoja wa Mataifa Juu ya Haki za Mtoto, wa mwaka 1989, Kiwango cha Umoja wa Mataifa juu ya Kiwango cha Chini cha Kanuni za Kusimamia Uhalifu wa Watoto (Kanuni za Beijing), Kanuni za Umoja wa Mataifa za Kuwalinda Watoto Walionyimwa Uhuru Wao, Miongozo ya Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Uhalifu wa Watoto (Miongozo ya Riyadh), Viwango vya Umoja wa Mataifa juu ya Kanuni za Kiwango cha Chini kwa Hatua za Kutoweka gerezani (Kanuni za Tokyo) na Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Ustawi wa Mtoto (1990).
[58] Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2012-14
[59] Taarifa za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora za ukaguzi wa vizuizi walimozuiwa  watoto kwa 2013 na 2014

### *2.12.3.5 Watoto wanaolelewa katika makao na vituo*

Watoto wanaolelewa katika makao/vituo ni kundi lingine ambalo utekelezaji wa haki zake unahitaji ufuatiliaji wa karibu kulingana na Kifungu cha 4 cha Kanuni za Makao ya Watoto (2012) kinachoainisha haki za mtoto aliye katika makao ya watoto. Tumeilifanya ufuatiliaji katika Makao ya Watoto Kurasini na kituo cha kulelea watoto yatima Mburahati jijini Dar es Salaam kwa lengo la kutathmini hali ya haki za watoto wanaolelewa katika vituo hivyo kulingana na kanuni za makao ya watoto

Katika ufuatiliaji huu zilibainika changamoto za upungufu wa mahitaji muhimu kama vile shuka, nguo za kuvaa, chakula, vifaa vya michezo, tatizo la ada kwa wanafunzi, maji, huduma ya afya, na jamii kutokuwa na utamaduni na hamasa ya kuasili watoto. Aidha makao ya Watoto Kurasini Tume ilitoa mapendekezo yake kwa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto kutenga bajeti ya kutosha. Tume ilishauri Wizara ishirikiane na mashirika ya dini yanayoendesha vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kuboresha huduma zinazotolewa katika vituo hivyo kwa mujibu wa sheria (2009) na kanuni ya makao ya watoto ya Mwaka 2012.

### *2.12.3.5 Tamko la Tume kuboresha haki za watoto nchini*

Katika Tamko ililotoa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika Juni 16, 2016, inasikitishwa na kukerwa na matukio ya ukatili wa aina mbalimbali wanayofanyiwa watoto ambayo yamekuwa yakiripotiwa na vyombo vya habari.[60] Matukio hayo yanajumuisha: kutupwa kwa watoto wachanga, ubakaji, ulawiti, ukeketaji, mauaji, na watoto wa kike kuozwa katika umri mdogo, hivyo kuwanyima haki zao, hususan haki ya kupata elimu. Matendo haya yenye kuvunja haki za watoto yanafanywa na watu wazima wenye akili timamu.

Tume inalaani kwa nguvu zake zote ukatili wa aina yoyote wanaofanyiwa watoto. Hivyo inawataka wananchi kuhakikisha kuwa watoto wote nchini wanapewa malezi na makuzi stahiki katika familia na jamii. Pia wanalindwa dhidi ya vitendo vya unyanyasaji na wanapata fursa katika maendeleo ya ustawi wao. Tume ilitoa wito kwa umma, Serikali na wadau mbalimbali wa haki za watoto kuunganisha nguvu kupinga vitendo vyote vya ukatili wanavyofanyiwa watoto mahali popote Tanzania kwa kuwa watoto ni sehemu muhimu kwa kuwepo, ukuaji na maendeleo ya Taifa lolote.

Tume inawataka Watanzania kuzingatia ukweli kwamba binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa na kwamba kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake kwa mujibu wa Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba ya haki za binadamu ya Umoja wa Afrika (AU) na kimataifa.

Tamko hilo linasisitiza kuwa Tanzania imesaini na kuridhia mikataba ya kimataifa na kikanda na kutunga sheria mbalimbali za kuharamisha makosa ya ukatili dhidi ya binadamu iikiwemo Sheria ya Mtoto, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana hivyo vitendo vya ukatili vikiwemo vitendo vya ubakaji, ulawiti, na ndoa za utotoni ni lazima vikomeshwe. Katika kufuatilia malalamiko ya watoto , Tume imebaini changamoto mbalimbali, zikiwemo:

---

[60] Kumbukumbu ya siku ya mtoto wa Afrika Juni 16, 2016 ikiwa ni mara ya 26 tangu uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) uizindue siku hiyo mwaka 1991

a) Upelelezi wa kesi hizi kuchukuwa muda mrefu, jamii kutokuwa na hamasa ya kupinga vitendo vya ubakaji na ulawiti, na kutowapeleka watoto hospitali mara inapogundulika wametendewa unyama huo, jambo ambalo hupoteza ushahidi.
b) Wahusika huwatishia maisha watoa taarifa, na wakati mwingine kwa kuwa matukio mengi yanawahusisha wanafamilia au watu wa karibu, hivyo ndugu hao hukaa na kusuluhishana nje ya mahakama.
c) Baadhi ya madaktari kutotoa ushirikiano wa kutosha katika mashauri haya, na ucheleweshwaji katika kusikiliza kesi hizi.

Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha haki za watoto:

1. Jeshi la Polisi kupitia Dawati la Jinsia na Watoto kuyapa kipaumbele mashauri yanayohusu ubakaji na ulawiti wa Watoto, kufanya upelelezi thabiti na kuwakamata wahusika, na kuwafikisha mahakamani kujibu mashtaka.
2. Madaktari katika hospitali mbalimbali kuyapa kipaumbele matukio ya ulawiti na ubakaji na kuwasaidia wahanga wa vitendo hivyo, hasa katika kutoa ushahidi mahakamani.
3. Mahakama ziharakishe usikilizaji wa kesi za ubakaji na ulawiti na kutoa hukumu kwa wakati.
4. Wananchi, jamii, kamati za ulinzi na usalama kwa ujumla watoe ushirikiano kwenye vyombo vya sheria kwa kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa watoto kama vile ndoa za utotoni, ubakaji na ulawiti wa watoto.
5. Wazazi na walezi waache kuharibu mwenendo wa mashauri ya ubakaji na ulawiti kwa kukubaliana na wabakaji nje ya vyombo vya sheria hivyo kupoteza ushahidi.
6. Wazazi watakaobainika kulinda uhalifu kwa kutotoa taarifa wachukuliwe hatua za kisheria.
7. Wazazi na walezi wawe makini na mienendo ya watoto ili kubaini mabadiliko ya kitabia.
8. Wazazi/walezi wawe karibu na watoto na kujenga urafiki nao ili kuwafanya waweze kutoa taarifa zozote zisizo za kawaida kwa urahisi.
9. Wazazi/walezi wachunguze mahusiano ya mtoto na jamii ya nyumbani na nje ili kubaini viashiria vya udhalilishaji wa watoto au vitendo vya ukatili na kuvizuia kabla havijatokea.

### 2.12.4 Haki za wazee

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya Wazee **2,449,257** (Wanaume 1,170,323 na Wanawake: 1,278,934) sawa na asilimia 5.6 ya Watanzania wote.[61] Ongezeko la Wazee linaikumbusha na kuihimiza serikali na wadau wote kuchukua hatua za kuboresha maisha ya Wazee wote wa mijini na vijijini.

[61] Taarifa za Msingi za Kigemografia Kijamii na Kiuchumi (2014) Matokeo muhimu sense ya watu na Makazi 2012(NBS)

Mwaka 2002, Umoja wa Mataifa ulipitisha Mpango wa Kimataifa wa Madrid kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka (*Madrid International Plan of Action on Aging* – MIPAA). Lengo la mpango huu ni kuhakikisha kwamba wazee wote ulimwenguni wanapata ulinzi, kuheshimiwa utu wao na wanaendelea kushiriki kikamilifu katika jamii na kupata haki zao za msingi. Mpango wa Madrid umeainisha maeneo matatu ya kipaumbele katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili wazee. Maeneo hayo ni: Wazee na Maendeleo; Huduma bora za Afya na Ustawi wa Jamii uzeeni na Mazingira wezeshi yenye Msaada kwa wazee.

Aidha Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatamka kuwa Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa; na kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake. Aidha, Ibara ya 14 inatamka kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupewa ulinzi wa maisha yake kutoka katika Jamii kwa mujibu wa Sheria za nchi.
Sera ya Taifa ya Wazee (2003) inatoa Dira na Mwongozo kwa wadau mbalimbali katika kulinda, kudumisha na kuimarisha hali ya maisha ya Wazee nchini.

Mijadala iliyofanyika katika maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika, tarehe 21 Oktoba 2015 Dar es Salaam ikishirikisha Tume, wawakilishi wa Wazee na Asasi zinazosimamia haki za wazee kutoka nchi nzima ilibaini kwamba hali ya utekelezaji wa haki na ustawi wa wazee nchini bado hauridhishi.

.



***Mwakilishi wa wazee akiwasilisha maazimio ya warsha ya wadau Kwa Mhe Alli Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya pili siku ya kilele cha maadhimisho ya siku ya haki za binadamu ya Afrika yaliyofanyika New Afrika Hotel 21/10/2015.***

Ilibainika kuwa pamoja na jitihada zinazochukuliwa na serikali na wadau mbalimbali maisha na ustawi wa wazee una changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na:

a) Wazee kutofaidika na mafao mbali mbali ya mifuko ya hifadhi ya jamii,
b) Wazee kutopata huduma muafaka za afya na matibabu bure,
c) kutokuwepo sheria maalum ya kushughulikia haki za wazee,

d) Umaskini wa kipato na hali ya ukali wa maisha kwa wazee,
e) Wazee kutokuwa na uwakilishi katika vyombo na ngazi mbalimbali za maamuzi
f) Ubaguzi na unyanyapaa kwa wazee,
g) Ukatili na mateso kwa wazee,
h) Usalama mdogo na mauaji kwa wazee katika maeneo mbalimbali nchini,
i) Rasilimali na uangalizi hafifu wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makazi ya wazee wasiojiweza

Aidha, pamoja na jitihada za kulinda haki za wazee kupitia Sera ya Taifa ya Wazee (2003) bado kuna taarifa za mauaji na unyanyasaji dhidi ya kundi hilo katika jamii zetu. Kwa mfano katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Machi, 2016[62] jumla ya matukio 222 ya mauaji ya wanawake na wazee yalijitokeza. Katika matukio hayo, wanawake 157 na wanaume 71 waliuawa. Matukio hayo yalitokea katika mikoa ya; Tabora (69), Mbeya (29), Shinyanga (22), Dodoma (11), Rukwa (12), Lindi (9), Geita (13), Simiyu (8), Katavi (7), Morogoro (7), Kigoma (5), Pwani (5), Mara (4), Kagera (3), Mwanza (3), Singida (2), Arusha (8), Songwe (2), Njombe (2) na Ilala (1). Kufuatia matukio hayo watuhumiwa 135 walikamatwa na kufikishwa mahakamani kati ya hao, 20 waliofungwa, 15 walioachiwa huru, 65 walishinda na kesi 35 zinaendelea.[63]

Aidha katika ufuatiliaji uliofanywa na Tume katika kutathmini hali ya ustawi wa wazee wa Nunge iliyoko Kigamboni jijini Dar es Salaam ilibainika kuwa wazee walioko katika kambi hizo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile;

i) Ugumu katika uendeshaji wa kambi hutokana na kuwepo kwa mchanganyiko wa makundi ya watu bila kujali umri tofauti na makusudio ya kuanzishwa kwake ( kambi hii ilianzishwa kwa ajili ya kuhudumia wazee wenye ugonjwa wa ukoma tu)
**ii)** Kambi haina utaratibu wa ukomo wa kukaa hapo"(*Exit Strategy*") na matokeo yake wazee waliohifadhiwa katika kambi kwa muda mrefu wameyageuza makazi ya kudumu na kama yao binafsi na baadhi wakiyarithisha kwa watoto wao.
iii) Rasilimali zinazotolewa na serikali /mamlaka kwa ajili ya kulea wazee hazitoshelezi hivyo huduma kwa wazee kama vile afya na chakula ni duni.
iv) Tatizo la watoto wanaohamishiwa katika kambi ya Nunge wengi bado hawajamaliza masomo ama ngazi ya sekondari au vyuo kushindwa kamalizia masomo kutokana na kukosa mahitaji muhimu ya elimu ambayo hayako katika bajeti ya uendeshaji wa kambi hiyo.
**v)** Jamii na wadau wa haki za binadamu kutokuwa na hamasa ya kutosha kuhusu wajibu wao kwa wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

### 2.12.5 Hali ya haki za watu wanaoishi katika maisha ya asili

Dhana ya watu asilia imekuwa katika mijadala inayoendelea ulimwenguni kuhusu ulinzi na utetezi wa haki zao. Baadhi ya asasi za haki za binadamu nchini zimekuwa na maoni kwamba kwa kuzingatia sifa/vigezo zinazokubalika kimataifa, Tanzania kwa hakika ina jamii za watu

[62] Taarifa ya waziri wa mambo ya ndani alipokuwa akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2016/2017
[63] Kama hapo awali

asilia. Lakini msimamo rasmi wa Serikali katika suala la watu asilia bado ni kwamba' *watanzania wote wenye asili ya Afrika ni watu asilia wa Tanzania'* ingawa inatambua uwepo wa makundi maalum au jamii ambazo zinahitaji ulinzi maalum nchini kama vile Wamasai, Waakiye, Wahadzabe na Wabarbaig.[64]

Tume ilitembelea Jamii ya watu wanaoishi maisha ya asili katika bonde la Yaeda Chini, Wilaya ya Mbulu, kwa lengo la kutathmini hali ya haki za jamii ya Wahadzabe kama kundi mojawapo la watu wanaoishi maisha ya asili na kuona changamoto zinazoikabili jamii hiyo, na kupendekeza mikakati ya kukabiliana nazo

Jamii ya Wahadzabe ni moja ya jamii pekee zilizosalia za wawindaji na wakusanya matunda ulimwenguni. Wahadzabe wanatambulika kama jamii ambayo lengo la maisha yao ni kutafuta nyama pori, mizizi na matunda pori na wala hawana nia ya kumiliki ardhi kwa matumizi mengine. Wahadzabe wamepoteza ardhi yao na misitu ya asili ambao umechukuliwa na jamii nyingine kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na uwekezaji.

Kwa sasa, Tanzania haina sheria maalumu na sera ya taifa kuhusu watu asilia na mipango inazingatia maeneo machache kama vile, maliasili na huduma muhimu za jamii lakini hauzingatii upatikanaji wa ardhi. Kwa watu asilia, maliasili na umiliki wa ardhi ndiyo rasilimali muhimu, Tanzania iliridhia Mkataba wa ILO Namba 29 wa mwaka 2007 na hivyo kupiga kura ya kuunga mkono azimio hilo. Ilifafanuliwa kuwa ukataji wa misitu kwa ajili ya ujenzi na uchomaji wa mkaa umeathiri mazingira na makazi yao kinyume na mfumo wao wa maisha ya asili. Uvamizi wa wafugaji na wakulima umesababisha wahadzabe kusukumwa nje ya maeneo yao na kuishi sehemu za milimani ambazo siyo rafiki kwa makazi yao.

Tume inaona kuwa kuna ukiukwaji wa haki ya jamii ya Wahadzabe kuishi katika mazingira safi na salama kwa kulingana na mfumo wa maisha yao ya asili na mila na desturi zao. Malalamiko yao yanashabihiana na changamoto za kimazingira zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu kama vile ufyekaji wa misitu, kuharibika kwa mifumo ya maji, kutoweka kwa baadhi ya makazi ya wanyama pori na viumbe anuwai na uharibifu wa mazingira.[65]

### *2.12.5.1 Upungufu wa chakula*

Tatizo la mabadiliko ya tabia nchi, na madhara ya shughuli za binadamu lilijitokeza na kuelezwa kuathiri maendeleo ya jamii Wahadzabe. Uoto wa miti ulikuwa wa asili na haukukatwa lakini kulikuwa na ukame. Mabadiliko ya tabia nchi yanaleta madhara kama vile uhaba wa mvua na ukame wa muda mrefu, umesababisha kuhama kwa wanyama wa porini, kukosekana kwa matunda na asali na hivyo tatizo la chakula ambayo hutegemewa na waHadzabe kama vyakula vya asili.

### *2.12.5.2 Haki ya Elimu ya watoto wa Ki-Hadzabe*

Kijiji cha Mongo wa Mono kina shule moja ya msingi na moja ya sekondari ambazo ziko umbali wa Kilometa (7) saba kati yao. Shule hizi zilijengwa na wazazi wa ki-Hadzabe kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya baada ya kuona changamoto ya watoto kwenda shule mbali wakipita

[64] Taarifa ya THBUB UPR ya mwaka 2015/ 2016
[65] Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013 -2017, uk 62 -63

maeneo yenye misitu na wanyama wakali. Hamasa ya elimu kwa watoto wa Hadzabe ilizaa changamoto nyingine kwamba mabweni yaliyojengwa kwa ajili ya watoto hawa yalitumika pia kwa watoto wa jamii zingine, baada watoto wa ki Hadzabe kurudishwa nyumbani kwani wanashindwa kulipa michango kutokana na umaskini. Hata hivyo kwa sasa, hali ya shule hiyo siyo nzuri kwa kuwa mabweni yamechakaa, vitendea kazi hafifu na mazingira ya kufundishia ni magumu.



***Moja ya mabweni ya wanafunzi katika shule ya Msingi ya Mongo wa Mono***

Kwa upande wa shule ya sekondari kulikuwa na tatizo la uhaba wa walimu, wanafunzi wa kike kuacha shule kutokana na mimba za utotoni, uhaba wa vifaa vya kusomea na kufundishia, tatizo la nyumba za walimu na mazingira magumu ya kazi na kutokuwepo kwa mabweni.

#### *2.12.5.3 Huduma za afya*

Suala la upatikanaji wa huduma ya afya lilielezwa kama changamoto kwani hakuna zahanati inayofanya kazi katika eneo lao. Serikali ilikuwa imeanza ujenzi wa zahanati katika eneo lao. Viongozi wa Ki Hadzabe waliomba serikali itoe kipaumbele katika kukamilisha ujenzi wake.



***Jengo la zahanati ambalo halijakamilika***

Huduma ya afya inatolewa na a na Hospitali ya Kilutheri ya Haydom mara moja kwa kila mwezi katika eneo lao. Hata hivyo, elimu ya afya kuhusu janga la Virusi vya Ukimwi na Ukimwi (HIV/AIDS) miongoni mwa jamii ya Wahadzabe ni muhimu ikizingatiwa kuwa muingiliano kati ya jamii ya Ki Hadzabe na wakazi wengine wa wilaya za jirani, mkoa na nchi kwa ujumla ni mkubwa.

#### *2.12.5.4 Nafasi ya Wahadzabe katika utalii*

Jamii ya Wahadzabe inaeleza pia, inatumika kwa biashara ya utalii bila kufaidika. Katika kambi ya Wahadzabe ya Mbuyuni ilielezwa kuwa shughuli za kitalii katika eneo hilo zinaratibiwa na taasisi isiyo ya kiserikali inayoitwa Lake Eyasi Cutural Tourism.



***Sehemu ya picha inayoonyesha ujumbe wa Tume na wananchi wa Jamii ya Wahadzabe wakati wa mkutano uliofanyka katika kambi ya Mbuyuni kijiji cha Qangden.***

Kwa mujibu wa taarifa kutoka mratibu wa taasisi hiyo, kila gari ya kitalii hutozwa kiasi cha Dola za Kimarekani 110, ambapo kiasi dola 20 hupelekwa kwa CBO ya Wahadzabe, dola 20 kwa jamii ya wafugaji ya Wadatoga na dola 20 kwa Wadatoga- (*Black Smith).* Jamii ya wahdzabe inaamini kuwa utaratibu unaotumika katika mgawanyo na matumizi ya rasilimali zinazokusanywa kwa jina lao una mapungufu. Hivyo, baadhi ya waHadzabe wanalalamika kuwa wamegeuzwa kama vivutio hali ambayo inasababisha utu wao kudhalilishwa na uvunjifu wa haki zao za binadamu.

Tume inapenda kuishauri Serikali na washirika wa maendeleo umuhimu wa kushauriana na jamii ya Watu wanaoishi maisha ya Asili (indigenous peoples) na kufikia muafaka katika maamuzi juu ya masuala yanayohusu maisha yao, badala ya kuwaamulia bila ya kuwashirikisha kikamilifu. Ushirikishwaji katika maamuzi yanayowahusu unatokana na Azimio la Umoja wa Mataifa linalohusu watu wenye maisha asilia ambalo Tanzania iliunga mkono mwaka 2007 (*The United Nations Decalaration on Rights of Indegenous Peoples)* Ushirikishwaji wa jamii hiyo na nyinginezo zenye kuishi maisha asili, utaiwezesha serikali kupata namna muafaka ya kuwapa huduma za kijamii.

Tume inashauri mamlaka zinazohusika na ustawi wa jamii na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia halmashauri za wilaya za Mbulu na Karatu kushirikisha jamii ya Kihadzabe katika kuboresha huduma za kijamii. Huduma hizo ni pamoja na;

a) Elimu bora kwa jamii ya waHadzabe kwa kujenga miundo mbinu, kuajiri walimu wa kutosha, ikibidi kutoa mafunzo maalum kwa wanafunzi kutoka katika jamii yao ili wawe walimu katika mazingira yao, na kutoa vifaa vya shule vya kiada na ziada ili watoto wa Kihadzabe wapate elimu katika mazingira yao,
b) Kuboresha huduma ya afya kwa kujenga zahanati, kusambaza madawa na vifaa tiba na kutoa elimu ya afya kwa jamii ya waHadzabe,
c) Uongozi wa wilaya pamoja na taasisi nyingine zitoe kipaumbele kwa makundi yawazee, watoto na wanawake ya jamii ya waHadzabe ili kuboresha haki na maslahi yao.
d) Kukuza na kuhifadhi mila na desturi ya jamii ya waHadzabe ikiwemo kuweka kwenye Makumbusho ya Taifa au Kijiji cha Makumbusho vifaa na tunu zinawazowahusu waHadzabe kwa ajili kumbukumbu ya vizazi vijavyo
e) Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira, sheria ya matumizi na umiliki wa ardhi kwa maslahi ya waHadzabe.

# SURA YA TATU

# 3.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME

## 3.1 Kupokea na kushughulikia malalamiko

### 3.1.1 Utangulizi

Kifungu cha 6 (1)(b) na (c) cha Sheria ya Tume Sura 391 ya kinaipa Tume jukumu la kupokea malalamiko yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kuyafanyia uchunguzi. Malalamiko yanaweza kuwa katika maeneo yafuatayo:-

a) Uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora
b) Mwenendo wa mtu yeyote au taasisi yoyote katika kutekeleza madaraka au utekelezaji unaokiuka madaraka
c) Matumizi au matendo ya watu wenye madaraka katika utumishi wa serikali kuu, serikali za mitaa (Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Vijiji/Kata n.k), mashirika ya umma, vyombo binafsi na watu binafsi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, kutotenda haki au kuonea.

Malalamiko yanayowasilishwa Tume huchambuliwa ili kubaini yale ambayo yapo ndani na yaliyoko nje ya mamlaka Tume. Malalamiko yaliyo ndani ya mamlaka ya Tume huainishwa kati ya yale yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na yale ya ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kisha kuchunguza. Kwa malalamiko yaliyo nje ya mamlaka ya Tume, walalamikaji wanaelekezwa kwenye mamlaka husika au taratibu za kufuata kuhusu malalamiko yao au Tume inaziandikia taasisi husika.

Malalamiko yaliyo katika mamlaka ya Tume hushughulikiwa kwa kuzingatia Katiba ya nchi, sheria husika za nchi, mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda kama vile Mkataba wa kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, Mkataba wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni na mikataba inayolenga makundi maalum kama vile wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

### 3.1.2 Malalamiko yaliyopokelewa na kuchunguzwa

Mwaka 2015/2016 Tume ilipokea malalamiko **579** yaliyowasilishwa katika ofisi za Tume makao makuu, Ofisi ya Zanzibar, na ofisi za matawi ya Lindi na Mwanza. Jumla ya malalamiko **7,913** yalishughulikiwa kwa mwaka 2015/2016 ambapo malalamiko **579** yalipokelewa kwa kipindi hiki na malalamiko **7,334** yalikuwa ya miaka ya nyuma

#### *3.1.2.1 Malalamiko yaliyoshughulikiwa na kuhitimishwa.*

Hadi kufikia Juni, 30, 2016, Tume ilishughulikia na kuhitimisha malalamiko **1,106.** Kati ya hayo, malalamiko **315 (28.5%)** ya walalamikaji yalipatiwa ufumbuzi. Mashauri **140 (12.7%)** ya walalamikaji yalishindwa kuthibitika kutokana na sababu mbalimbali. Malalamiko **156 (14.1%)** yalielekezwa mamlaka nyingine ikiwa na maana hayakupaswa kuwasilishwa Tume. Malalamiko **254 (22.9)** yaliachwa ikiwa na maana yalifungwa kutokana na walalamikaji kutotoa ushirikiano kwa Tume baada ya kuyawasilisha. Malalamiko **241 (21.8)** yalikuwa nje ya mamlaka ya Tume,

yaani hayakukidhi vigezo vinavyotakiwa ili yachunguzwe Tume .Malalamiko **6,807** yataendelea kufanyiwa uchunguzi katika mwaka wa fedha **2016/2017.**

**Jedwali Na 3.1: Mwelekeo wa jinsi malalamiko yaliyohitimishwa tangu mwaka 2002 hadi Juni 2016.**

| | **Yaliyopokelewa** | **Jumla ya malalamiko kwa mwaka** | **Yaliyofungwa** | **Yanayoendelea na uchunguzi *(pending)*** |
|---|---|---|---|---|
| Kutoka TKU | 2,237 | 2,237 | - | |
| 2001/2002 | 1,074 | 3,311 | - | |
| 2002/2003 | 2,458 | 5,769 | 1,595 | 4,174 |
| 2003/2004 | 2,691 | 6,865 | 1,564 | 5,301 |
| 2004/2005 | 2,789 | 8,090 | 2,447 | 5,643 |
| 2005/2006 | 3,812 | 9,455 | 3,021 | 6,434 |
| 2006/2007 | 4,948 | 11,382 | 3,538 | 7,844 |
| 2007/2008 | 2,660 | 10,504 | 2,424 | 8,080 |
| 2008/2009 | 2,459 | 10,539 | 2,731 | 7,808 |
| 2009/2010 | 1,454 | 9,262 | 1,588 | 7,674 |
| 2010/2011 | 1,355 | 9,029 | 1,058 | 7,971 |
| 2011/2012 | 965 | 8,936 | 1,672 | 7,264 |
| 2012/2013 | 1,545 | 8,809 | 1,250 | 7,559 |
| 2013/2014 | 1,080 | 8,639 | 1,202 | 7,437 |
| 2014/2015 | 914 | 8,351 | 1,017 | 7,334 |
| 2015/2016 | 579 | 7,913 | 1,106 | 6,807 |

**Chanzo; THBUB 2015/2016**

## 3.2 Ufuatiliaji wa Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora.

### 3.2.1 Migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi

Tume ilifanya ufuatiliaji wa kutathmini migogoro ya ardhi na athari zake kwa haki za binadamu na utawala bora katika wilaya kumi na nane za Tanzania Bara. Uchunguzi huu uliwashirikisha wananchi katika kubaini aina za migogoro ya ardhi, vyanzo, athari zake na hatua zilizochukuliwa na kutoa mapendekezo ya kutatua migogoro hiyo.

Ufuatiliaji ulifanyika katika wilaya za Geita, Bukombe, Nyang'wale, Misenyi, Bukoba, Karagwe, Muleba, Karatu, Ilemela, Misungwi, Magu, Kilosa, Manispaa ya Shinyanga, Kahama, Kishapu, Shinyanga Ushetu, Msalala na Wilaya ya Shinyanga. Wilaya hizo zilichaguliwa kutokana na kuwepo kwa maeneo yenye migogoro ya mara kwa mara ya umiliki na matumizi ya ardhi. Tume ili baini kuwa migogoro ya matumizi na umiliki ardhi kati ya makundi mbalimbali

kama vile wakulima na wafugaji, wananchi dhidi ya serikali na taasisi zake na wananchi dhidi ya wawekezaji.

Aidha, migogoro ya ardhi imesababisha uvunjwaji wa haki za binadamu na hali ya kutokuwepo kwa utengamano na uvumilivu miongoni mwa jamii katika maeneo yaliyotembelewa. Athari za migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi ni pamoja na uharibifu wa mazingira, kushuka kwa kiwango cha uzalishaji na kipato, kuathirika kisaikolojia, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kupungua maendeleo katika ngazi ya familia, vifo na majeraha yanatopelekea ulemavu, uharibifu wa mali na makazi ya watu na kudorora kwa huduma za jamii.

Aidha, ilibainika kuwa migogoro ya ardhi imesababishwa na uvunjwaji wa sheria na taratibu za umiliki na matumizi ya ardhi. Katika baadhi ya maeneo wananchi wamevamia na kutumia ardhi ambayo hawana umiliki wa kisheria kwa mfano hifadhi za taifa, mapori tengefu, mashamba makubwa ya mikataba, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya huduma za jamii na vyanzo vya maji ili kupata maeneo ya kilimo, malisho ya mifugo na makazi.

#### *3.2.1.1 Mapungufu katika kusajili ardhi na uwekaji wa mipaka*

Mapungufu katika mamlaka zinazosimamia ardhi lilionekana kuwa ni chanzo cha migogoro ya ardhi. Vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sera za serikali kama zile zinazohusu uanzishaji wa makazi na ugawaji upya wa ardhi ambayo awali ilikuwa ikimilikiwa na wananchi vilionekana kutoshirikisha wananchi ipasavyo. Kwa mjibu wa Sheria Namba 4 ya Ardhi ya Vijiji mamlaka sahihi ya kuweka mipaka ya vijiji ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopo kwenye wilaya husika. Baadaye, taarifa inatakiwa kupelekwa katika wizara inayohusika na masuala ya ardhi kwa ajili ya kutoa vyeti vya umiliki. Mfano mmoja ni wa mgogoro kati ya ranchi ya Misenyi (NARCO) iliyoko wilya ya Misenyi mkoa wa Kagera na kijiji cha Bubale inasababishwa na kila mmoja kati yao kuwa na hati ya kumiliki eneo hilo. Katika eneo moja wakati ina hati ya kumiliki 18079 ya miaka 99, iliyotolewa mwaka 1970, kijiji cha Bubale kina hati ya usajili yenye namba ZM/BK/ 131 iliyotolewa tarehe 30 /12/1975.

#### *3.2.1.2 Utwaaji wa ardhi na ulipaji wa fidia*

Ilibainika kwamba mahitaji ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji yamekuwa mojawapo ya sababu kuu za utwaaji wa ardhi. Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Ardhi vinamaanisha kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki ardhi na haki ya hifadhi ya ardhi anayomiliki kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, Ibara ya 24 (2) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kutaifisha au madhumuni mengine kinyume na sheria na bila kulipwa fidia.

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Sura ya 118 ya Sheria za Tanzania (2002) kimempa Rais wa Jamhuri madaraka ya kutwaa au kuhaulisha ardhi kwa manufaa ya umma. Kifungu cha 11 cha Sheria hii kinaeleza kuwa kila mtu ambaye ardhi yake imetwaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 anatakiwa kulipwa fidia. Aidha kifungu cha 13(2) na (3) cha Kanuni za Ardhi (Tathmini ya Thamani ya Ardhi kwa Ajili ya Fidia) 2001 vinahitaji malipo ya fidia kufanyika ndani ya miezi sita tangu ardhi itangazwe kutwaliwa na kwamba iwapo fidia hiyo haitalipwa ndani ya muda huo, itabidi malipo hayo yafanyike pamoja na riba.

Kutolipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili uwekezaji, ujenzi wa miradi ya maendeleo na huduma za jamii ni baadhi ya mifano ya miradi iliyotekelezwa na serikali bila kulipa fidia kulingana na sheria katika baadhi ya maeneo. Malalamiko ya kutolipwa fidia kwa wakati baada ya ardhi kutwaliwa yalijitokeza katika kati ya wilaya Nyang'wale na Mgodi wa Bulyankulu, Kijiji cha Muhunze Wilaya ya Kishapu (ujenzi wa ofisi ya halmashauri), ujenzi wa viwanda vya kuchakata bidhaa kwa mauzo ya nje (Export Preocessing Zome Authority –EPZA) katika kata ya Usagara wilaya ya Misungwi. Wnanchi wa vijiji vya Lunguya na Segese katika wilaya ya Msalala , Nyasubi wilaya ya Kahama kwa kutolipwa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari za kata.

Kwa mfano, katika wilaya ya Bukombe pekee hadi kufikia mwaka 2015 wananchi walikuwa wanadai kiasi cha shilingi **377,571,911.00** toka taasisi za serikali, mashirika ya dini na halmashauri ya Bukombe zikiwa ni sehemu ya fidia ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya maendeleo mbali mbali katika mji huo ifuatavyo;

**Jedwali 3.2; Madeni ya fidia ya ardhi wanazodai wananchi katika wilaya Bukombe**

| Na. | Taasisi inayodaiwa | kinachodaiwa |
|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Bukombe | 219,989,051.00 |
| 2 | Kanisa la Roma | 86,135,960.00 |
| 3 | Jeshi la Magereza | 55,057,600.00 |
| 4 | Mahakama | 16,389,300.00 |
| | **Jumla** | **377,571,911.00** |

**Chanzo; THBUB /Bukombe, 2015**

### *3.2.1.3 Kuhamishwa katika maeneo bila kufuata taratibu za kisheria*

Ibara ya 24 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaeleza kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake ikiwemo ardhi aliyonayo kwa mujibu wa sheria. Katika ufuatiliaji wa Tume, ilionekana kuwa yapo malalamiko ya wananchi kuhamishwa bila kuzingatia sheria na kuwepo kwa rushwa kunakofanywa na baadhi ya mamlaka za serikali kuu na serikali za mitaa.

Kifungu cha 17 cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi sura ya 118, kinatambua watu waliopo kwenye ardhi inayotakiwa kutwaliwa kwamba ni wamiliki halali iwapo itathibitika kuwa walikuwa wanamiliki ardhi hiyo kwa kuilipia kodi Serikalini. Sheria hii na Sheria ya Ardhi inatambua kuwa wamiliki halali tu wa ardhi ndiyo wanastahili kulipwa fidia. Hata hivyo kwa mujibu wa maamuzi mbalimbali ya Mahakama[66],mvamizi wa ardhi hastahili kulipwa fidia yeyote na kwamba mtu atahesabika kuwa ni mmiliki halali wa ardhi iwapo itathibitika kuwa amemiliki ardhi husika kwa muda wa miaka 12 na zaidi bila ya kubugudhiwa. Lalamiko la watu wa kabila la Wamasai kuondolewa toka katika maeneo yao ya asili kwa yaliyokuwa yanumika kulishia mifugo yao limeanzia tangu mwaka 1959, walipoondolewa katika maeneo hayo kupisha kuanzishwa kwa hifadhi ya Serengeti. Miaka ya 1970 hadi 1980 waliondolewa katika sehemu

[66] Kesi ya Rupiana Tungu na Wenzake dhidi ya Abdul Buddy na Haliki Abdul, Rufaa ya Madai Nambari 115/2004 Mahakama Kuu (T) Dar es salaam, iliyoamuliwa na Jaji Mlayi, ukurasa wa 18-20: Pia Kifungu cha 72 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334 (Land Registration Act, Cap 334, R.E 2002), inatambua usajili wa ardhi iliyomilikiwa kwa muda mrefu (adverse possession)

walizohamia kupisha kuanzishwa na kupanuliwa kwa hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara. Mwaka 2006 na 2009 waliondolewa katika maeneo ya Loliondo kwa kutumia nguvu kupisha uwekezaji katika biashara ya uwindaji.[67] Aidha, kuanzia Mwaka 2013 Serikali ilipanga kuondoa wafugaji wa kimasai 25,000 kupisha upanuzi wa hifadhi za Taifa.

Matukio ya wananchi kuondolewa kwa nguvu toka katika ardhi yao yalibainika pia katika maeneo ya Wilaya ya Misenyi ambapo baadhi ya wananchi walilalamika kwamba waliondolewa kwa nguvu na jeshi la polisi kutoka katika ranchi ya Rubale kwa maagizo ya Mkuu wa Wilaya hiyo. Ilielezwa kwamba zoezi hili liliambatana na ubakaji na uharibifu wa mali yakiwemo mashamba na kuchomwa kwa nyumba 47. Matukio kama hayo yaliripotiwa pia katika Wilaya ya Muleba ambapo wananchi wa vijiji vya Rutoro, Kyobuheke, Byangeregere, Bishambya na Kyalutare walihamishwa kwa nguvu kupisha wawekezaji katika sehemu ya ardhi ya Ranchi ya Kagoma.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ya Sheria za Tanzania toleo la 2002, ardhi ni mali. Hivyo Ibara ya 24(1) ya Katiba ikisomwa pamoja na Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Ardhi vinamaanisha kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki ardhi na haki ya hifadhi ya ardhi anayomiliki kwa mujibu wa sheria. Aidha, Ibara ya 24 (2) inakataza mtu yeyote kunyang’anywa mali yake kwa madhumuni ya kutaifisha au madhumuni mengine kinyume na sheria na bila kulipwa fidia.

#### *3.2.1.4 Kutokuwepo kwa mpango wa matumizi ya ardhi*

Kutokuwepo na mpango maalum wa matumizi ya ardhi sambamba na urasimishaji wa ardhi ya kimila katika wilaya nyingi kumesababisha migogoro mingi katika vijiji. Kwa mara kadhaa jitihada za wananchi zinazobuniwa kabla ya mipango ya serikali huenda kinyume na mipango miji ya baadaye ya matumizi. Tume ilibaini kuwa katika baadhi ya maeneo ambayo kulikuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ilisaidia kuepusha migogoro ya wakulima na wafugaji. Matumizi bora ya ardhi katika kilimo na ufugaji kuliepusha migogoro katika wilaya ya Nyang’wale (mkoa wa Geita) ambapo pamoja na kuwepo kwa mifugo na ukulima kama vyanzo vikuu vya mapato, kulikuwa hakuna migogoro kati yao

Umuhimu wa mpango bora wa matumizi ya ardhi ulionekana kuwa changamoto kwa jamii ya Wahadzabe, na suala hilo lilikuwa linashughulikiwa na uongozi wa wilaya ya Karatu kwa kushirikiana na Asasi ya Kiraia (NGO) inayoitwa Ujamaa Community Resource Centre (UCRT). Kwa Mujibu wa Afisa Mradi wa UCRT, eneo la Mang’ola Chini limeshapimwa na kufanyiwa Mpango Wa Matumizi Bora ya Ardhi katika hatua za awali.

#### *3.2.1.5 Kuongezeka kwa mifugo na kilimo na uhaba wa ardhi*

Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Tanzania inakadiriwa kuwa na ngombe milioni 22.8 , mbuzi milioni , 15.6, kondoo milioni 7.0 na nguruwe milioni 2.01 . Takwimu zinaonyesha kuwa kwa 2013, sekta ya mifugo ilikuwa kwa asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 3.1 kwa mwaka 2012.[68] Kupanuka kwa sekta ya mifugo kunatokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo wakati ukubwa wa ardhi ya malisho inabakia ile ile.

[67] Taarifa ya Uchunguzi wa Tume Loliondo ya mwaka 2009

[68] Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Bungeni la Bajeti , 2014/2015

Kuongezeka kwa idadi ya mifugo ambayo haiendani ardhi ya malisho na miundombinu iliyopo, kunachangia katika migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi. Mabadiliko ya tabia ya nchi na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika maeneo ambayo yalitumika kama malisho yameongeza msukumo katika matumizi ya ardhi na migogoro. Kuondolewa kwa Wafugaji wa Kimasai huko kumewafanya wafugaji wa Kimasai kupoteza zaidi ya asilimia 50% ya eneo la malisho ya mifugo yao huku wakiondolewa kila maeneo mengine walikohamishia mifugo yao (Meatu (2011) na Rufiji 2011/2012).[69]

Kwa jamii nyingi za wafugaji kupoteza ardhi ambayo ilikuwa muhimu kwa maisha yao, kumewalazimisha kuhamia katika sehemu nyingine za nchi kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Watu haohao wanaoondolewa kutoka katika mazingira au maeneo fulani bila ya kuonyeshwa kwa kwenda wanalaumiwa kwa kusababisha migogoro katika sehemu wanazohamia. Zoezi la kuwaondoa wafugaji bila kuwatafutia eneo mbadala au kulipa fidia limewanyima haki za msingi wafugaji wa kimasai.

Migogoro inayosababishwa kugombania maeneo ya malisho ilitaarifiwa katika wilaya za Misenyi, Misungwi, Magu, Karatu, Karagwe, Muleba, Bukoba, Bukombe na Kilosa. Katika wilaya ya Misenyi ilitaarifiwa kuwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inamiliki hekta 23,000 kwa ajili ya kulisha ngombe 2000 tu, wawekezaji wengine walikuwa na hekta 23,000 kwa ajili ya ngombe 7,800 na kiwanda cha Sukari cha Kagera kilikuwa kinamiliki hekta 14,000. Wananchi wanamiliki eneo lililobaki la hekari 18,000 kwa ajili makazi, eneo la kilimo, na malisho ya ngombe zaidi ya 20,000 walionao. Hali hii imesababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji kugombania malisho kwa ajili ya mifugo yao.Ushindani kwa ajili ya ardhi ya malisho kati ya wawekezaji, wafugaji na wakulima

### *3.2.1.6 Haki za watu wanaoishi maisha ya asilia na makazi ya kudumu*

Suala la haki ya kumiliki ardhi, haki ya kuishi na kupata mahitaji muhimu kwa watu wanaoishi maisha ya asili lilijitokeza katika ufuatiliaji huu. Mgogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi kati ya jamii ya Wahadzabe na jamii zingine kama vile wakulima wa vitunguu na wafugaji waliohamia na kuvamia maeneo yao ya asili pamoja na mpaka kati ya jamii ya Wahadzabe wanoishi kijiji cha Endamaghan na NCAA liliripotiwa wakati uchunguzi.

Jamii ya Wahadzabe wilaya ya Karatu hawana ardhi wanayomiliki kisheria kwa ajili ya makazi ya kudumu na shughuli za kujikimu kama uwindaji, uokotaji wa matunda na uvunaji wa asali tofauti na Wahadzabe wenzao wanaoishi kijiji cha Mongo wa Mono, Yaeda Chini, wilaya ya Mbulu ambao wanamiliki ardhi kisheria na pia imefanyiwa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Jamii hii ililalamika kuwa maeneo yao ambayo walikuwa wakiishi tokea zamani yamevamiwa na jamii za wafugaji na wakulima ambao wamekuwa wakikata miti kwa ajili ya ujenzi na uchomaji wa mkaa. Uvamizi wa wafugaji na wakulima umesababisha wahadzabe kusukumwa nje ya maeneo yao na kuishi sehemu za milimani. Ilibainika kuwa kuna eneo la mraba la ekari 100 ililotengwa kwa ajili ya jamii hii lakini bado kulikuwa na changamoto la eneo hili kuvamiwa

[69] CHRAGG /IFAD; Report of the Side Event on the Exixtance and Rights of Indegenous Peioples in Tanzania ; 17 th December 2014.

na jamii za wafugaji kwa ajili ya malisho na makazi. Hivyo pamoja na nia njema ya serikali kuwasaidia Wahadzabe lakini bado jamii haijanufaika na mpango huo wa serikali

Kwa maelezo yao Wahadzabe wanakosa haki yao ya msingi ya kutumia na kumiliki ardhi kwa mujibu wa Katiba na sheria kutokana na kutoshirikishwa na kuwa na uwakilishi katika ngazi za maamuzi kama vile ujumbe katika Halmashauri ya Kijiji na Mabaraza ya Ardhi ya kijiji. Hali hiyo pia imesababishwa na mila na desturi na mfumo wao wa maisha ya uwindaji na kuhama hama kutoka sehemu mmoja kwenda nyingine umechangia maeneo yao kuonekana wazi na kushawishi jamii zingine kuyavamia.

Pamoja na kwamba tatizo la ardhi kuonekana kuwa changamoto kwa jamii ya Wahadzabe, lakini Tume ilijiridhisha kuwa suala hilo linashughulikiwa na uongozi wa wilaya ya Karatu kwa kushirikiana na Asasi ya Kiraia (NGO) inayoitwa Ujamaa Community Resource Centre (UCRT). Kwa Mujibu wa Afisa Mradi wa UCRT, eneo la Mang'ola Chini limeshapimwa na kufanyiwa Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi katika hatua za awali. Aidha, Wahadzabe wanalalamikia mgogoro wa mpaka kati ya jamii ya Wahadzabe wanaoishi katika kijiji cha Endamaghan na NCAA. Iliarifiwa kuwa mwaka 2002, Hifadhi ya Ngorongoro iliongeza mpaka wa hifadhi *"Fire Break"* ndani ya eneo la kijiji bila kuwashirikisha wananchi na hali hii imepelekea upungufu maeneo ya makazi, uwindaji na uhaba wa chakula kwa jamii ya wahadzabe.

#### *3.2.1.7 Rushwa na matumizi mabaya ya madaraka katika usimamizi na ugawaji wa ardhi*

Kutokana na rushwa na kutozingatia kwa maadili katika mamlaka zenye kusimamia ardhini chanzo kingine cha mogogoro ya ardhi. Tuhuma za rushwa, kukosekana kwa uwazi, ushirikishwaji mdogo wa jamii, kutoza faini zisizo halali, kutolipa fidia inavyostahili na ugawaji wa viwanja usiokuwa wa haki. Kuwepo wa wahamiaji haramu kutoka nchi jirani ulihusishwa na tabia ya baadhi ya maafisa wa serikali wasiokuwa na maadili wakiwemo maafisa wa uhamiaji na viongozi wa vijiji. Wananchi walitoa tuhuma za uuzwaji wa ardhi kiholela kwa wageni katika vijiji vya Kakukyu (Misenyi), Kihanga na Katanda (Karagwe) wa vijiji vya Kuwepo kwa wahamiaji haramu na makundi makubwa ya mifugo wanatuhumiwa kutoa hongo kwa baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa ili wawaruhusu kuvuka mipaka wakiwa na mifugo yao kinyume cha sheria.

Tuhuma za uuzaji na wa ardhi bila kufuata utaratibu ilitolewa pia katika kijiji cha Qangden wilaya ya Karatu ambako wananchi wanatuhumu uongozi wa kijiji kwa kuuza/kukodisha shamba la ekari 130 bila kufuata utaratibu. Hata hivyo suala hii lilikuwa linaendelea kushughulikiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wilaya ya Karatu pamoja na Baraza la Nyumba na Ardhi la Wilaya.

Ilidaiwa kwamba kuna kukosekana kwa uwazi hususan katika kutwaa ardhi kwa matumizi ya umma. Ukosefu wa ushiriki wa wananchi katika kufanya maamuzi ya ugawaji wa ardhi ni tatizo kubwa hasa katika mchakato wa kubadilisha matumizi ya ardhi au utwaaji wa ardhi. Suala hili la ushirikishaji wananchi halitiliwi maanani kama inavyotakiwa. Kwa mfano katika kijiji cha Mhunze wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, iliripotiwa kwamba mgogoro uliibuka kufuatia uamuzi wa mamlaka husika za serikali za mitaa kupandisha hadhi ardhi kuwa ardhi ya mji bila kuwashirikisha wananchi kwa ujumla. Huu unafanana na uamuzi wa kukipandisha hadhi kitongoji cha Mabwegere kuwa kijiji ambao mchakato wake haukushirikisha kikamilifu vijiji

jirani .Tukio hili limesababisha msururu wa migogoro ya mipaka katika eneo hili na uhalali wa hadhi ya kijiji kinachotumiwa na wafugaji.

### *3.2.1.8 Uelewa wa sheria zinazosimamia ardhi na madini*

Kukosekana kwa uelewa wa sheria za ardhi katika jamii na haki za wananchi lilionekana kuwa ni tatizo linalosababisha migogoro ya ardhi kati ya wachimbaji wadogo, mamlaka husika na wamiliki wa leseni.Wananchi hawajui ni kwanini hawaruhusiwi kuendelea na shughuli zao za uchimbaji wa mdogomdogo katika ardhi yao waliyoirithi kutoka kwa mababu zao. Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na.5 na Sheria ya Mahakama (Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi) ya mwaka 2002, pamoja na sheria za madini na uwekezaji zimekuwa zikifanya kazi kwa zaidi ya muongo mmoja sasa tangu zilipotungwa, bado shera hizi hazijulikani kwa watumiaji wa ardhi wengi.

Ilibainika pia kuwa baadhi ya wananchi hawaelewi taratibu za sheria za kudai haki zao na huduma za kisheria hazipatikani kwa watu wa kawaida maskini katika maeneo ya vijijini. Hata katika maeneo ambapo huduma hizi zinapatikana wananchi haelewi majukkumu ya Mabaraza ya Vijiji na Kata na Mabaraza ya Ardhi za Nyumba ya Wilaya. Taratibu na matakwa ya kisheria katika kufungua na uendeshaji wa kesi za migogoro ya ardhi pia haieleweki kwa wananchi walio wengi.

Kutokana na rushwa na kutozingatia maadili viongozi kumesababisha kuwepo kwa wahamiaji haramu katika maeneo ya mipaka toka nchi za jirani. Hali hii ilielezwa kuwa ndio sababu ya migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima katika mikoa ya mipakani, ambako kuna idadi kubwa ya wahamiaji haramu kutoka nchi jirani na makundi makubwa ya mifugo kwa ajili ya kutafuta malisho. Matukio ya kuingia kwa makundi makubwa ya mifugo yameripotiwa katika wilaya za Misenyi (Bubale, Kakunyu na Bugango), Bukombe, na Karagwe. Katika hali isiyokuwa ya kawaida baadhi ya sehemu za ardhi zimeuzwa kinyume cha sheria kwa wahamiaji haramu katika vijiji vya Kihanga na Katanda katika wilaya ya Karagwe

### *3.2.1.9 Mapungufu katika Mabaraza ya Ardhi*

Mabaraza ya Ardhi yameanzishwa kama chombo cha kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi mbalimbali. Mabaraza haya ni baraza laa Ardhi la Kijiji, Baraza la Kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.[70] Hata hivyo, uchunguzi ulibaini kwamba katika baadhi ya kata hakuna mabaraza ya ardhi jambo linalosababisha wananchi kusafiri umbali mrefu ili wapate huduma hii au kuamua kutumia nguvu.

Katika maeneo mengine mabaraza yalikuwa yameundwa lakini yalikuwa hayafanyi kazi kwa sababu ya kukosekana raslimali fedha na watu. Baadhi ya Mabaraza hayana zana za kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na ofisi. Vilevile, wajumbe wa mabaraza hawalipwi mishahara badala yake hupata posho ambazo ni ndogo kukidhi mahitaji yao muhimu na hazilipwi kwa wakati.

[70] Kifungu cha 3, Sheria namba 2 ya 2002

Eneo jingine muhimu lililobainika ni tuhuma za rushwa miongoni mwa wajumbe wa mabaraza. Wananchi wanaamini kwamba viwango vya rushwa katika mabaraza viko juu na wengi wao wamepoteza matumaini ya kupata haki pasipo kutoa rushwa. Maoni ya wananchi ni kwamba kama mtu akitaka kukata rufaa kutokea Baraza la Kata kwenda kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya huchukua zaidi ya miezi sita ili kesi yake iweze kusikilizwa. Hali hii inasababababisha wananchi wasiyaamini mabaraza haya na ufanisi wake katika utendaji kazi.

***3.2.1.10 Changamoto za maeneo yenye uwekezaji katika madini***

Tume ilibaini kuwa migogoro ya ardhi inayotokana na uwekezaji kwenye madini ni mingi na yenye gharama kubwa kwa maendeleo ya wananchi. Wilaya za mikoa ya Geita, Shinyanga, Kagera na Mwanza zenye uwekezaji mkubwa na mdogo wa uchimbaji wa madini ya dhahabu zilitaarifiwa kuwa na migogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wananchi, wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa, wananchi na serikali. Katika Mkoa wa Geita wananchi wanalalamikia kuondolewa kwenye maeneo yao kwa fidia ndogo kupisha uwekezaji mkubwa wa uchimbaji wa dhahabu uliofanywa na Mgodi wa Geita Gold Mine(GGM) Wananchi wa mitaa ya Katoma na Nyakabahale yanayopakana na mgodi huo.

Wananchi hao pia wanalalamikia uharibifu wa unaofanywa na shughuli za uchimbaji kuwa zinaharibu mazingira na makazi yao. Kwa Kijiji cha Katoma na vijiji vya jirani mtetemo unaotokana na ulipuaji wa miamba umebomoa au kusababisha nyufa katika nyumba zao.



***Kilichokuwa chanzo cha maji katika mtaa wa Katoma kabla ya kufunikwa na tope linatoka katika mgodi wa dhahabu Geita***

Aidha, ujio wa GGM mwaka 2000 ulikiweka kijiji cha Nyakabhale chenye hati ya tangu mwaka 1989 ndani ya leseni ya uchimbaji wa GGM na kupiga marufuku shughuli zozote za uchimbaji mdogo. Ilielezwa kuwa mwaka 2004 GGM ililipa fidia kwa baadhi ya wananchi na baadhi hawakulipwa. Ilielezwa kwamba eneo la Mtagata ambalo wachimbaji wadogo walikuwa wanafanya uchimbaji mdogo mdogo na kujipatia chakula nalo lisimamishwe na kupewa eneo la Nyamhanga ambako wameshindwa kupata madini. Wakati huo, eneo la kilimo ni dogo hivyo ilibidi wavamie sehemu katika hifadhi katika eneo la Manga ambalo wakati wa kuondolewa nyumba na mazao yao yalichomwa moto.

Wananchi pia, wanalalamikia uchafuzi wa mazingira kutokana na milipuko ya baruti na matumizi ya sumu wanaoitaja kuwa ni aina ya ***"Cynide***." Wananchi hasa wanaoishi karibu na

bwawa la kuchujia sumu la mgodi huo walieleza kuwa wanajua kuwa kemikali zinazotokana na maji mgodini hapo ni sumu kali na pamoja na kuwa hawajui ni kwa kiasi gani wanaamini sumu hizo zina madhara makubwa kwao. Walieleza kuwa, kwa njia moja maji yenye sumu huzama chini na kunywa na mimea ambayo huliwa nao na wanyama wao. Pia, kuwa wakati wa jua kali vumbi laini toka kwenye bwawa hilo hupeperuka kufika kijijini Wananchi hao walilalamika kuwa ambayo ni hatari kwa maisha ya wanadamu hivyo kupigwa marufuku matumizi yake katika maeneo mengi duniani.

#### *3.2.1.11 Mapendekezo*

Katika taarifa, ya uchunguzi Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo kwa halmashauri, Idara za ardhi na madini. Kwa Wizara zinazushughulikia ardhi, kilimo, mifugo, mazingira, madini kushirikiana na wadau asasi za kiraia kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusu sheria mbalimbali za ardhi ili waweze kushughulikia migogoro ya ardhi ipasavyo.

(a) Kushirikisha wananchi na wadau wengine katika michakato wa kupanga au kutoa maamuzi juu ya umiliki na matumizi ya ardhi.

(b) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara zinazosimamia mifugo, Kilimo , mali Asili na Mdini kushirikiana halmashauri katika kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa mpango bora wa matumizi ya ardhi.

(c) Kuhamasisha wananchi na wadau wote wa haki kupambana na rushwa na matumizi mabaya ya madaraka ili kupunguza migogoro ya ardhi katika jamii. Rushwa katika usimamizi wa ardhi inahusishwa na kutokuwepo uwazi, usawa, uadilifu na programu endelevu.

(d) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Idara na serikali za mitaa (Halmashauri na manispaa) ziongeze3 rasilimali katika usimamizi wa ardhi kwa kuwa ilibainika kwamba idara nyingi zinazoshughulika na masuala ya ardhi zina uwezo mdogo wa kusimamaia eneo hilo kutokana na kukosa bajeti na vitendea kazi.

(e) Kujenga dhana ya kushughulikia migogoro inapotokea kwa kufanya kuchunguza malalamiko ya wananchi mapema. Ilibainika kwamba kutotatuliwa kwa malalamiko yanayowasilishwa katika mamlaka husika kwa wakati ni tatizo linalosababisha wananchi kutozingatia sheria.

(f) Tume inasistiza kuzingatiwa Katiba, na sheria za ardhi panapotokea hitaji la kutumia ardhi inayomilikiwa na wananchi kwa shughuli za maendeleo ikiwemo kufuata taratibu za kuondoa wananchi kwenye makazi ua maeneo yao na kuwalipa fidia.

### 3.2.2 Uchunguzi wa lalamiko la bomoamoa uliofanyika Dar es Salaam

Tume ilifuatilia ubomoaji wa nyumba zilizojengwa kando ya Bonde la Mto Msimbazi katika kata za Hananasifu, Magomeni, Mzimuni, Kigogo, Mchikichini, Jangwani, Kariakoo, Upanga magharibi na Ilala katika Manispaa za Ilala na Kinondoni. Wananchi wa kata hizo walilalamikia Baraza la Taifa la Mazingira, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Manispaa za Ilala na Kinondoni kwa ubomoaji wa nyumba katika maeneo yaliyotajwa na baadhi ya nyumba kuwekewa alama ya ‘‘X’’ kwa madai kuwa ziko katika bonde la mto Msimbazi eneo

ambalo ni hatarishi kwa maisha ya binadamu.Wananchi hao walilalamikia zoezi la ubomoaji kufanyika pasipo kuzingatia misingi na taratibu na haki za binadamu kama ifuatavyo:

1) Kutokuwepo taarifa yoyote kwa wenyeviti wa Serikali za Mitaa au tangazo kuhusu ubomoaji katika maeneo yao.
2) Uharibifu na upotevu wa mali kama vile fedha na samani za ndani, mavazi, vyakula na nyaraka mbalimbali na vifaa ya watoto wa shule.
3) Baadhi ya wakazi kuathirika kiafya na kisaikolojia baada ya kushuhudia zoezi la ubomoaji wa makazi yao.
4) Kusimama kwa shughuli zao za kiuchumi, kubomolewa nyumba zao ambazo baadhi zilikuwa zimetambulika, ikiwa ni pamoja na kulipa kodi za majengo, leseni za makazi, leseni za biashara, huduma za umma kama vile maji na umeme na kuwepo uongozi wa serikali za Mitaa.

Tume ilifanya uchunguzi wake kwa kutembelea Uongozi wa Manispaa, kata za Manispaa ya Kinondoni na Ilala na kuonana na wenyeviti wa mitaa, wataalamu wa ardhi wa manispaa na wananchi wa maeneo yaliyoathirika. Aidha, Tume ilifanya mahojiano na viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kupata ufafanuzi wa utekelezaji wa zoezi hilo na kupitia nyaraka mbali mbali zinazohusu suala hilo.

Bonde la mto Msimbazi lenye urefu wa kilomita 36 ni sehemu ya bonde la mito minne mikubwa katika jiji la Dar es Salaam. Mito mingine ni Mpiji (kilomita 12.7), Kizinga (kilomita 17.5) na Mzinga (kilomita 10.4). Bonde la Mto Msimbazi linachukua sehemu kubwa ya ikolojia hizo na uhifadhi wa maeneo oevu na mazingira ya Dar es Salaam. Kwa kuzingatia ikolojia hiyo, bonde la Mto Msimbazi lilipendekezwa libaki wazi katika mipango ya Jiji la Dar es Salaam ya mwaka 1949, 1968 na 1979 kama eneo oevu na hatarishi kwa maisha ya binadamu *(‘Hazardous land’*).
Ilibaini kuwa, pamoja na katazo la kisheria la kutoendeleza eneo Bonde hilo lina huduma zinazotolewa na taasisi za umma kama vile umeme, maji pamoja na makusanyo ya kodi katika maeneo yaliyokataliwa kisheria kulionekana kwa wananchi kama kiashiria cha uhalali wa kuendelea kuwepo kwao katika eneo hilo.

Aidha ilibainika kuwa pamoja na kuwepo kwa sheria hizi eneo hilo lina maendelezo ya shughuli za makazi na shughuli za uzalishaji kama vile kilimo, gereji, maduka, nyumba za kulala wageni na hoteli. Inakadiriwa kwamba zaidi ya nyumba 8,000 zimejengwa ndani ya bonde hilo huku baadhi zikiwa na hati miliki. Athari za maendelezo katika bonde la Msimbazi ni pamoja na uchafuzi wa mazingira unaofikia hadi kwenye bahari na kuathiri ikolojia ya bahari, upotevu wa mali na maisha ya binadamu.

Taarifa zinaonesha katika kata za Hananasif na Magomeni nyumba 744 zilibomolewa katika zoezi lililofanyika tarehe 12 – 17 Desemba, 2015. Aidha ilibainika baadhi ya wananchi waliokuwa na makazi katika Bonde hilo walikuwa wakilipa kodi ya majengo.

Kuhusu wananchi kupewa taarifa juu ya zoezi la ubomoaji, ilibainika kuwa “Taarifa kwa Umma” iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwezi Novemba, 2015 ililenga kuelezea zoezi la uvunjaji wa nyumba (maendelezo) zilizojengwa katika maeneo ya wazi, nyumba zilizojengwa bila kufuata utaratibu na nyumba

zilizojengwa bila kufuata ramani. Mwongozo huo ulilenga kubomoa nyumba zilizo ndani ya mita "60" au zenye alama "X", na kutovunja nyumba zenye hati na leseni za makazi na kutoa muda wa kuondoa vifaa kwa wakazi. Hata hivyo, kilichojitokeza ni kwamba zoezi la ubomoaji liliendeshwa bila kuzingatia mwongozo kwani baadhi ya nyumba zilizovunjwa zilikuwa nje ya mita 60. Tume ilijiridhisha kuwa mwongozo huo haukuzingatia sheria, na misingi ya haki za binadamu inayotakiwa kufuatwa kabla ya kuwaondoa wakazi wanaoishi maeneo yasiyo rasmi.
Aidha, kutoguswa majengo ya viwanda au biashara kubwa zilizo ndani ya bonde la Msimbazi kama vile ujenzi wa kituo cha mabasi ya mwendo kasi cha Jangwani, na majengo yaliyoko eneo la Al-hamza wakati wa ubomoaji kunaonyesha kuwepo kwa dalili za ubaguzi dhidi ya mali za watu wa kipato cha chini

Kutotoa taarifa za ubomoaji kwa wakazi hao, na kutofuata utaratibu wa kuwaondoa wakazi katika makazi hayo ni uvunjwaji wa haki zao za msingi za binadamu za watu hao. Pamoja na ubomoaji huo, ilielezwa kuwa, serikali haikuwa na mpango wa kuwafidia wananchi waliobomolewa nyumba hizo. Aidha, ilifahamika kuwa wapo wananchi waliokuwa wamepewa viwanja na Kamati ya Kitaifa ya Maafa eneo la la Mabwepande mwaka 2011 kutokana na mvua iliyosababisha maafa, na sio kwa sababu walijenga katika eneo linalotakiwa kubomolewa.

Bomoabomoa ya makazi ya watu hao ilipoteza mali zao bila kutoa msaada wa mahali pengine pa kujihifadhi kilikuwa ni kitendo cha ukatili na uvunjifu wa haki za msingi. Tume ilijiridhisha kuwa nguvu (forced eviction) ilitumika katika kuwaondoa bila kufuata taratibu za kisheria, bila ya makazi mbadala na fidia baada ya makazi kubomolewa.

Aidha, Serikali ikiwa msimamizi wa sheria ni lazima iongoze kwa mfumo wa kufuata taratibu za kisheria katika maamuzi yake na utekelezaji wa maamuzi hayo. Ubomoaji wa nyumba bila kutoa notisi kama sheria inavyotaka ni kitendo cha ukiukaji wa sheria zinazotaka kutoa notisi jambo ambalo lingepunguza athari.Ubomoaji huu ni "forced eviction" kulingana na vigezo vya misingi ya sheria ya kimataifa ya haki ya binadamu. Pia ni kinyume na haki ya umiliki wa mali inaolindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwenye ibara ya 24 inayotoa haki ya kila mtu kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria, ikiambatana na haki ya kulipwa fidia mali hiyo inapotaifishwa au kuchukuliwa kwa manufaa, au mahitaji ya umma au taifa.

Hivyo Tume inapendekeza yafuatayo kuhusu watu waliobomolewa nyumba zao;

i. Serikali ipitie madai ya watu wote waliobomolewa nyumba na kuharibiwa nyumba zao ili kuwafidia kama Katiba inavyotaka.
ii. Wizara ya Ardhi ifanye uhakiki wa kina kuhusu ugawaji wa viwanja vya Mabwepande ili kubaini watu waliopata viwanja huko lakini baadaye wakaonekana ni waathirika wa bomoa bomoa bonde la Msimbazi.
iii. Mamlaka zinazohusika na mazingira zichukue hatua za makusudi na za kitaalam kudhibiti kupanuka kwa bonde la msimbazi
iv. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi izitambue nyumba zenye hati za umiliki na ifanyiwe tathmini na wamiliki walipwe fidia.
v. Wizara inayosimamia mazingira itoe elimu kwa wananchi walioko katika maeneo yasiyo rasmi ili wafahamu maeneo ya ardhi ya hifadhi, ardhi hatarishi na ufafanuzi kuhusu mita 60 na "*Highest Water Mark*".

### 3.2.3 Ufuatiliaji wa Hali za Wazee na Watu Wasiojiweza katika Makazi ya Wazee Nunge, Dar es Salaam

Septemba, 2015 ufuatiliaji wa hali za wazee katika makazi na Nunge jijini Dar es salaam ili kuona hali halisi ya maisha wanayoishi, changamoto zinazowakabili na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili. Hatua hii ni kwa mujibu wa **Sheria ya Tume Na. 7/2001, kifungu cha6 1 (a) (b) na (c)** kinachoitaka Tume kufanya ufuatiliaji wa suala lolote linalohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Makazi ya wazee na watu wasiojiweza Nunge yaliyopo mtaa wa Vijibweni, tarafa ya Kigamboni, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam yalianzishwa mwaka 1936 na Serikali ya kikoloni. Mwaka 1970 makazi hayo yalichukuliwa na serikali ya Tanzania na kwa sasa yapo chini ya usimamizi wa Wizara ya afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, wazee na Watoto (Idara ya ustawi wa jamii)

Makazi ya wazee na watu wasiojiweza Nunge yalianzishwa kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye maradhi ya ukoma na baada ya ugonjwa huo kumalizika, serikali ilibadilisha matumizi ya makazi hayo na kwa sasa yanawahudumia wazee, watu wasiojiweza kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na vijana wanaovuka umri wa kuhifadhiwa katika makao ya watoto Kurasini.

#### *3.2.3.1 Hali ya Kambi na haki za wakazi wake*

Tume ilipotembelea makazi ya wazee na watu wasiojiweza kulikuwa na jumla ya wahudumiwa 122 kwa mchanganuo uliooneshwa kwenye jedwali. Aidha uwezo wa makazi ni kuhudumia watu 90 tu. Idadi hiyo ya wahudumiwa katika makazi ya Nunge ni kubwa kuliko uwezo wake na ina wakazi wengi wa umri mdogo tofauti na malengo ya kuanzishwa kwake.

**Jedwali 3; Jedwali Idadi na umri wa wakazi wa kambi ya Nunge**

| | **Umri** | **Wanaume** | **wanawake** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | 60+ | 16 | 06 | 22 |
| | Kati ya 36- 60 | 05 | 06 | 11 |
| | Kati ya 18-35 | 45 | 27 | 72 |
| | Kati ya 0- 17 | 10 | 07 | 17 |
| | **Jumla Kuu** | **76** | **46** | **122** |

**Chanzo THBUB 2017**

#### *3.2.3.3 Changamoto zinzoathiri utelezaji wa haki za wakazi wa Nunge*

1. Upungufu wa bajeti ni changamoto katika utekelezaji wa haki za wazee kwakuwa unasababisha mahitaji muhimu kama vile chakula, umeme, maji, madawa na usafiri kwa

wahudumiwa kutopatikana au kuchelewa kuwafikia.Ufinyu huo wa bajeti pia unawaathiri wanafunzi/ wahudumiwa wanaosoma kwa kuwacheleweshea fedha kwa ajili ya karo na mahitaji mengine muhimu kama vile madaftari, kalamu, vitabu na nauli za kila siku kwenda na kurudi shuleni. Kutokana na tatizo hili baadhi ya wanafunzi wamelazimika kuacha masomo kwa ajili ya ukosefu wa fedha. Ukosefu wa fedha kwa ajili ya utengamano umesababisha vijana wenye umri wa zaidi ya miaka 18 kuendelea kuwa tegemezi katika makazi kwa kuwa serikali imeshindwa kuwawezesha kujitegemea.

2. Upatikanaji wa huduma za afya ni moja ya changamto zinazoathiri haki za wazee. Huduma za matibabu kwa wahudumiwa wa makazi ya wazee Nunge zinatolewa na Halmashauri ya wilaya ya Temeke ambayo huipatia zahanati ya kituo madawa. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mahitaji halisi ya matibabu ya wazee waliokadiriwa kuwa 130 yalikuwa jumla ya **Tshs. 17,790,700/=** lakini kwa mwaka huo fedha iliyoidhinishwa na Serikali kwa ajili ya matibabu ni jumla ya **Tshs. 2,600,000/=**. Kutokana na mahitaji maalumu ya dawa na vipimo hasa kwa magonjwa yanayowakabili wazee kama vile Kisukari, shinikizo la damu, ARV's na ukosefu wa vipimo hali inayoulazimu uongozi wa makazi kutafuta namna ya kuwapatia wazee matibabu nje ya kituo. Pia wahudumiwa walilalamikia huduma duni za matibabu na kutozwa gharama kubwa za matibabu (madawa na vipimo) kinyume na sera ya wazee ambayo imeelekeza kuwa gharama za matibabu kwa wazee itolewe bure. Aidha waliwalalamikia wahudumu wa afya katika makazi kwa kutowapatia huduma ya usafi katika nyumba wanazoishi na kutowahudumia wazee wanapozidiwa usiku.

3. Makazi yanakabiliwa na ukosefu wa usafiri wa kuaminika kwa ajili ya kuwasaidia wahudumiwa, hasa wazee wanaohitaji huduma mbalimbali nje ya kituo..

4. Makazi yana upungufu wa vitendea kazi kama vile komputa, printa, shajala, vifaa vya usafi, vyombo vya kupikia na vyombo vya kulia chakula.

5. Makazi yanakabiliwa na uchakavu wa miundombinu unahusisha majengo, mfumo wa umeme, mfumo wa maji safi na maji taka. Baadhi ya nyumba ni chakavu, zina nyufa, hazina milango na madirisha. Katika Mwaka wa fedha 2015/2016 mahitaji halisi ya makazi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo na miundombinu ilikuwa ni jumla ya **Tshs.1,535,516,000/=** na Serikali iliyapatia makazi Kiasi cha **Tshs. 300,000,000/=** ambacho hakitoshelezi mahitaji.

6. Baadhi ya huduma kama vile vyoo si rafiki kwa wazee kwani vyoo vingi havina milango kwa ajili ya kujisitiri hasa nyakati za mchana. Pia vimejengwa nje ya nyumba hali inasababisha usumbufu mkubwa kwa wazee hasa nyakati za usiku kwani huwalazimu baadhi yao kujisaidia ndani kwa kutumia ndoo.

7. Aidha Makazi yana jumla ya watumishi 29 wa kada mbalimbali, hata hivyo bado kuna upungufu wa watumishi hasa katika kada ya wahudumu wa afya na walinzi. Mfawidhi katika makazi hayo aliueleza ujumbe wa Tume kuwa makazi yenye jumla ya ekari 20.6 yanalindwa na mlinzi mmoja tangu mwezi Januari, 2015.

8. Kuvamiwa kwa eneo la makazi kunaendelea kuongezeka. Makazi haya yalipoanzishwa yalikuwa na ukubwa wa ekari 50.4 na kwa sasa zimebaki jumla ya ekari zipatazo 20.6 baada ya kuvamiwa na wananchi na kujenga nyumba hali iliyosababisha kuwepo kwa mgogoro wa ardhi kati ya makazi na wananchi wanaolizunguka eneo hilo. Imeelezwa kuwa baadhi ya wananchi wamevamia maeneo hayo kwa madai kuwa yalichukuliwa na serikali bila ya fidia.

9. Aidha, Tume imebaini kuwa baadhi ya wahudumiwa wanaoishi katika makazi hayo siyo walengwa hali inayoongeza mzigo kwa serikali kuwatunza watu ambao hawastahili.

#### *3.2.3.2 Mapendekezo ya Tume katika kuimarisha haki za wazee walio katika kambi ya Nunge*

**Wizara ya Afya, maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kwa kushirikiana na Manispaa ya Temeke**

- Wizara iongeze bajeti kwa ajili ya mahitaji ya wakazi hasa kwa ajili ya huduma ya afya.
- Iongeze wafanyakazi, hasa wahudumu wa afya, walinzi na washauri nasaha.
- Wafanyakazi katika makazi walipwe stahili zao kama njia ya kuwapa motisha wa kazi.
- Wizara iandae sheria ya wazee, kanuni na taratibu za uendeshaji wa makazi ya wazee.
- Wizara iwapatie wazee matibabu bure kama inavyoelekezwa katika sera ya taifa ya Wazee ya mwaka 2003,Aidha utaratibu wa bima ya afya uandaliwe
- Serikali iyawezeshe makazi ili kuwe na shughuli za uzalishaji mali kwa watoto/ndugu wa wahudumiwa waliopo katika makazi.
- Wizara ishughulikia suala la mgogoro wa uvamizi wa ardhi ya makazi (ihakikishe makazi yanapata hati miliki).
- Wizara iweke fensi (Wigo) kwa ajili ya kuzuia uvamizi wa eneo la makazi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo Makazi**

- Wizara ishughulikie mgogoro wa ardhi katika makazi hasa katika kuhakikisha kuwa makazi ya wazee yanapatiwa hati miliki.

**Uongozi wa Makazi ya Nunge**

- Uongozi wa makazi uhakikishe kuwa wazee wanapewa huduma zinazostahili.
- Uongozi wa makazi kwa kushirikiana na wahudumiwa uandae kanuni zitakazotumika katika makazi.
- Uongozi uwe na mahusiano ya wazi na shirikishi kati yake na wahudumiwa ili kupunguza migogoro.
- Kuanzisha program zinazotoa fursa kwa wazee kushiriki katika mipango ya uchumi kwa ajili ya maendeleo yao.

**Jamii/ Wananchi**

- Ielimishwe juu ya umuhimu wa kuheshimu na kulinda haki za wazee nchini.
- Familia na jamii zielimishwe juu ya wajibu wao wa kuwatunza wazee

### 3.2.4 Utekelezaji wa haki za watu wenye ualbino

Tume ilitekeleza jukumu lake la kulinda na kutetea haki za watu wenye ualbino kwa kushirikiana na wadau kama vile UNESCO, Tanzania Albino Society (TAS) na Under the Same Sun (UTSS). Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume ilishiriki maadhimisho ya siku ya kitaifa na kimataifa ya watu wenye ualbino, kutoa mada kwenye warsha na matamko katika vyombo vya habari, kukagua sehemu wanazoishi watoto wenye ualbino na kufanya mikutano na wadau mbali mbali kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kukomesha mauaji dhidi ya watu wenye ualbino.

#### *3.2.4.1 Ukaguzi wa Vituo Wanavyoishi Watoto Wenye Ualbino*

Tume ilifanya ukaguzi wa vituo vya Buhangija katika wilaya ya Shinyanga na Mitindo iliyopo Wilaya ya Misungwi ambavyo watoto wenye ualbino wanaishi na kuhifadhiwa kwa ajili ya usalama wao. Pia, ukaguzi ulifanyika katika Shule ya Msingi ya Alliance iliyoko mkoani Mwanza yenye watoto wenye ualbino. Lengo la kaguzi hizi ilikuwa ni kutathmini hali ya haki za binadamu na maslahi ya watoto wenye ualbino katika vituo na shule hizo na kutoa mapendekezo ya kuboresha mazingira ya vituo husika.

#### *3.2.4.2 Ushiriki Katika Warsha Kuhusu Haki za Watu Wenye Ualbino*

Tume ilishiriki katika warsha mbali mbali zilizokuwa na lengo la kuongeza uelewa wa jamii kuhusu haki ya kundi hili na pia mikakati ya kupambana na ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino nchini. Kwa mfano, warsha na mafunzo juu ya uhusiano kati ya Ualbino na makundi mbali mbali katika jamii iliyofanyika kanda ya ziwa katika wilaya za Kahama, Sengerema, Misungwi na Bariadi. Warsha hizi ziliandaliwa na kuratibiwa na Shirika la UNESCO nchini.

#### *3.2.4.3 Maadhimisho ya Siku ya Watu Wenye Ualbino*

Tume ilishiriki katika maadhimisho ya siku ya watu wenye ualbino ambayo hapa nchini yalifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Maadhimisho hayo ambayo kauli mbiu yake ilikuwa ni “Dumisha Amani na Ulinzi Katika Jamii Kwa Watu Wenye Ualbino” yalikuwa na lengo la kuimarisha utetezi na ulinzi wa haki za watu wenye ualbino na kuimarisha mikakati ya kukomesha ukatili na mauaji ya watu wa kundi hili.

Tume iliitisha mkutano na Waandishi wa Habari na kutoa tamko juu ya utetezi na uelimishaji umma kuhusu haki za watu wenye ualbino katika ofisi za Tume na ilishirikisha wadau kutoka sekta za umma na asasi za kiraia na kimataifa.

Siku ya kilele cha maadhimisho siku ya kimataifa ya watu wenye ualbino ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Arusha, Tume ilitoa mada kuhusu dhana ya ualbino, changamoto na mikakati ya kutokomeza vitendo vya ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino. Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ambayo kilele chake kilikuwa tarehe 11/06/2015 alikuwa mhe. Jakaya Kikwete, raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hotuba yake, Mhe. Rais alilaani kwa vikali vitendo vya ukatili na mauaji wanavyofanyiwa watu wenye ualbino na kutoa rai kwa kila mwananchi kuheshimu na kulinda haki za wengine. Pia aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia watuhumiwa wa vitendo vya ukatili na mauaji ili kukamilisha upelelezi ili kesi zilizopo mahakamani ili zisikilizwe na kukamilishwa kwa wakati. Vilevile aliwasihi viongozi wa madhehebu mbalimbali waendelee kutoa elimu kwa waumini wao yenye lengo la kujenga jamii yenye kupenda, kuheshimu na kuthamini utu wa binadamu.

### *3.2.44.4 Mikutano na Wadau wa Haki za Watu Wenye Ualbino*

Tume kama mdau muhimu wa haki za watu wenye ualbino nchini ilifanya mikutano na wadau mbali mbali kama mkakati wa kuimarisha ulinzi na kukomesha ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino. Wadau hao ni pamoja na: Shirika la kiraia la Under The Same Sun (UTSS), Wawakilishi wa vyama vya michezo, Tanzania Albino Society na Shirikisho la Mpira wa miguu Tanzania (TFF).Tume ilifanya mikutano na wawakilishi wa vyama vya michezo kwa lengo la kujadili namna michezo hususan mashindano ya mpira wa miguu inavyoweza kusaidia katika jitihada za kukabiliana na vitendo ya ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino. Katika majadiliano hayo washiriki walikubaliana kuandaa ujumbe ambao utawafikia wananchi pamoja na wanamichezo kwa njia ya vyombo vya habari na kuandaa mabango ambayo yatabeba ujumbe katika viwanja mbalimbali wakati michezo inaanza na ikiendelea uwanjani.

### *3.2.4.5 Mkutano wa Afrika kupinga ukatili dhidi ya watu wenye ualbino*

Katika hatua nyingine Tume kwa kushirikiana na Mtaalam wa Watu Wenye Ualbino wa Umoja wa Mataifa Bi. Ikponwosa Ero ilifanya Kongamano lililoshirikisha wanasiasa, na wataalamu wa haki za binadamu na maendeleo ya jamii na wawakilishi wa watu wenye ualbino kutoka baadhi ya nchi za Afrika kujadili haki, ulinzi na maendeleo ya watu wenye ualbino Afrika.




*Sehemu ya washiriki wa Komgamano la Kutoka kushoto ni Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa Mr Bwana Alvaro Rodriguez, Bwana Isaac Mwaura (Mb) toka Kenya, Mh. Abdalah Possi(Mb) Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu wenye Ulemavu na Bi. Ikponwosa Ero Mtaalam wa Watu Wenye Ualbino wa Umoja wa Mataifa*

Kongamano hilo liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu , Ofisi ya Umoja wa Mataifa nchini ( *the UN Country Team in Tanzania)* Benki ya Dunia (*The World Bank*), Asasi ya Standing Voice, Asasi ya Under The Same Sun, Balozi za nchi za Norway, Ireland Canada na USA nchini.




*Mh. Naibu Waziri Abdala Possi (Mb) akihojiwa na waandishi wa ulinzi na maendeleo ya watu wenye ualbinism Afrika habari katika kongamano la huo.*

Kongamano hilo lilofanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 17-19 Juni 2016 ulishirikisha wawakilishi wa taasisi za kiserikali, Bunge na Asasi za kiraia kutoka katika nchi za Msumbiji, Kenya, Nigeria, Senegal, Niger, Mali,Liberia, Tanzania, Namibia, Uingereza, Afrika Kusini, Malawi na Namibia.

a) Kutambua hatua halisi ili kumaliza mashambulizi dhidi ya watu wenye ualbino, kushughulikia ulinzi na kuhakikisha watu wanaojihusisha na biashara za viungo wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.
b) Kuainisha kanuni za mwongozo na sera za jumla juu ya watu wenye ualbino ambazo serikali inaweza kuzitumia kuweka mikakati katika ngazi ya kitaifa na kwa ufanisi kushughulikia masuala ya haki za binadamu kwa watu wenye ualbino

Maazimio yafuatayo yalitolewa katika mkutano huo:-

a) Serikali za nchi za kiAfrika kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya haki za watu wenye ualbino zianzishe mfumo wa kutunza taarifa ili kuhakikisha mahitaji na haki zao zinaingizwa kwenye mpango wa kitaifa na halmashauri zote nchini
b) Serikali zihakikishe masuala yanayohusu matibabu ya watu wenye ualbino yanapewa kipaumbele.
*c)* Nchi za Kiafrika ziimarishe ushirikiano katika utetezi na uhamasishaji wa kutokomeza ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino ifikapo 2030 ili iendane na agenda ya maendeleo endelevu. *(‘SDGs: leave no one behind’.).*

## 3.3 Elimu, Mafunzo na Uhamasishaji kwa Umma

Tume ilitekeleza jukumu lake la kueneza elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa, na ya kiraia yenye uzoefu katika ukuzaji na utetezi wa haki za binadamu na misingi utawala bora.

### 3.3.1 Elimu kwa kutumia machapisho na vipindi vya redio na luninga

Tume iliandaa na kusambaza machapisho mbalimbali na kwa kupitia mabango, majarida, vijitabu, vya elimu kwa umma. Nakala **11,440**, za machapisho hayo zilisambazwa kwa wananchi katika mikutano ya hadhara, semina za mafunzona katika maonesho mbalimbali ambayo Tume ilishiriki. Aidha, Makamishna na watumishi wa Tume washiriki katika vipindi katika luninga na redio, lengo likiwa kufikisha ujumbe kwa wananchi wengi zaidi.

Tume ilishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MoEVT) kuanzisha na kuvisaidia vilabu vya haki za binadamu shuleni, vyuoni, taasisi za elimu ya juu na katika jamii. Kuanzishwa na kuimarishwa kwa klabu hizo kunalenga kuendeleza elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa wanafunzi ili kujenga utamaduni wakuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora

Tume ilitumia tovuti yake kutangaza taarifa za matukio sabini na saba (77) ya utekelezaji wa kazi za Tume. Uwepo wa taarifa hizi unatoa fursa kwa wananchi na wadau kufahamu kazi za Tume, kupata taarifa mbalimbali wanazozihitaji na elimu ya masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Aidha, Tume ilitoa matamko kumi na tatu **(13)** kuhusu masuala mbalimbali, na kufanya mikutano takriban saba (7) na waandishi wa habari kwa lengo la kutoa taarifa mbalimbali kwa umma, ikiwemo matamko ya kulaani vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

### 3.3.2 Kushiriki katika Maadhimisho ya Kitaifa na Kimataifa

Tume ilishiriki kwenye maadhimisho mbalimbali yakiwemo ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika, tarehe 21 Oktoba 2015, siku ya Haki za Binadamu Ulimwenguni, tarehe 10 Desemba, 2015, Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 16 – 23, 2016), Siku ya Watetezi wa Haki za Binadamu Duniani, Aprili 27, 2016) na Wiki ya Sheria Tanzania (Januari 30 – Februari 3, 2016). Kupitia shughuli hizi Tume iliwafikia wananchi wengi na walinufaika na elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, pamoja na msaada wa kisheria uliokuwa ukitolewa, wakati wa kuadhimisha baadhi ya siku hizo.

#### *3.3.2.1 Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu*

Katika kuendeleza elimu Tume iliratibu maadhimisho ya Kumbukumbu ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu yanayofanyika kila mwaka tarehe 10 Desemba. Kabla ya siku ya kilele cha maadhimisho hayo, ulifanyika mdahalo wa wadau wa haki za binadamu kuhusu utekelezaji wa Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu, yaani, *Sustainable Development Goals* (SDGs) katika shughuli za maendeleo ya taifa

Sherehe za kilele cha maadhimisho hayo zilifanyika katika Viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa wawakilishi wa taasisi za kiserikali na za kiraia, mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, na wawakilishi wa wanafunzi toka vyuo na shule mbali mbali za Dar es Salaam. Kauli mbiu ya mwaka 2015 ilikuwa **Haki Zetu, Uhuru Wetu Daima** (*Our Rights, Our Freedoms, Always*)



***Mhe. Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitoa hotuba siku ya kilele cha maadhimisho ya Haki za Binadamu Disemba 10, 2015 zilizofanyika katika Ukumbi wa mikutano Karimjee –Dar es Salaam***

Katika hotuba yake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliwaasa Watanzania kuchukua hatua za makusudi kuanzisha kampeni maalum za kukuza maadili katika sehemu za kazi, kuboresha mazingira ya upatikanaji na utoaji wa Haki za Binadamu nchini, na kukemea ongezeko la matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini kama yale ya mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, mauaji ya wanawake wazee, ghasia zinazohusiana na vurugu za makundi; Mahabusu kuwekwa rumande muda mrefu kabla ya kesi kusikilizwa, unyanyasaji dhidi ya wanawake, unyanyasaji wa watoto ikiwemo ukeketaji, ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni, mauaji kwa wanaozaliwa na ulemavu, utekaji nyara na ajira mbaya. Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahahakikshia Watanzania kuwa Serikali ya Awamu ya tano imejipanga vema kukabiliana na uovu huo bila kumwonea huruma mtu yeyote anayejihusisha na maovu hayo.



*Brass Band ya Jeshi la Magereza ikiongoza maandamano kuelekea katika Viwanja vya Karimjee*

### *3.3.2.2 Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu ya Afrika*

Tume ilishirikiana na shirika la kimataifa la kuhudumia wazee, Help Age International, Tanzania (HAI) kuandaa maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu ya Afrika ambayo huadhimishwa barani tarehe 21 Oktoba Afrika kila mwaka. Maadhimisho haya hufanyika siku mkataba wa Afrika wa Haki za Binadmu na Watu wa mwaka 1981( African Charter on Human and People's Rights) ulipoanza kutekelezwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika. Lengo la maadhimisho haya lilikuwa ni kutathimini utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu hapa nchini.

Kwa kutambua umuhimu wa siku hiyo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la kuhudumia wazee Help Age International ilifanya maadhimisho kwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa haki za Wazee nchini. Maadhimisho hayo yalitanguliwa na warsha ya wadau wa haki za binadamu tarehe 20/10/2015 kutathmini hali na utekelezaji wa haki za wazee nchini.

Tathmini hiyo ilibainisha kwamba, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali na asasi za kiraia kutekeleza haki za wazee , bado kuna changamoto zinazokabili utekelezaji wa haki na ustawi wa wazee. Changamoto hizo ni pamoja na;-

a) Kutofaidika na mafao ikiwemo ya mifuko ya hifadhi ya jamii) pamoja na kwamba walitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.
b) Wazee kutopata huduma muafaka za afya na matibabu na sera na sheria
c) Kutokuwepo kwa sheria maalum ya kushughulikia maslahi na na haki za wazee.
d) Umaskini wa kipato na hali ngumu ya maisha kwa wazee,
e) Wazee kutokuwa na uwakilishi katika vyombo na ngazi mbalimbali za maamuzi
f) Unyanyasaji na unyanyapaa kwa wazee.
g) Usalama mdogo na mauaji , ukatili na mateso kwa wazee

Mgeni rasmi wa Siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku hiyo alikuwa Mhe Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya pili. Baadhi ya viongozi waliohudhuria ni Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mwakilishi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliyoko Arusha, na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP). Sherehe hiyo ilihudhuriwa na Balozi wa nchi 20 za Afrika na wawakilishi wizara na idara za serikali, Mashirika ya Kimataifa, asasi za kiraia na za kidini. Kauli mbiu ya maadhimisho nchini ilikuwa ni ***" Kulinda na Kutetea Haki na wa Ustawi wa Wazee"*** ka**ma** ***kundi athirika na lililosahaulika katika kutet***ewa na kusemewa



***Mgeni rasmi Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya pili Mhe Ali Hassan Mwinyi akihutubia washiriki na wageni waalikwa katika kilele cha maadhimisho ya siku ya haki za binadamu ya Afrika 21/10/2015 kwenye hotel ya New Afrika Dar es Salaam.***

Katika hotuba yake, Mgeni rasmi alisisitiza umuhimu wa jamii kuzitambua na kuzisimamia haki za wazee kwani kila mmoja katika jamii ni mzee mtarajiwa na kushauri serikali kutengeneza mazingira yatakayowezesha wazee kupata haki za msingi.

Mzee Mwinyi alilaani mauaji ya wazee kutokana na imani potofu za kishirikina na kutoa wito kwa Serikali kuchukua hatua stahiki zitakazokomesha ukiukwaji huo wa haki ya wazee ya kuishi. Mgeni rasmi alihitimisha hotuba yake kwa kupongeza jitihada na huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali zikiwemo *Help Age International* na mpango wa TASAF kuhusu huduma kwa wazee, kaya maskini. Hali kadhalika, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua iliyoichukua ya kuhudumia wazee kwa kutoa huduma za afya na malipo ya pensheni jamii kwa wazee wote.

Mapendekezo ya mkutano huo ya kuboresha haki za wazee yaliyosomwa mbele ya Mgeni Rasmi na mwakilishi wa wazee. Wazee hao walimwomba Mzee Mwinyi kuyakabidhi Serikalini kwa utekelezaji. Maadhimisho hayo yaliridhia maazimio yafuatayo;

- **TASAF** iendelee kutoa kipaumbele kwa wazee katika miradi ya kunusuru kaya masikini ili kuwafikia na kuwanusuru wazee wote nchini, kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.
- **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala (THBUB)** kwa kushirikiana na **Idara ya Ustawi wa Jamii na CSOs** iongeze jitihada za kuhamasisha wananchi nchini kote kulinda kukuza na kutetea haki na ustawi wa wazee nchini

  a) **Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**; zianzishe mabaraza ya wazee kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya wazee ya mwaka 2003 ili mahitaji ya wazee kila wilaya yazungumzwe na kupata majibu ya haraka kutoka kwenye mamlaka husika za serikali.

b) **Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa** kwa kushirikiana na **Idara ya Ustawi wa Jamii** wahakikishe na kuiwezesha Tanzania inashiriki kikamilifu katika vikao vya Umoja wa Mataifa na vya Afrika vinayvohusu haki na ustawi wa wazee .

c) **Serikali** kupitia **Idara ya Ustawi wa Jamii**; ikamilishe mchakato unaoendelea wa kutunga sheria ya wazee unakamilika ili haki maslahi na mahitaji ya wazee yalindwe kisheria.

d) **Serikali kwa kuishirikisha Jamii; ihakikishe** inaweka mikakati endelevu ya kukomesha kutokomeza mauaji ya wazee yanayochangiwa kile kinachojulikana kama imani za kishirikina. Mauaji haya yanavunja haki za binadamu na kuitia doa na aibu kubwa nchi yetu.

**e) Madhehebu ya Dini yahakikishe** yanawajengea waumini wake na jamii kwa ujumla hofu juu ya Mungu na upendo miongoni mwao ili jamii iheshimiane na kuthaminiana jambo litakalokomesha chuki na imani potofu zinazochangia mauaji ya wazee nchini hasa kwenye mikoa ya kanda ya ziwa.

f) **Serikali** kupitia Wizara ya **Katiba na Sheria**; ianishe haki za wazee kwenye Katiba pendekezwa kama za makundi mengine zilivyoainishwa katika Katiba hiyo.

g) **Serikali** kupitia **Wizara ya Fedha, Mifuko ya Hifadhi za Jamii na Idara ya Ustawai wa Jamii** itekeleze kwa vitendo malipo ya pensheni/hifadhi jamii kwa wazee wote nchini wakiwemo wakulima wafanyabiashara na wastaafu kutambua mchango wao kwa taifa letu wakati wakiwa na nguvu za kuzalisha.

h) **Tume ya kurekebisha Sheria**; ipitie na kupendekeza maboresho sheria ya Uchawi, Sura18 ya Sheria za Tanzania.

i) **Serikali** kupitia **Wizara ya fedha na Ofisi ya Rais;** iongeze kasi kutekeleza mipango endelevu ya kurasimisha mali za wazee hususan urasimishaji wa ardhi

j) **Wizara ya Afya;** itenge madaktari na madirisha maalumu kutekeleza mpango wa utoaji wa huduma za afya muafaka ,kwa wakati na bure kwa wazee katika hospitali zote za serikali nchini.

**k) Halmashauri za miji na wilaya;** zitenge bajeti katika vyanzo vyake vya mapato kusaidaia familia za wazee wanaoishi na kulea yatima

**l) Serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii** ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili kutoa huduma za wazee katika makazi yanayoendeshwa na serikali yanakidhi viwango vya kimataifa na vilivyoainishwa katika sera ya nchi ya wazee ya mwaka 2003

## 3.3.3 Mafunzo ya haki za watu wanaoishi maisha ya asili

***3.3.3.1 Mafunzo juu ya utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili***

Tume iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa Tume na wakilishi toka katika wizara na idara za serikali kuhusu haki za watu wanaoishi maisha ya asili kwa kushirikiana na ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa (OHCHR). Washiriki walitoka katika Wizara ya Habari michezo na Utamaduni, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali, Idara ya Ustawi wa Jamii na Ofisi za wakuu wilaya ya Mbulu. Mafunzo hayo ambayo yalihudhuriwa na jumla watumishi ishirini na mbili (22) ilifanyika tarehe 21-22 Julai, 2015 jijini Arusha.

Mafunzo yalijumuisha ziara ya mafunzo kwa washiriki katika eneo la Yaeda Chini, (vijiji vya Mongo wa Mono na Domango) wilaya ya Mbulu mkoani Manyara Julai, 2015




Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwaongezea uelewa washiriki kuhusu uwepo, utambuzi na utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili, mfumo wa maisha na changamoto zinazozikabili. Ziara hiyo iliwawezesha washiriki kujifunza hali ya maisha na changamoto zinazowakabili jamii zinazoishi maisha ya asili, hususan wa Hadzabe. Ziara hiyo ilitoa fursa kwa Tume kutathmini utekelezaji wa haki zao na kutoa elimu ya haki za binadamu kupitia mikutano ya hadhara, majadiliano na mahojiano na jamii ya wa Hadzabe.



***Baadhi ya wawakilishi wa jamii ya Wahadzabe wakitoa maoni yao wakati wa mkutano uliofanyika katika kijiji cha Mongo wa Mono***

Mada zilizowasilishwa na wataalamu wa kimataifa na wa hapa nchini wakati wa mafunzo hayo iliwaongezea uelewa wa washiriki kuhusu mifumo na mikataba ya kimataifa na ya kikanda kuhusu ulinzi, utetezi na uhifadhi wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili. Aidha washiriki walijifunza kuhusu sera, sheria na mifumo iliyopo nchini ambazo zinahusu utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili.

Kupitia mafunzo hayo, washiriki waliweza kufahamu masuala ya uvunjwaji wa haki za binadamu na changamoto zinaziokabili kundi hili. Kwa njia ya majadiliano waliweza kuanisha mbinu za kukabiliana na changamto hizo, kubadilishana uzoefu kutoka nchi nyingine na kuandaa mikakati ya ushawishi na utetezi katika kulinda na kutetea haki za watu wanaoishi maisha ya asili.

Ziara ya mafunzo iliyofanyika katika vijiji vya Mongo wa Mono na Domango katika eneo la asili la Wahadzabe, Wilayani Mbulu iliwawezesha washiriki kujifunza kuhusu maisha ya asili ya wahadzabena kama vile chakula, mavazi, vifaa wanavyotumia na nyumba wanazoisha. Hali kadhalika, washiriki walijifunza changamoto zinazowakabili Wahadzabe kama vile tatizo la chakula, afya, elimu, maji, ukame na mabadiliko ya tabia ya nchi na umaskini.

**_3.3.3.2 Mafunzo_ kwa viongozi wa Halmashauri wanazoishi watu wanaoishi maisha asilia**

Tume ilifanya semina nyingine Kwa kushirikiana na asasi ya kiraia ya PINGOs Forum Kwa kushirikiana na asasi ya kiraia ya PINGOs Forum kuwajengea uwezo viongozi wa Serikali za Mitaa kutoka wilaya za Mbulu, Kiteto, Babati, Simanjiro, Hanang, Karatu, Arusha Mjini, Monduli, Ngorongoro na Aru-Meru kutoka mikoa ya Manyara na Arusha.kuhusu uwepo, utambuzi na utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili yaliyofanyika tarehe 27 -28, Julai, 2015 mjini Arusha. Mafunzo hayo yalifanyika kwa ufadhili wa Asasi ya kimataifa ya nchini Denmark linaloshughulikia ya masuala ya watu asilia- International Working Group for Indigenous Affairs –IWGIA

Mafunzo hayo yalikuwa ni sehemu ya mradi wa mwaka mmoja ambao ulihusu utambuzi na utekelezaji wa Haki za watu wanaoshi maisha ya asili nchini Tanzania. Washiriki wa semina hii walikuwa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa wilaya zilizotajwa.



*Sehemu ya washiriki wa semina ya uhamasishaji wa viongozi Serikali za Mitaa juu ya utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili*

Aidha, washiriki walitaja changamoto ambazo halmashauri zao zinakabiliana nazo katika kutoa huduma kwa jamii hizi. Changamoto hizo ni pamoja na; utamaduni wa kutokuwa na makazi ya kudumu na maeneo wanayoishi, aina ya mfumo wa uzalishaji na mahitaji ya chakula,imani yao kuhusu tiba za jadi, kubadilika kwa tabia nchi, na uvamizi wa maeneo yaona jamii za kifugaji.

(a) Washiriki walisisitiza jukumu la msingi na wajibu wa serikali kulinda, kukuza na kuheshimu haki za watu asilia. Umma kwa ujumla wanatakiwa kutekeleza wajibu wao na pia kuhakikisha kuwa watu asilia wanafaidika na haki zao. Washiriki waliafiki umuhimu wa kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kwa makundi haya kwa kuzingatia mfumo wa maisha yao ya asili ya kuhamahama, na kuendelea na kampeni za ushawishi na utetezi ili watu asilia watambuliwe rasmi. Washiriki walipendekeza kuanzisha na kutekeleza miradi ya ustawi wa watu asilia.
(b) Kutengeneza sheria ndogo ndogo zinazotambua ustawi na haki za watu asilia na kuwashirikisha kikamilifu.
(c) Kuongeza programu za uhamasishaji na elimu kuhusu uwepo wa watu asilia na haki zao hususan miongoni mwa viongozi wa serikali na umma kwa ujumla.
(d) Kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kwa makundi haya kwa kuzingatia maisha yao ya asili ya kuhamahama.
(e) Kuendelea na kampeni za ushawishi na utetezi ili watu asilia watambuliwe rasmi kupitia sheria maalum na sera pamoja na utekelezaji wa haki zao.

### 3.3.4 Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa/Kikanda na Kitaifa

Tume iliendeleza ushirikiano na taasisi mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa. Kifungu cha 6(1)(m) cha Sheria ya Tume Na. 7 ya mwaka 2001 (Sura ya 391ya Sheria za Tanzania toleo la 2002) kinaitaka Tume kushirikiana na taasisi za Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Madola taasisi nyingine za kimataifa zinazoshughulika na haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

#### *3.3.4.1 Ushirikiano na Taasisi za kitaifa*

Kifungu cha 14(2) cha Sheria ya Tume kinazitaka serikali na taasisi zake, asasi na watu binafsi kushirikiana nayo katika kufanikisha majukumu yake. Tume ilipata ushirikiano wa kuridhisha kutoka Serikalini katika kutekeleza majukumu yake, hata hivyo baadhi ya taasisi hazikutoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza mapendekezo ya Tume.

Tume ilitembelea katika mifuko ya hifadhi ya jamii mkoani Dar es Salaam ikiwemo . Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF), Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF kwa malengo ya kufahamiana kujifunza kuhusu masuala ya kiutendaji na changamoto zinazojitokeza katika kushughulikia malipo ya mafao ya mifuko iliyo chini ya Mamlaka hiyo. Ziara hizo zilihitimishwa kwa Tume kutembelea Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya jamii (SSRA). Katika ziara hizo Tume ililenga pia, kutathmini uzingatiaji wa sheria zinazosimamia mifuko hiyo, hasa katika kutoa haki za mafao kwa wastaafu baada kufuatia malalamiko ya ya uchelewashwaji wa malipo ya

wastaafu yaliyofikishwa Tume. Kwa mwaka 2016/2017, Tume ilipokea na kuchunguza malalamiko 21 yanayohusu haki za mafao.

**Jedwali 3.1 Malalamiko yaliyopokelewa Tume dhidi ya mifuko ya jamii 2015/2016.**

| Mfuko | Kupunjwa mafao | kutolipwa mafao | Madai ya pensheni | Kukiukwa taratibu za mirathi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| GEPF | 1 | | | | 1 |
| NSSF | 2 | 1 | 2 | | 5 |
| PSPF | 2 | 4 | 1 | | 7 |
| PPF | | | 4 | | 4 |
| LAPF | 2 | 1 | | 1 | |
| | | | | | |
| Jumla | 7 | 6 | 6 | 1 | 21 |

**Chanzo THBUB 2016**

Pamoja na kufuatilia malalamiko hayo ilitumia fursa hiyo kubadilishana uzoefu na kupanga mikakati ya pamoja katika kuyapatia ufumbuzi kwa wakati malalamiko yanayoletwa Tume dhidi ya mifuko hiyo. Katika mjadala inayohusu kucheleweshwa kwa malipo katika mifuko ya jamii ilielezwa kuwa ucheleweshaji wa malipo ya mafao kutoka katika mifuko ya hifadhi ya jamii nchini unasababishwa na kuanzishwa kwa kituo kimoja kikuu cha malipo ya mishahara ("*Centralization of payroll")* ambapo, mishahara ya watumishi hutumwa na Hazina moja kwa moja kwa watumishi na makato yao kupelekwa kwenye mifuko. Hii imekuwa ikileta usumbufu kwani Hazina imekuwa ikituma fedha hizo za michango bila ya mchanganuo ya mwanachama yupi na wa taasisi gani.



***Makamu Mwenyekiti wa Tume Mh. Iddi Ramadhani Mapuri akikabidhi vipeperushi kwa Afisa Mafao Mkuu wa NSSF Bi. Christina Kamuzora***

Aidha, ilibainika kuwa waajiri kutowasilisha michango kwa wakati. Hivyo kusababisha ama kuchelewa au kutolipwa kwa mafao ya wastaafu kwa wakati. Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa, Tume na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) ziliona umuhimu wa kuweka utaratibu maalum wa kushughulikia malalamiko yanayoelekezwa katika mifuko hiyo.

- Namna ya kukabiliana na waajiri wanaodanganya kuhusu kiasi cha mshahara wanaolipwa watumishi wao tofauti na ile ilioandikwa kwenye mikataba
- Umuhimu wa SSRA kusaidia mifuko inayosumbuliwa na waajiri wasiolipa michango yao kwa wakati.
- Kuwa na mkakati wa pamoja wa utoaji elimu kuhusu Sheria Na. 8 ya 2008 hasa kifungu cha 8 (i) kinachoelezea wajibu wa SSRA kwa kushirikiana na taasisi nyingine kuhakikisha kuwa wanachama katika mifuko ya mafao wanakuwa na uelewa wa sheria, taratibu na huduma za mifuko husika.
- Kuwepo na mkakati wa SSRA kuhakikisha kuwa pensheni inapopandishwa inalipwa kwa wakati ili kuondoa ucheleweshwaji unaopelekea malalamiko.
- Kufanya utafiti kwa tatizo ambalo limeanza kujitokeza la malalamiko ya kupunjwa malipo ya mafao kwa kutozingatiwa muda wa utumishi wa watumishi walioajiriwa awali kwenye kada ya uongozi (Katibu Tarafa) baadae kuhamishiwa kwenye utumishi wa umma na kuanza kuchangia kwenye mifuko kutozingatiwa kwa muda.

Kwa ujumla matokeo ya ziara hizo ni pamoja na kufanikiwa kujenga mahusiano kati ya Tume ya mifuko hiyo. Aidha, malalamiko ya Tume yameanza kujibiwa kwa wakati. Pia kila mfuko umeteua Afisa (Focal Persons) wa kushughulika masuala ya Tume. Utaratibu huu umefanikisha ufuatiliaji wa malalamiko kuimarika na haki zao kupatikana kwa wakati.

### *3.3.4.2 Ushirikiano na Asasi za Kiraia*

Aidha, Tume ilishirikiana na asasi za kiraia katika kuhamasisha elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Taasisi hizo ni pamoja na PINGOs Forum, taasisi ya *Association for Law and Advocacy for Pastoralists* (ALAPA), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, (LHRC), *Under the Same Sun,* (UTSS), *Tanzania Human Rights Defenders' Coalition* (THRDC) na mtandao wa *Policy Forum*. Ushirikiano kati ya Tume na taasisi hizi ulihusu mafunzo juu ya masuala mbali mbali ya haki za binadamu na ufuatiliatiaji wa hali ya haki za binadamu nchini, yakiwemo maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015 na utayarishaji wa taarifa ya Tanzania katika Mzunguko wa 2016 Kujitathmini kwenye Baraza la Haki za Binadamu a Umja wa Mataifa mwezi Mei 2016 (*UPR 2016 Circle*). Ushirikiano huu ulichangia Tume kutekeleza majukumu yake ya kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora.




***Mwenyekiti wa Tume ,Mhe. Bahame Tom Nyanduga akizindua Ilani ya Uchaguzi ya Azaki Tanzania katika ukumbi wa Millenium Towers Kijitonyama Jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Dr. Helen Kijo Bisimba na kulia ni Bw Onesmo Ole Ngurumwa, Afisa Mtendaji wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Oktoba 2015.***

### 3.3.5 Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa na Kikanda

Katika kipindi hiki Tume ilishirikiana na taasisi za kimataifa katika kutimiza majukumu yake ya kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za biadamu na misingi ya utawala bora nchini. Taasisi hizo ni pamoja na African *Ombudsman and Mediators Association* (AOMA),UN Tanzania na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja Wa Mataifa linaloshughulikia Haki za Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni(UNESCO), Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu (OHCHR), Mahakama ya ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), Shirika la Umoja wa Mataifa linalosaidia Kilimo (IFAD) na Asasi isiyo ya kiserikali ya nchini Denmark inayoshughulikia ya Masuala ya Watu wanao ishi maisha ya Asilia IWGIA, Umoja wa Tume za Haki za Binadamu Duniani, (GANHRI) na Umoja wa Tume za Haki za Binadamu Afrika, (NANHRI)

#### *3.3.5.1 Ushirikiano na AOMA katika maandalizi ya maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi Tanzania*

Mkutano Mkuu wa nne wa AOMA, yaani Umoja wa Tume za Uchunguzi barani Afrika, uliofanyika mwezi Novemba, 2014 huko Addis Ababa, Ethiopia uliiteua THBUB kuandaa Mkutano Mkuu wa Tano wa AOMA. 50 tangu kuanzishwa kwa Tume ya Kudumu ya

Uchunguzi Tanzania mwaka 1965, ikiwa ni Tume ya Uchunguzi ya kwanza baraniAfrika. Hata hivyo Mkutano huo haukuweza kufanyika kama ilivyopangwa kutokana na ufinyu wa bajeti.



***Pichani Mwenyekiti wa Tume Mhe. Bahame Nyanduga (aliyekaa katikati) na Katibu Mkuu wa AOMA Dr. Ottiende Amolo ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchunguzi Kenya, (wa pili kulia) alipoitembelea Tume kufuatilia maandalizi ya Mkutano Mkuu wa AOMA. Mkutano huo ulitarajiwa kufanyika Mwezi, Septemba, 2016 Jijijni Arusha, Tanzania.***

### *3.3.5.2 Ushirikiano na IWGIA katika kukuza haki za watu wanaoishi maisha ya asili*

Tume ilishirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya nchini Denmark inayoshughulikia Masuala ya Watu Asilia- "International Work Group for Indigenous Affairs" (IWGIA) kuzindua taarifa ya utafiti kuhusu hali ya haki za watu wanaoishi maisha asilia uliofanywa na Kikosi Kazi cha Tume ya Haki za Binadamu na Watu African Commission on Human and Peoples Rights (ACHPR) tarehe 26 Novemba, 2015

*The Report Of The African Commission's Working Group on Indigenous Populations/Communities: Research And Information Visit to The United Republic of Tanzania, 2015.*



*Makamu Mwenyekiti wa Tume Mheshimiwa Idd Ramadhan Mapuri, akiwa na Katibu wa Tume Bibi. Mary Massay, na Dr. Naomi Kipuri (aliyeko kulia wa Mjumbe wa Kikuundi Kazi la Haki za Watu waishi maisha ya Asili la ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR – WGIP)*

Uzinduzi wa Taarifa hiyo ulilenga kuongeza uelewa wa wananchi na viongozi juu ya hali ya haki za watu wanaoishi maisha ya asili Tanzania. Aidha, ililenga pia, kuendeleza majadiliano ya kuwatambua na kutekeleza haki za kundi hili nchini Mjadala huo ulitarajiwa pia kubuni mikakati na mbinu za kuhakikisha kuwa wananchi na viongozi wanaelewa, kusimamia na kuboresha haki za watu wanaoishi maisha ya asili nchini.Taarifa hiyo ya Utafiti ilibaini mambo yafuatayo kuhusu jamii za watu wanaoishi maisha ya asili;

(i) Kutengwa na unyanyapaa
(ii) Kutotambulika kisheria
(iii) Kuhamishwa kwa nguvu katika maeneo yao ya asili kutokana na shughuli za maendeleo uwekezaji na uhifadhi
(iv) Kuathirika kwa mila na desturi za asili

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na washiriki 65 kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Asasi za Kiaraia za haki za binadamu na haki za watu wanaoishi maisha ya asili pamoja na waakilishi wa mashirika ya kimataifa.

Katika Hafla hiyo,pia Tume iliwasilisha taarifa yake ya Mradi wa Utambuzi na Utekelezaji wa Haki za Watu waishio Maisha ya Asili Tanzania uliofadhiliwa na IWGIA na kutekelezwa kwa ushirikiano kati ya Tume na Asasi ya PINGOs forum kati ya mwezi Julai 2014 na Agosti 2015. Taarifa zote zilijadiliwa kwa kina na kusaidia kuongeza uelewa wa washiriki juu ya maisha na utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha ya asili nchini.



*Mwakilishi wa Wizara ya Mali Asili na Utalii akichangia jinsi Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori ya Mwaka 2009 (Wildlife Conservation Act of 2009) na kanuni zake zinavyozingatia haki za jamii za asili na majirani zake.*

Baada ya ya mjadala, washiriki walitoa mapedekezo yafuatayo kwa THBUB, Serikali na wadau wengine;

1. Serikali na taasisi mbali mbali kuongeza kasi ya kutoa elimu juu ya maisha na haki za watu wanaoishi maisha ya asili kama zilivyoainishwa kama Mikataba ya Kimataifa ambayo Nchi yetu ni mwanachama au imekubaliana nayo.
2. Serikali kufanya utafiti wa kina juu ya utekelezaji wa haki za watu wanaoishi maisha asili nchini Tanzania kama ilivyoahidi katika taarifa zake kwenye Taasisi za Kimataifa ambazo nchi ni mwanachama

3. Serikali ya Tanzania kujifunza na kuiga mifano mizuri ya Sheria za kulinda Watu wanaoishi maisha asili katika nchi jirani za Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Rwanda, Burundi, Namibia and Kenya. Nchi hizi zimeweka sheria na sera maalumu za kuendeleza na kulinda haki za watu wanaoishi maisha asili.

4. Serikali Kwa kupitia Wizara za Ardhi , Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa , Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na jamii husika kulinda ardhi na tamaduni za jamii za watu wanaoishi maisha ya asili zinazoathiriwa na biashara ya utalii, kilimo na ufugaji.
   i. .
5. Serekali kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika mijadala ya kutambua na kuendeleza haki za watu wanaoishi maisha ya asili zilizofanywa na kwa ushirikiano wa Tume na Asasi za kiraia.
6. Serikali, THBUB, Asasi za kiraia, na Washirika wa Maendeleo (Development Partners (DPs) na wadau wa haki za binadamu kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa zilizozinduliwa (ACHPR-WGIP na THBUB/PINGOs) katika kuboresha haki za watu waishio maisha ya asili
7. Wadau wote wakiongozwa na Tume kushirikiana kuandaa mpango kaz*i* ambao utakua *ni msingi* wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hizi

### 3.3.6 Taarifa ya Tathmini ya Hadhi ya Tume katika Umoja wa Mataifa

Tume iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni za Paris-(*Paris Principles*)[71] kwa Kamati ya Tathmini ya Hadhi za Tume za Haki za Binadamu Kimataifa ya Mtandao wa Tume za Haki za Binadamu Duniani (GANHRI) katika Ofisi ya Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, katika jitihada za kukamilisha zoezi la kuitathmini Tume kama bado inakidhi vigezo vya Hadhi ya "A" ya Mtandao huo. Tathmini hii hufanyika kwa Tume zote za haki za binadamu kote ulimwenguni kila baada ya miaka mitano na taarifa huwasilishwa kwa Sekretarieti ya Mtandao wa Tume za Haki za Binadamu Duniani. Moja wapo ya vigezo muhimu ni iwapo Tume ni huru kutoa maamuzi yake na ina fungu la bajeti linaloiwezesha kufanya kazi zake bila vipingamizi vya kibajeti. Tume isipokidhi vigezo hivyo inaweza kuvuliwa hadhi hiyo.

Tathmini ya mwisho ya Tume ilifanyiwa mwaka 2011 na kupewa hadhi ya daraja "A".[72] Daraja A linaiwezesha Tume kushiriki vikao vya GANHRI, (General Assembly of National Human Rights Institutions) na shughuli nyingine zinazoratibiwa na OHCHR kama vile mafunzo kwa watumishi wake kama mwanachama kamili.

## 3.4 Utoaji wa huduma za kisheria

Msaada wa kisheria nchini unajumuisha huduma za kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kugharamia huduma za mawakili. Huduma za msaada wa kisheria hujumuisha msaada na ushauri wa kisheria, uwakilishi mahakamani, uwezeshaji wa kufikia vyombo vya kutoa haki, elimu ya sheria na usuluhishi wa migogoro.

### 3.4. 1 Msaada wa sheria kwa wananchi

Katika kipindi hiki Tume ilitoa huduma za ushauri kisheria kwa walalamikaji waliofika katika ofisi zake, kuwasaidia kuandaa nyaraka za mahakamani, kuwakilisha walalamikaji mahakamani na pia kutoa elimu ya sheria kwa umma. Ushauri huu hutolewa ana kwa ana kwa waliofika ofisini, kupitia barua za kawaida na barua pepe, simu na katika mikutano ya hadhara iliyofanywa na Tume katika ziara mbalimbali za utafiti, utoaji elimu kwa umma na ukaguzi wa vituo vya polisi na magereza.

---

[71]. Kanuni hizi zinatokana na Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la mwaka 1993 (Resolution 48/134 la tarehe 20 Desemba 1993) linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha kuwa Tume za Haki za Binadamu zinawezeshwa kufanya kazi zake kwa uhuru na bila kuingiliwa.

[72] Tathmini ya awali ilifanyika mnamo mwezi Novemba 2016 na kwa sasa Tume kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mtandao wa Kidunia kwa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu - Kamati Ndogo ya Tathmini (*Secretariat of the GANRHI Sub-Committee on Accreditation (SCA),* wanaendelea na awamu nyingine ili kukamilisha mchakato wa tathmini hii.

Jumla ya wananchi **2,903** walipokea ushauri wa kisheria, miongoni mwao, wananchi **210** walipata ushauri kuhusu masuala ya mirathi, **900** kuhusu migogoro ya kazi ikiwemo, kutopandishwa vyeo, kuachishwa kazi na mafao, **1750** kuhusu migogoro ya ardhi na **43** kuhusu masuala ya haki jinai ikiwemo utaratibu wa kukata rufaa.

Kifungu cha 6(1)(e) cha Sheria ya Tume, kinaipa mamlaka ya kufungua kesi mahakamani kwa ajili ya kuzuia vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu. Jumla ya kesi nne (4) zilisimamiwa na Tume na kumalizika katika mwaka wa fedha 2015/16 ambapo ziliisha kwa walalamikaji waliokuwa wanawakilishwa na Tume kupewa haki zao. Kesi hizo ni pamoja na; Shauri la Ndoa Na. 22/2014, Kesi ya Madai Na 87/2008, Madai Namba 61/206 na Namba 13/2007. Kesi Land Revision No. 115/207 inayohusu madai ya ardhi bado inaendelea kusimamiwa na Tume katika Mahakama jijini Dar es salaam. .

## 3.4. 2 Mapitio ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa

Kifungu cha 6(1)(k) na (l) cha Sheria ya Tume Na. 7/2001, Sura 391 ya Sheria za Tanzania kinaipa Tume mamlaka ya kupitia sheria mbalimbali, kanuni, miongozo ya kiutawala na mikataba mbalimbali ya kimatifa iwapo inakidhi matakwa ya haki za binadamu na misingi ya utawala Bora. Tume ilipitia sheria mbalimbali na kuishauri serikali kuhusu umuhimu wa uwiano wa sheria hizo na haki za binadamu.

Tume ilipitia Sheria ya Takwimu Na. 9/2015 (*Statistics Act No*. 9/2015), Sheria ya Makosa ya Mtandao Na. 14/2015 (*Cybercrime Act No*. 14/2015) na Sheria ya Hati na Nyaraka za Kusafiria ya Mwaka, 2002 (*The Tanzania Passports and Travel Documents Act of* 2002)

### *3.4.2.1 Sheria ya Takwimu Na. 9/2015 (Statistics Act No. 9/2015)*

Tume ilibaini kuwa baadhi ya vifungu vinakinzana na matakwa wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya utekelezaji wa haki ya kupata na kutoa taarifa. Kwa mfano kifungu cha 20(2) kimempa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuidhinisha takwimu lakini hakijaweka ukomo wa muda kwa Mkurugenzi huyo kuthibitisha takwimu hizo. Tume iliona kuwa pasipowekwa muda maalum, mamlaka haya yanaweza kutumika vibaya na kuchelewesha uidhinishaji wa takwimu. Aidha kifungu cha 37 kinachoainisha makosa na adhabu, kimetoa adhabu kali na kubwa kwa vyombo vya habari, asasi za kiraia, taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu vinavyotenda makosa ya kutoa takwimu zitakazoonekana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa kuwa ni za uongo. Tume ilipendekeza kiwango cha faini kipunguzwe na makosa yote yalioainishwa yawekewe fani inayolingana. Uwepo wa adhabu hizo kutadumaza uhuru wa mawazo chanya yenye takwimu zisizo sahihi, ambayo yangeweza kusahihishwa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

### *3.4.2.2 Sheria ya Hati na Nyaraka za Kusafiria ya Mwaka, 2002*

Tume ilishirikiana na wadau wa haki za binadamu kupitia Sheria ya Hati na Nyaraka za Kusafiria ya Mwaka, 2002 (The Tanzania Passports and Travel DocumentsAct of 2002) kujadili changamoto zinazohusiana na hati za kusafiria za kidiplomasia, ikiwemo haja ya kuongeza wigo wa makundi ambayo hayatambuliki kisheria kupata hati hizo. Tume iliipitia Sheria hii na kubaini kuwa haina tafsiri halisi ya hati ya kidiplomasia na kutoainisha misingi ya mtu kutambulika

kama mwanadiplomasia kama ilivyo katika Mkataba wa Kimataifa wa Mahusiano ya Kidiplomasia wa Vienna wa mwaka 1961.

***3.4.2.3 Sheria ya Makosa ya Mtandao (The Cyber Crimes Act No. 14/2015)***

Tume ilibaini kuwa sheria hii ina mapungufu ambayo yanaweza kuzuia uhuru wa kutoa maoni au uhuru wa kutoa na kupokea taarifa. Kwa mfano Sheria hiyo imetoa adhabu kwa mtu yeyote ambaye kwa makusudi atapokea taarifa zisizothibitishwa kinyume na sheria, lakini haijatafsiri maana ya taarifa ambazo hazijathibitishwa. Sheria hiyo pia imewapa polisi nguvu kubwa wakati wa ukaguzi na ukamataji, haina kifungu kinachowalinda wasiri wanaotoa taarifa (whistle blowers). Hata hivyo sheria ina vifungu ambavyo vinahamasisha ulinzi dhidi ya watoto kwa kuzuia picha na video zisizo na maadili za mtandaoni kwa watoto.

Tume iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika vifungu ambavyo vinakiuka haki za binadamu ili viendane na Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Ulinzi wa Mtandao na Taarifa za Siri Binafsi wa Mwaka 2014 (*African Union Convention on Cyber Security and Personal Data Protection of 2014*) na mikataba mingine ya kimataifa kuhusu haki za binadamu.

## 3.5 Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu

Katika kipindi cha 2015/16, Tume iliendelea na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (National Human Rights Action Plan-NHRAP 2013-2017) chini ya mradi wa "*Support for National Human Rights Priorities"* unaotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ufadhili wa UNDP.

Mradi huu ulilenga; kuwajengea wananchi uelewa wa masuala ya utekelezaji wa mpango kazi na upatikanaji wa haki. (*Monitoring Access to Justice)*, kuzijengea taasisi uwezo wa kiutendaji (*Institutional Capacity Development)* kwa kuzingatia jicho la haki za binadamu (*Human Rights Based Approach*), na kufanya tathmini ya mpango kazi wa Kitaifa wa haki za binadamu (*Monitoring and Evaluation)*

### 3.5.1 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi

(i) Kutoa elimu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu kwa watumishi na wakuu wa idara 319 (wanaume 222 na wanawake 97) kutoka katika halmashauri 61 za mikoa tisa ya Tanzania Bara

(ii) Wawakilishi 74 ( 44 kutoka Tanzania bara na 30 kutoka Zanzibar) kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali-) walijengewa uelewa wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora pamoja na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu.

(iii) Nakala **3,220** za vitabu vya Mpango Kazi na nakala **2300** za machapisho mbalimbali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora ilisambazwa kwa lengo la kuongeza uelewa wa wananchi.

(iv) Maafisa 95 kutoka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali waliteuliwa kama '*Link officers'* na kujengewa uwezo wa utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu kwa Tume kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

(v) Watumishi 55 wa Tume walijengewa uwezo wa kuandaa na kuchanganua taarifa mbalimbali za kitaifa na kimataifa kwa kuzingatia majukumu ya Tume.

(vi) Wahariri 42 kutoka vyombo vya habari (magazeti, radio na TV) walijengewa uwezo na majukumu ya vyombo vya habari , kuhusu tathmini ya haki za binadamu katika utoaji taarifa katika masuala ya haki za binadamu.

(vii) Taarifa 51 kuhusu utekelezaji wa Mpango Kazi zilipokelewa kutoka *Link Officers* ambazo ziliwasilishwa Tume kwa njia ya mfumo wa kielektronik (*M & E data base system*)

(viii) Tume imeongeza wigo wa kujitangaza kwa wananchi na kueleweka majukumu yake ki-katiba na kisheria

(ix) Uratibu wa mchakato wa uandishi wa taarifa ya tathmini ya nchi ya haki za binadamu kwa mwaka 2016 (*Universal Periodic Review-UPR).* Mchakato huo uliwezesha kuandikwa kwa taarifa mbili (Taarifa ya Nchi na Taarifa ya Tume) kwenda Baraza la Haki za Binadamu huko Geneva (*Human Rights Council*) ambapo Tanzania iliwasilisha taarifa yake na kufanyiwa tathmini mwezi Mei, 2016 huko Geneva

## 3.6 Ziara ya Mhe. Rais Jakaya Kikwete Tume

Mnamo tarehe 20 Agosti2015 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembelea Tume ikiwa ni ziara yake ya kuagana na watumishi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Jakaya Mrisho Kikwete akisisitiza jambo kwa wafanyakazi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika ziara ya kumuaga mara baada ya kumaliza uongozi wake katika Serikali ya awamu ya nne.*

Katika hotuba yake mheshimiwa rais alianza kwa kutambua juhudi mbalimbali zilizofanywa na serikali katika kuhakikisha kwamba misingi ya haki za binadamu na utawala bora inaheshimiwa nchini. Aidha, Mheshimiwa Rais alitoa ufafanuzi kuhusu haki ya uhuru wa kutoa maoni na vyombo vya habari akishauri na kuelekeza vyombo vya habari kuheshimu sheria za nchi katika utoaji wa habari na utoaji wa habari uzingatie misingi na weledi wa taaluma yao. Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa uhuru usio na mipaka usipozuiliwa unaweza kusababisha vurugu na

uvunjifu wa  amani jambo ambalo haliwezi kuvumuliwa kwa namna yoyote ile ispokua kuzuia na kufungia vyombo vyovote vya  habari vinavyosababisha  uchochezi kwa wananchi



Mhe Rais (katikati) akipokea tunzo kutoka kwa *Mwenyekiti wa Tume  Tom Nyanduga akimkabidhi Mheshimiwa Rais Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete tuzo maalum kwa kutambua mchango wake katika kuboresha haki za binadamu na utawala bora nchini muda mfupi baada ya Rais Kikwete kuhutubia na kuagana rasmi na wafanyakazi wa Tume.Watatu kushoto ni Waziri wa Katiba na Sheria Dkt.Asha Rose Migiro na kulia ni Mwanasheria Mkuu wa Serkali Mh.George Masaju.*

Mwenyekiti wa  Tume Bahame Tom Nyanduga alitoa maoni yake kwa Mheshimiwa Rais kuwa katika kuelekea kipindi cha uchaguzi  vyombo vya ulinzi na usalama vitumike kwa ajili ya kulinda raia na kuhakikisha kuwa  uchaguzi unakuwa  huru na wa haki ili  kuzuia viashiria vyovyote vitakavyosababisha  uvunjifu wa amani nchini.

Aidha, Mheshimiwa Rais alitunukiwa Tuzo maalum kwa  kutambua mchango wake wa kuthamini na kuheshimu Misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika kipindi chote cha uongozi wake

# SEHEMU YA TATU

# UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA, ZANZIBAR

# SURA YA NNE:

# 4.0 UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME ZANZIBAR

Ofisi ya Tume Zanzibar ilifanya shughuli mbalimbali za kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na kupokea na kuchunguza malalamiko, kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, uangalizi wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 25, 2015 na ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar .

## 4.1 Kupokea na kushughulikia malalamiko

Kifungu cha 6 (1)(b) na (c) cha Sheria za Tume Na. 7 ya mwaka 2001 na Kifungu cha 28A(1) cha Marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2006 *(written Laws (Miscellaneous Amendments) Act )kinaipa* Tume mamlaka ya kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu masuala yanayohusu haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, visiwani Zanzibar. Tangu Ofisi ya Tume Zanzibar ianze kupokea malalamiko Julai 2001 ilikuwa imepokea jumla ya malalamiko **548.**

Tume ilipokea na kushughulikia malalamiko mapya **20** kwa mwaka 2015/2016. Aidha, Tume iliendelea na uchunguzi wa malalamiko **162** yaliyopokelewa miaka iliyopita hivyo kufanya idadi ya malalamiko yaliyoshughulikiwa mwaka huo kufikia **182**.

***Jedwali 4.1Malalamiko yaliyopokelewa na kushughulikiwa na ofisi ya Zanzibar kuanzia Julai, 2001 hadi Juni, 2016***

| Mkoa | Julai 2001 - Juni 2016 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mjini/Magharibi | 315 | 31 | 37 | 11 | 17 | 25 | 20 | 456 |
| Kaskazini Unguja | 10 | 3 | 1 | 2 | | | - | 16 |
| Kusini Unguja | 25 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | - | 31 |
| Kaskazini Pemba | 8 | 0 | 0 | - | | 1 | - | 9 |
| Kusini Pemba | 18 | 3 | 3 | - | | 1 | - | 25 |
| Mikoa ya Tanzania Bara | 9 | 0 | 0 | | | 2 | - | 11 |
| JUMLA | 385 | 38 | 42 | 15 | 18 | 30 | 20 | 548 |

Chanzo; THBUB 2016

Malalamiko yote yaliyopokelewa katika kipindi hiki yalitoka Mkoa wa Mjini Magharibi. Mkoa huo pia unaongoza kwa kuwasilisha malalamiko 456 ambayo ni asiliamia 83 ya malalamiko 548 yaliyopokelewa na ofisi ya Zanzibar kuanzia mwaka 2001.

Malalamiko yaliyopkelewa yalihusu kupigwa na kuteswa, ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi, kubambikizwa kesi, kunyanyaswa, ucheleweshaji wa malipo kutoka hazina, kutotendewa haki,

kuzuiwa kufanya kazi na madai mengine mbali mbali. Baadhi ya taasisi zilizolalamikiwa ni pamoja Idara Maalum za SMZ, Jeshi la Polisi, Halmashauri za Wilaya, shehia, Hazina, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, mamalaka ya viwanja vya ndege na watu binafsi.

**Jedwali na 4.2: Idadi ya malalamiko yaliyopokelewa kijinsia.**

| **Mwaka** | **Yaliyo Pokelewa** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Watoto** | **Makundi** | **Tume** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Yaliyorithiwa kutoka TKU | 90 | - | - | - | - | - |
| 2001/02 | 15 | 2 | 12 | - | 1 | - |
| 2002/03 | 20 | 5 | 12 | 1 | 1 | 1 |
| 2003/04 | 11 | 1 | 8 | 1 | 1 | - |
| 2005/06 | 9 | - | 9 | - | - | - |
| 2006/07 | 67 | 6 | 52 | 2 | 5 | 2 |
| 2007/08 | 104 | 11 | 75 | 3 | 12 | 3 |
| 2008/09 | 43 | 6 | 27 | 1 | 7 | 2 |
| 2009/10 | 26 | 3 | 22 | - | - | 1 |
| 2010/11 | 38 | 8 | 24 | 2 | 2 | 2 |
| 2011/12 | 42 | 6 | 32 | - | 3 | 1 |
| 2012/13 | 15 | 2 | 11 | - | 2 | - |
| 2013/14 | 18 | 1 | 12 | 1 | 2 | 2 |
| 2014/15 | 30 | 8 | 17 | 3 | 2 | - |
| 2015/16 | 20 | 7 | 8 | 1 | 2 | 2 |
| JUMLA | 548 | 66 | 321 | 15 | 40 | 16 |

Chanzo; THBUB 2016

Kati ya malalamiko 182 yaliyoshughulikiwa, uchunguzi wa malalamiko **29** ulikamilika na kuhitimishwa. Hadi kufikia mwezi Juni, 2016 idadi ya malalamiko yaliyokuwa yanaendelea kushughulikiwa yalikuwa **153**

**Jedwali na 4.3: Mchanganuo wa idadi na asilimia ya malalamiko, yaliyofungwa na yanayoendelea.**

| MWAKA | YALIYO POKELEWA | YALIYOFUNGWA | | | | YANAYO ENDELEA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyo faulu | Yasio faulu | Yaliyo achwa | Yaliyo elekezwa | |
| 2010/11 | 38 | 2 | 6 | 8 | 2 | 20 |
| 2011/12 | 42 | 5 | 6 | 8 | 7 | 16 |
| 2012/13 | 15 | 3 | 3 | 3 | 1 | 5 |
| 2013/14 | 18 | 0 | 0 | 2 | 0 | 16 |
| 2014/15 | 30 | 0 | 4 | 2 | 1 | 23 |
| 2015/16 | 20 | - | - | - | - | 20 |
| JUMLA | 548 | 106 | 109 | 143 | 34 | 153 |

**Chanzo; THBUB 2016**

## 4.2 Kufuatilia uchaguzi Mkuu

### 4.2.1 Uangalizi wa Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Tume ilifuatilia uandikishaji na boreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Unguja. Jumla ya vituo 38 vya uandikishaji na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura vilifanyiwa uangalizi katika mkoa wa kusini Unguja. Kati ya hivyo vituo, 21 ni vya Wilaya ya Kusini na 17 ni kutoka Wilaya ya Kati. Kutokana na ufinyu wa bajeti shughuli hiyo haikufanyika katika mikoa mingine ya unguja na Pemba.



***Wananchi katika kituo cha kujiandikisha cha Mtopepo, Unguja wakisubiri kujiandikisha kupiga kura.***

#### *4.2.1.1 Yaliyojitokeza wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura*

Wakati wa uandikishaji wapiga kura, Tume ilibaini mapungufu yafuatayo ambayo ni kinyume na haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

i. Pamoja na kwamba majengo mengi yaliyotumika katika uandikishaji na uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura yalikuwa karibu na makazi ya wananchi na kuwa na nafasi za kutosha lakini mazingira ya baadhi ya majengo hayo hayakuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu, wagonjwa na wazee. Aidha vituo vingine vilikuwa katika maeneo yasiyo salama kwa waandikishwaji kutokana na kuwepo pembezoni mwa barabara kuu.

ii. Kuwepo kwa matatizo ya waliopoteza shahada za kujiandikisha kupigia kura, waliohama, waliohitaji kukata rufaa na waliohitaji kurekebisha. Hata hivyo tatizo hili lilirekebishwa kwa waandikishwaji kuelimishwa kujaza fomu husika.

iii. Usumbufu katika baadhi ya vituo kutokana na mashine zilizokuwepo kushindwa kutambua vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi vya baadhi ya waandikishwaji na kutakiwa warudi muda au siku iliyofuata.

iv. Idadi kubwa ya vyama vya siasa kushindwa kuweka mawakala katika vituo vya uandikishaji. Kati ya vyama 22 vilivyopata usajili wa kudumu ni vyama viwili (2) tu vilivyoshiriki kwa asilimia kubwa kuweka wakala wa uandikishaji katika kila kituo.

v. Uwepo wa watu waliodhaniwa kuwa ni askari wa Idara maalum waliokuwa wakizunguka baadhi ya maeneo ya vituo na kuzunguka ndani ya magari yenye namba za Idara hiyo wakiwa wamevaa kiraia huku wameziba nyuso zao na kubeba silaha za jadi na za moto ilionesha kusababisha hofu kwa baadhi ya wananchi waliojitokeza kujiandikisha

vi. Malalamiko ya kuandikishwa watu wasiokuwa na sifa au kuruhusu baadhi ya watu kujiandikisha bila ya kupanga foleni hali iliyotaka kusababisha uvunjifu wa amani.

vii. Utumiaji wa magari na silaha zinazoaminika kuwa ni mali ya Serikali katika zoezi la uandikishaji daftari na raia kutishiwa usalama wa mali na maisha yao ni kinyume na sheria na utendaji kazi wa Serikali.

viii. Kitendo cha wananchi kuzuiwa na baadhi ya wenzao kwenda vituoni kujiandikisha kwenye daftari ni ukiukwaji wa Sheria.

ix. Malalamiko ya wananchi kupigwa na kundi linalojulikana kwa umaarufu kama Zombii. Wananchi walipigwa katika kituo cha Skuli ya Chunga (Shehia ya Chunga), katika kituo cha skuli ya Maandalizi eneo la Magomeni , Eneo la Kilimani katika Viwanja vya Maisara, Kuvamiwa kwa wafanyakazi wa kituo cha redio cha Coconut FM, Kituo kilichokuwepo katika Skuli ya Kisiwandui(Eneo la Kisiwandui), Eneo la Kipilipili (Chwaka katika Wilaya ya Kati, na Eneo la Shehia ya Ngamani (Makunduchi)

Malalamiko kuhusu watu kukataliwa kupewa vitambulisho vya kujiandikisha ukaazi na Masheha ili kupata kitambulisho cha Mzanzibari Makazi (*ZAN ID*) kutoka kwenye Mamlaka inayotoa vitambulisho hivyo pia yaliarifiwa. Hii ilisababisha baadhi ya watu kutoandikishwa kwenye daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutokuwa na *ZAN ID*, hivyo kukoseshwa haki yao ya kupiga kura. Hata hivyo pamoja na mapungufu yaliyoashiria ukiukwaji wa utaratibu wa

unadikishwaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, kulikuwa mafanikio katika zoezi hilo. Pamoja na changamoto hizo, kulikuwa na mafanikio ikiwa ni pamoja

i. Kuwepo kwa ulinzi wa askari Polisi uliokuwepo ndani ya vituo ulifuata majukumu ya Jeshi hilo katika kudumisha demokrasia wakati wa zoezi la uandikishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.

ii. Mwitikio wa wananchi ulioonekana katika vituo vya uandikishaji, uliashiria mafanikio ya jitihada za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, vyama vya siasa na vyombo vya habari katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujitokeza kutumia haki yao ya kujiandikisha.

iii. Maofisa uandikishaji walionesha kutekeleza majukumu yao kwa bidii na ustaarabu katika muda wote wa uandikishaji. Hapakubainika malalamiko yoyote dhidi yao kwenda kinyume na maadili au Sheria.

iv. Uandikishaji ulimalizika kwa amani

***4.2.1.2 Mapendekezo ya Tume***

Kutokana na masuala yaliyobainika katika uangalizi wa uandikishwaji na uboreshaji wa daftari la wapiga kura, Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo**:-**

a) Vituo vya uandikishwaji ambavyo si rafiki kwa watu wenye ulemavu, wazee na wagonjwa virekebeshwe na vile vilivyopo pembezoni mwa barabara visitumike katika uchaguzi mkuu ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea.

b) Maafisa uandikishaji waendelee kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu sheria ya uchaguzi ili watekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

c) Ofisi ya Msajili wa Vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi ihakikishe inaingiza mapema taarifa za usajili wa vitambulisho mara tu baada ya usajili kufanyika na kabla ya mhusika kukabidhiwa kitambulisho chake.

d) Vyombo vya ulinzi na Usalama zikiwemo Idara maalum za SMZ vihakikishe vinaweka ulinzi kwa mujibu wa sheria na kutumia askari wenye mfumo unaofahamika kwa wananchi ili kuondoa hofu kwa watu na uwezekano wa wahalifu kutumia mwanya huo.

e) Tume ya Uchaguzi Zanzibar iongeze jitihada katika kutoa elimu ya uraia kwa umma kuhusu masuala ya uchaguzi ili wananchi waweze kutambua, kutumia na kuzidai kikamilifu haki za kiraia na kisiasa zinapokiukwa.

f) Ofisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali na Idara ya Msajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwa pamoja ziandae mpango mkakati ambao utahakikisha kuwa Wazanzibari wote wanapatiwa vyeti vya kuzaliwa na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ili waweze kuitumia haki yao ya kupiga kura kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa kisheria.

g) Wizara ya Tawala za Mikoa ihakikishe Masheha na wananchi katika Shehia zao wanapewa elimu kuhusu uchaguzi na haki za kiraia na kisiasa ili kuepusha migogoro inayotokea mara kwa mara miongoni mwao wakati wa utekelezaji wa shughuli mbali mbali za serikali, hususan wakati wa zoezi la uchaguzi.

h) Vyama vya siasa vihakikishe vinapanga mipango na shughuli zao kwa kufuata sheria na taratibu, na kuelimisha wanachama na wafuasi wao kujiepusha na

vitendo ambavyo husababisha matukio ya kuhatarisha usalama na uvunjifu wa amani.

i) Serikali ihakikishe uhuru wa vyombo vya habari unalindwa na kuheshimiwa ipasavyo bila kuingiliwa na vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla.

j) Taasisi za Serikali na wadau mbalimbali wa uchaguzi zitekeleze wajibu wake kwa mujibu wa sheria za nchi.

### 4.2.2 Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu

Katika uchaguzi wa mwaka 2015, vyama vya siasa 14 vilisimamisha wagombea wa kiti cha Urais wa Zanzibar, na 22 viliwania viti katika Bunge, Baraza la Wawakilishi na Udiwani. Aidha, vyama vya CHADEMA, NCCR- Mageuzi, CUF na NLD vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) vilikubaliana kusimamisha mgombea mmoja kwenye uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wawakilishi na Masheha.

***4.2.2.1 Mikutano ya kampeni ya vyama vya siasa na siku ya uchaguzi mkuu***

Mikutano ya kampeni ya Uchaguzi Mkuu ilianza Septemba, 2015 na ilifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi na kuratibiwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Kampeni za vyama vya siasa zilifanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi Na. 11 ya mwaka 1984, Mwongozo wa vyama vya siasa wa Maadili ya Uchaguzi wa mwaka 2015 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya uangalizi wa Kampeni katika mikoa yote ya visiwa vya Unguja na Pemba.



***Wafuasi wa Chama cha Wananchi (CUF) wakiwa katika mkutano wa kampeni.***

Mikutano ya kampeni iliendeshwa kwa amani huku ikihudhuriwa na idadi kubwa ya watu na iliendeshwa kwa amani jambo ambalo lilidhihirisha kwamba wananchi walihamasika ipasavyo na kuelewa umuhimu wa kutumia haki yao ya kupiga kura. Vyama vya CCM na CUF vilionekana kuvutia umati mkubwa wa wananchi katika mikutano ya hadhara na kupitia vipindi vya moja kwa moja vya redio na televisheni. Kwa nyakati tofauti vyama hivyo vilikuwa vikiomba ridhaa ya kuongoza Zanzibar ili viweze

kuboresha huduma za Afya, Elimu, Maji, Kilimo na Uvuvi pamoja na kulipatia ufumbuzi tatizo linalowakabili vijana wengi la ajira.



***Wafuasi wa Chama cha Mapinduzi CCM wakiwa katika mkutano wa kampeni***

Siku ya uchaguzi, ZEC iliandaa vituo vya kupigia kura 1,582 vyenye wastani ya wapiga kura 350 kwa kila kituo. . Takriban vituo vyote vya kupigia kura vilikuwa katika majengo ya Serikali na vilikuwa na ulinzi na askari kwa kila kituo.Vituo vilifunguliwa kuanzia saa 1.00 asubuhi na kufungwa saa 12.00 jioni. Majina ya wapiga kura yakionesha namba za vituo walivyopaswa kupigia kura yalibandikwa hadharani kwenye maeneo mbalimbali ya kuta za majengo ya vituo hivyo.



***Wananchi wakiangalia majina yao nje ya vituo vya kupigia kura kabla ya kuingia ndani ya vyumba vya kupigia kura***

### *4.2.2.2 Masuala yaliyojitokeza katika kampeni na upigaji kura*

(i) Wananchi walijitokeza kwa wingi katika kupiga kura.

(ii) Kulikuwa na kasoro katika baadhi ya vituo kama vile baadhi ya mawakala wa vyama kukosa vitambulisho.
(iii) Baadhi ya vyama havikuweka mawakala katika baadhi ya vituo hasa vituo vya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.
(iv) Kulikuwa na matukio ya watu kupigwa katika baadhi ya vituo kisiwani Pemba, jambo ambalo ni kinyume cha sheria, kutokana na kuwepo kwa imani ya kuhofia kuibiwa kura;
(v) Baadhi ya watu kushindwa kupiga kura kwa kuwa hawakuandikishwa kwenye daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutokuwa na vitambulisho vya mZanzibar mkaazi.

***4.2.2.3 Kufutwa kwa matokeo na marudio ya Uchaguzi.***

Matokeo ya uchaguzi kwa upande wa wagombea wa Wawakilishi na Udiwani yalitolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo baada ya majumuisho ya kura katika vituo vya kupigia kura. Kwa upande wa matokeo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar majumuisho na uhakiki yalifanyika katika Hoteli ya Bwawani. Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi au Makamu wake walikuwa wakitangaza matokeo hayo kwa awamu kabla ya Mwenyekiti Jecha Salim Jecha kutangaza kupitia Shirika la Habari Zanzibar (ZBC) kufuta matokeo yote ya uchaguzi huo tarehe 28 Oktoba, 2015 ikiwa ni siku ya tatu baada ya upigaji kura kumalizika akinukuu kasoro ambazo alisema zilibatilisha uchaguzi wa kura ya Rais wa Zanzibar, na ilisababisha uchaguzi kurudiwa.
Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, matokeo yalifutwa kutokana na "ukiukwaji na uvunjaji wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi. Mapungufu yaliyojitokeza ni pamoja na vitisho kwa wapiga kura hasa kwenye maeneo ambako ni ngome za vyama, kupoka mamlaka ya Tume juu ya utangazaji wa matokeo ya kura ya urais na idadi ya wapiga kura katika baadhi ya vituo kuzidi ile ya waliojiandikisha.



***Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar Bwana Jecha S. Jecha akitangaza matokeo ya awali katika ukumbi wa mikutano wa Bwawani kabla ya kutangaza kuufuta uchaguzi wa Zanzibar.***

*4.2.2.4 Mapendekezo ya kuboresha demokrasia Zanzibar*

I. Serikali ifanyie mapitio Sheria ya Uchaguzi Na. 11 ya mwaka 1984 na Sheria ya Mzanzibari Mkaazi na Kanuni zake ili kuondoa vikwazo vinavyosababisha wananchi kukosa fursa ya kutumia haki yao ya kupiga kura.

II. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 zifanyiwe marekebisho ili ziruhusu mgombea binafsi kwenye chaguzi.

III. Vyama vya siasa vijenge na kudumisha misingi ya demokrasia wakati wote ikiwemo kuheshimu matokeo ya uchaguzi.

IV. Viongozi na wafuasi wa vyama kupuka lugha zinazoweza kuchochea uvunjifu wa amani na kudumaza demokrasia.

V. Muundo wa ZEC ubadilishwe kwa kuzingatia sifa ya uweledi na uadilifu badala ya kuundwa na wawakilishi wa vyama vya siasa.

VI. Katiba ifanyiwe marekebisho kuruhusu matokeo ya Urais kuhojiwa mahakamani

## 4.3 Ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar

Tume Zanzibar ilifanya ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo tisa ambavyo vitanovikiwa Unguja na vinne kwa upande wa Pemba. Vyuo hivyo ni Kiinua Miguu, Langoni, Kinumoshi, Hanyegwa Mchana, na Ubago kwa upande wa Unguja na Wete, Tungamaa, Kangagani na Kengeja kwa upande wa Pemba. Madhumuni ya ukaguzi huo ilikuwa ni kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika vyuo hivyo.



***Kamishna Mkazi wa Tume Zanzibar akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa na Askari waChuo cha Mafunzo***

### 4.3.1 Hali ya Haki Wafungwa na mahabusu

Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa hali ya haki za watu waliozuiliwa haziridhishi, na pia mazingira ya vyuo hayakidhi viwango kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na kikanda ya haki za binadamu pamoja na sheria za nchi. Mapungufu yafuatayo yalijitokeza wakati wa ukaguzi**:-**

1) Baadhi ya majengo ya Vyuo vya mafunzo vilivyokaguliwa ni machakavu na hayana huduma muhimu kama za vyoo
2) Mitondoo bado inaendelea kutumika katika baadhi ya vyuo.
3) Vyuo vilivyokaguliwa havina huduma ya usafiri.
4) Vyuo vichache vilikuwa na huduma ya afya na vingine havikuwa na daktari wala dawa.
5) Baadhi ya nyumba za askari wa vyuo vya mafunzo ni mbovu na chakavu na hazikidhi kuishi binadamu.
6) Hakuna mabweni kwa ajili ya wafungwa na mahabusu watoto pamoja na kwamba kulikuwa na watoto wawili katika chuo kimoja wakati wa ukaguzi.
7) Maji safi, mawasialiano na burudani vyote vinapatikana katika vyuo vilivyokaguliwa.
8) Kukosekana kwa vitendea kazi vya wanafunzi kwenye baadhi ya vyuo vilivyokaguliwa mfano kinga (mask) wakati wa kumwagilia dawa za wadudu katika mashamba pamoja na viatu madhubuti ili kuepusha majeraha kulingana na mazingira ya kazi. Pia vitendea kazi kwa askari ili kuboresha utendaji wa kazi. Madai ya malipo ya posho ya uhamisho na nauli ya likizo kwa baadhi ya askari wa vyuo vya mafunzo.
9) Kutotekelezwa kwa ombi la Askari kurejeshwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na mfuko wa Bima ya Afya.



*Jiwe la msingi la ujenzi wa mabweni ya mesi ya chuo cha mafunzo lililowekwa 1913*

Pamoja na mapungufu na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi, Tume ilibaini kuwa hapakuwa na msongamano wa mahabusu au wanafunzi katika vyuo vilivyokaguliwa.

***4.3.1.1 Malalamiko dhidi ya Askari Polisi***

(a) Askari polisi wanachelewesha kukamilisha upelelezi.

(b) Malalamiko ya polisi kuwadhalilisha na kuwapiga watuhumiwa kwa lengo la kuwalazimisha kukiri makosa.

(c) Malalamiko ya askari polisi kuwabambikiza watu kesi,

(d) Askari polisi walilalamikiwa kuchukua vitu wanavyokutwa navyo watuhumiwa wakati wanapokamatwa bila kurudishiwa wenyewe.

***4.3.1. 2 Mahakama***

i) Ucheleweshaji wa hukumu pamoja na nakala za hukumu kwa wafungwa hali inayosababisha kukosa haki ya kukata rufaa kwa wakati.

ii) Mahakama zinachelewa kusikiliza rufaa.

***4.3.1.3 Uendeshaji wa vyuo vya mafunzo na changamoto zake***

Ilibainika kuwa vyuo vya Mafunzo vinakabiliwa na changamoto za ukosefu wa rasilimali hivyo kushindwa kutekeleza haki za wanafunzi na watumishi ipasavyo. Ilielezwa kuwa mahitaji ya fedha kwa ajili ya huduma za Idara ya vyuo vya mafunzo ni tofauti na Idara zingine zilizomo katika Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hii ni kwa sababu Idara ya vyuo vya mafunzo huhitaji fedha kwa ajili ya huduma za uendeshaji wa Idara na pia kwa ajili ya huduma za wanafunzi na mahabusu. Ilielezwa kuwa vyuo vya mafunzo kama Idara nyingine za Serikali vinakabiliwa na tatizo la upatikanaji mdogo wa fedha za uendeshaji kutoka Serikalini.

Changamoto nyingine ambayo inaikabili Idara ya vyuo vya mafunzo ni kutokuwepo utaratibu wa kupatiwa fedha kwa kila chuo moja kwa moja kwa ajili ya huduma za chuo husika, badala yake kila chuo hupata bidhaa za huduma zinazohitajika kutoka Makao Makuu ya vyuo hivyo. Katika kutatua changamoto hiyo na kupunguza utegemezi kutoka Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo baadhi ya Uongozi wa vyuo umekuwa ukibuni miradi mbalimbali ya maendeleo katika vyuo kulingana na mazingira yaliyozunguka vyuo husika.

***4.3.1.3 Malalamiko ya wanafunzi na mahabusu***

Tume ilipata fursa ya kufanya vikao na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ili kusikiliza malalamiko na mapendekezo yao kuhusu hali ilivyo katika sehemu walimozuiliwa. Wanafunzi walikuwa na malalamiko yafuatayo:-

i) Wanafunzi na mahabusu walilalamika kupekuliwa wakiwa uchi mbele ya askari wa jinsia tofauti wakati wanapoingizwa chuoni.

ii) Kutokuwepo usafiri wa kuwapeleka mahakamani siku za kesi zao au rufaa.

iii) Ucheleweshaji wa kesi kutokana na upelelezi kutokamilika mapema.

iv) Mahabusu walilalamikia kutengenezewa mazingira ya kubambikiwa kesi wakati wakiwa rumande baada ya kuonekana dalili za kushinda kesi walizotuhumiwa.

v) Watuhumiwa kutorudishiwa mali zao wakati wanapotoka rumande.

vi) Mateso ikiwemo kupigwa, kutundikwa au kuingizwa chupa sehemu za siri ili kulazimishwa kukiri kosa.

vii) Ucheleweshaji wa kusikilizwa na kutolewa hukumu za kesi.

viii) Ucheleweshaji wa mienendo ya kesi na nakala za hukumu .

ix) Mahakama kuchelewa kusikiliza rufaa za wanafunzi hadi kufikia kumaliza vifungo walivyokatia rufaa.

x) Upungufu wa dawa na kutokuwepo daktari mkaazi katika baadhi ya vyuo.

#### *4.3.1.4 Mapendekezo ya mahabusu na wanafunzi*

(a) Vyuo vya mafunzo vipatiwe dawa za kutosha na Daktari mkaazi ili kuondoa tatizo la ukosefu wa dawa na kushughulikia dharura za wanafunzi.
(b) Wanafunzi wanaopelekwa kufanya kazi za kilimo wapatiwe vitendea kazi ikiwemo kinga (mask) wakati wa kunyunyizia dawa mashambani na viatu vinavyolingana na mazingira ya kazi.
(c) Upelelezi wa kesi uharakishwe ili mahabusu wasikae muda mrefu rumande na kupunguza gharama za kuwahudumia.
(d) Serikali itunge sheria zitakazoweka muda maalum wa kusikiliza rufaa za wanafunzi
(e) Wanafunzi na mahabusu waliomba wapatiwe sabuni zenye dawa ya kinga (medicated soap) ili kusaidia kuondoa maradhi ya ngozi.
(f) Vyuo vya mafunzo vipatiwe magodoro ya inchi nne kwani yanayotumika ni membamba ya inchi 1 hadi 2.
(g) Wanafunzi wanaotumikia adhabu zao katika vyuo vinavyojishughulisha na kilimo waliomba kipimo cha chakula kiongezwe ili kiweze kuendana na aina ya kazi wanazofanya.
(h) Wanafunzi na Mahabusu waliomba kuwe na utaratibu wa kutembelewa na viongozi wa dini.

#### *4.3.1.5 Changamoto zinazowakabili watumishi*

Ukaguzi wa vyuo vya mafunzo pamoja na majadiliano na askari ulibaini changamoto mbali mbali zinazowakabili watumishi wa taasisi hizi. Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

i) Tatizo la makazi na ufinyu wa posho ya makazi. Nyumba wanazoishi ni finyu (kwa maana ya chumba kimoja na sebule kwa familia yenye mke/ mume na watoto wenye umri wa shule ya msingi na sekondari) na zimechakaa. Miundombinu yake ikiwemo maji, vyoo na umeme haviko katika hali nzuri.



*Mojawapo ya nyumba zinazotumiwa na askari na familia zao kwa makaazi katika kambi za idara ya chuo cha mafunzo*

ii) Upatikanaji wa sare ni tatizo kwani hazikidhi mzunguko wa mwaka mzima. Pia sare zinazotolewa ni za daraja la chini na hazipatikani zote (sare za viatu mara nyingi askari hujinunulia wenyewe).

iii) Mazingira ya kazi ambapo Askari wanafanyakazi Pemba wakati wameziacha familia zao Unguja na kulazimika kugawa mishahara yao mara mbili. Aidha, hakuna muda maalumu wa uhamisho matokeo yake hukaa Pemba miaka mingi bila kufikiriwa kurudishwa Unguja.

iv) Vile vile Askari anapopata tatizo ruhusa ya kusafiri kwenda Unguja kutatua shida yake ni sharti itoke kwa Kamanda wa Vyuo vya Mafunzo Makao Makuu Unguja kwa kuwa Kamanda Mkuu Pemba hana mamlaka hayo.

v) Changamoto hizi husababisha baadhi ya ndoa za Askari kuvunjika pamoja na Vyuo vya Mafunzo Pemba kukosa maendeleo kwa sababu wafanyakazi wanakosa ari yakufanya kazi.

vi) Mazingira ya kazi sio mazuri kutokana na uhaba wa vitendea kazi. Ofisi za Makamanda ni mbovu, chakavu, hazina samani na vitendea kazi vya kutosha. Makao Makuu ya Vyuo vya Mafunzo zina kompyuta chache na Chuo cha Wete kina kompyuta moja na mashine ya kunakili (*Photocopy machine*).

vii) Mishahara wanayolipwa ni midogo ambayo haikidhi kujikimu kimaisha, inalipwa bila nyongeza ya kila mwaka (*increment*) hivyo kutokuwa na tofauti ya mshahara kati ya waajiriwa waliotangulia kazini na wapya waliopo katika cheo kinacholingana.

viii) Kutokuwepo kwa utaratibu au mpango wa kujiunga na mafunzo kwa askari asiye au aliye na cheo, na kama upo haufuatwi kwani baadhi hufikia hadi miaka kumi na mbili bila kupelekwa mafunzoni. Hali hii husababisha baadhi ya walioajiriwa kwa muda mrefu kulingana au kupitwa mshahara na walioajiriwa karibuni ambao huchaguliwa kujiunga na mafunzo katika muda mfupi baada ya kuajiriwa au kupandishwa cheo.

.

ix) Likizo kwa wafanyakazi hupatikana kila inapostahiki na kama kuna kazi maalumu husogezwa mbele. Changamoto ipo katika ulipwaji wa nauli ya likizo ambapo baadhi ya askari wamelipwa mara moja ndani ya miaka kumi na tano.

x) Mafunzo ya muda au semina zinazohusiana na haki za binadamu ambazo hutolewa na UNICEF au taasisi nyingine haziwafikii watendaji ambao ndio hasa walinzi au waalimu wa wanafunzi badala yake zimekuwa zikihudhuriwa na viongozi wa Makao Makuu ya Chuo.

xi) Uhamisho ni suala lililochukua nafasi kubwa katika malalamiko ya askari wa Vyuo vya Mafunzo hususani walioko Pemba. Mambo kadhaa yamelalamikiwa kutokana na

utaratibu wa uhamisho wa Idara ya Chuo cha Mafunzo kutokuwa wa haki ikilinganishwa na Idara Maalumu za SMZ nyingine. Ilielezwa kuwa uhamisho unachukuliwa kama ni adhabu kwa askari, kwani baadhi hupewa uhamisho bila kujali ndoa, kwa mfano mwanamke atahamishiwa Pemba wakati mumewe ni raia au mtumishi wa taasisi nyingine.

xii) Idara ya Chuo cha Mafunzo haitoi fidia wala msaada wa tiba kwa Askari anayeumia kazini.

xiii) Matukio ya Askari kupigwa, kutemewa mate, kumwagiwa vinyesi au mikojo na wakati mwingine kutorokwa na wanafunzi au mahabausu wakati wanawasimamia.

### 4.3.2 Maoni na mapendekezo

***4.3.2.1 Maoni na mapendekezo ya askari***

i) Uandaliwe utaratibu wakulipwa posho maalumu kutokana na mazingira magumu ya kazi zao.

ii) Upatikanaji wa huduma za Afya katika Vyuo vya Mafunzo hauridhishi. Huduma zinazopatikana ni kwa ajili ya wanafunzi pekee. Ilipendekezwa itolewe kwa Askari na Wanafunzi wa Vyuo vyote.

iii) Uandaliwe utaratibu wa kupatiwa Bima ya Afya na Mafao ZSSF kwa Askari wa Vyuo vya Mafunzo.

iv) Kutokana na majukumu waliyonayo Askari walipendekeza wapewe semina za mara kwa mara za kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(vi) Baadhi ya Askari waliomba wafahamishwe kuhusu muda unaotakiwa kukaa katika kituo cha kazi baada ya kuhamishwa.

(vi) Baadhi ya Askari walipendekeza kuwa washirikishwe katika maamuzi ya kukata mishahara yao kwa ajili ya shuguli mbalimbali ikiwemo kununulia vifaa vya michezo.

***4.3.2 2 Mapendekezo ya Tume kwa hatua za muda mfupi***

(i) Idara ya vyuo vya mafunzo itafute mkandarasi atengeneze vyoo vya ndani ili wanafunzi waondokane na matumizi ya mitondoo.

(ii) Idara ya vyuo vya mafunzo ipeleke Daktari na dawa katika kila chuo cha mafunzo ili kuepusha usumbufu wakati huduma hiyo inapohitajika.

(iii) Uongozi wa Idara ya vyuo vya mafunzo uandae utaratibu wa kuwalipa posho ya mazingira magumu askari wake.

(iv) Idara ya vyuo vya mafunzo ihakikishe inazingatia haki katika taratibu za uhamisho kwa askari wanaohamishwa kwenda Pemba/Unguja ikiwemo muda maalum wa kuwepo uhamishoni.

v) Kamanda wa vyuo vya mafunzo Pemba apewe mamlaka ya kutoa ruhusa kwa askari aliyepo chini ya uongozi wake kwa wakati atapoona upo umuhimu wa kufanya hivyo.

(vi) Uongozi wa vyuo vya mafunzo ufuate utaratibu wa kulipwa fidia mfanyakazi anayeumia akiwa kazini.

(vii) Serikali na Idara ya Vyuo vya Mafunzo waangalie uwezekano wa kuboresha vitendea kazi na maslahi ya askari ili kuongeza ufanisi katika kazi.

(viii) Polisi wasicheleweshe Upelelezi wa kesi za watuhumiwa,

(ix) Polisi waache tabia ya kubambikiza kesi, kuwadhalilisha na kuwapiga watuhumiwa pamoja na kutowarudishia watuhumiwa vitu wanavyovizuia wakati wanapowakamata na kuwaweka rumande.

(ix) Uongozi wa Jeshi la Polisi upeleleze tuhuma hizo na kuchukua hatua kali dhidi ya askari atakayetuhumiwa kubambikiza kesi, kudhalilisha, kupiga, na kutorudisha vitu vya mtuhumiwa.

(x) Mahakama ziharakishe kutoa hukumu za kesi, nakala za hukumu pamoja na kusikiliza rufaa katika wakati unaofaa.

***4.3.2 3 Mapendekezo ya Tume kwa hatua za muda mrefu:***

a) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iboreshe maslahi na mazingira ya kazi, kwa askari wa Vyuo vya Mafunzo b) Baadhi ya majengo ya vyuo vya mafunzo yaliyojengwa tokea wakati wa ukoloni hayakujengwa kwa madhumuni ya kuwa vyuo vya mafunzo. Majengo hayo yote yamechakaa na/au hayafai tena, serikali kupitia wizara husika iangalie uwezekano wa kuyakarabati na kujenga majengo mengine.

c) Serikali kupitia Wizara husika iwajengee askari nyumba zinazofaa kuishi kambini zikiwemo za wenye familia, pia izifanyie ukarabati nyumba zilizopo ambazo ni mbovu na hazifai kuishi watu, ili askari wasipange uraiani na pia kupata utulivu utakaowawezesha kufanya kazi na kuishi katika mazingira yanayofaa.

d) Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia ziara za masomo askari wanaolinda wanafunzi angalau katika nchi za jirani kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya kazi zao zinazofanywa na nchi nyingine.

## 4.4 Tathmini ya hali ya haki za binadamu na utawala bora baada ya Uchaguzi –wa marejeo

Tume ilifanya ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora baada ya Uchaguzi mkuu wa marejeo uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 kutokana na kuwepo kwa viashiria vya uvunjifu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Uchunguzi uliofanywa na Tume ulibaini kuwepo kwa matukio ya uharibifu wa mali, mfarakano wa familia, migomo, hujuma, ubaguzi wa kiitikadi na kutoshirikiana katika shughuli za kijamii na huduma za kijamii. Matukio ya uhalifu na uharibifu wa mali, kama vile kukata mazao, na kuchoma moto nyumba viliripotiwa kutokea katika shehia za Tumbe, Kiungoni, Maziwangombe, Mtambwe na Kojani.

Vitendo vya kukata na kuharibu mali, ni kinyume na haki za binadamu kwani kila mtu ana haki ya kumiliki mali kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, na Kifungu cha 17 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Aidha kumekuwepo taarifa za matukio kama vile migomo[73] katika takriban maeneo mengi ya Mikoa ya Pemba na baadhi ya maeneo katika kisiwa cha Unguja, zenye kuashiria vitendo vya kubaguana kwa maana ya kutoshirikiana katika shughuli za kijamii na huduma za kijamii. Kwa mfano baadhi ya watu wananyimwa usafiri katika magari, kususiwa harusi, maziko na nyumba za ibada.

Matukio ya watu kubaguliwa kwa itikadi za kisiasa pia yaliarifiwa kujitokeza katika huduma za usafiri wa nchi kavu na majini katika maeneo ya Kojani, Fundo, Kisiwapanza na Makoongwe. Ilielezwa kuwa baadhi ya madereva wa magari ya abiria na vyombo vya baharini vikiwemo mashua na madau walilazimishwa kutowapakia wafuasi wa CCM. Pia suala la ubaguzi lilijitokeza katika huduma za kuuza na kununua bidhaa ambako wafuasi wa CCM wamekuwa hawauziwi bidhaa kutoka maduka yanayomilikiwa na wafuasi wa CUF. Matukio hayo yalijitokeza katika maeneo ya Mtambwe, Kojani, Kiungoni, Fundo, Mchangamdogo na Pembeni. Kuwanyima watu huduma ya aina yoyote katika jamii ni kinyume na misingi ya haki za binadamu, hasa haki ya kutobaguliwa kama ilivyoelezwa katika ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 11 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Pia ilielezwa kuwa tofauti za itikadi za kisiasa zinasababisha ndoa kuvunjika kutokana na wanawake kuadhibiwa kwa kupewa talaka kutokana na kutotii amri ya waume zao za kuwazuia kushiriki uchaguzi wa marejeo. Hali hii ni kinyume na kifungu cha 21(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambacho kinaeleza kuwa ***"kila Mzanzibari anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa hiari"***. Haki hii haitakiwi kuingiliwa na mtu yeyote, kwani ni haki inayotambua uhuru na utu wa kila mwanadamu kuamua yeye mwenyewe kushiriki au kutoshiriki katika shughuli za kisiasa, awe mwanamume au mwanamke.

Tume pia inapenda kutoa ushauri kuhusu yanayoendelea kisiwani Pemba na Zanzibar kwa ujumla kuwa ili hali irudi kama ilivyokuwa kabla ya chaguzi zilizopita, panahitajika hatua za makusudi zitakazo leta maelewano katika jamii. Tume inashauri yafuatayo:-

(i) Hatua za makusudi na haraka zifanyike kwa Viongozi wa Kitaifa na wa vyama vyote vya siasa vikiwemo CUF na CCM wakae pamoja kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa suluhisho la kudumu Katika kulinda amani

(ii) Taasisi zinazosimamia ulinzi na usalama hususan vyombo vya dola na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zizingatie misingi ya utawala bora, haki za binadamu na utawala wa sheria wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao ili kuepuka madhara yasiyotarajiwa katika jamii.

(iii) Wananchi wote wanatakiwa kutii sheria za nchi, na kutojiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa amani na usalama.

[73] Maeneo ya Mtambwe, Kojani, Kiungoni, Fundo, Mchangamdogo na Pembeni

## 4.5 Utoaji wa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Katika kipindi hiki cha 2015/2016 Tume ilitekeleza jukumu lake la kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kushirikiana na wizara na idara ya SMZ, shirika la habari la Zanzibar (ZBC), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) na Club ya Waandishi wa Habari Zanzibar. Kazi hii ilifanyika kwa njia ya vyombo vya habari, kongamano, semina na kutoa mada mbali mbali kuhusu haki za binadamu na utawala bora, wajibu wa jamii, Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013-2017, haki za watoto, mahabusu na wafungwa.

Tume pia ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wake, na watumishi wa Wizara na Idara za Serikali ili kuongeza ufahamu wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, usuluhishi wa migogoro (Conflict Management), Usawa wa Kijinsia katika utoaji haki (*''Gender Equality in the Administration of Justice'')*, uangalizi wa mchakato wa uchaguzi, na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu

Aidha, Tume ilishirikiana na taasisi na wadau mbalimbali katika masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa lengo la kuendeleza utulivu na amani. Ushirikishwaji huo ulikuwa katika uzinduzi wa taarifa mbalimbali, kutathmini kampeni ya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto Zanzibar, mkutano wa Wadau kuhusu utafiti wa sheria zinazokinzana na Utawala Bora, na mkutano wa Kikundi Kazi cha kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mageuzi ya Mfumo wa Sheria ya Mtoto.

Kwa ujumla, utoaji wa elimu ya haki za bindamu na misingi ya utawala bora ulikabiliwa na changamoto kama vile uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora, uwepo wa Tume na shughuli zake, na wajibu wa taasisi nyingine katika kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu Zanzibar

# SURA YA TANO

# 5.0 CHANGAMOTO, MAPENDEKEZO NA MATARAJIO

## 5.1 Changamoto

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume ilipata na changamoto mbali mbali ambazo zimepunguza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Tume.

### 5.1.1 Ufinyu wa bajeti na changamoto zake

Tume ilipewa bajeti ndogo kinyume na mahitaji yake sambamba na matakwa ya kanuni za Paris (Paris Principles) zinazozitaka serikali husika kutenga bajeti za kutosha kwa taasisi za kitaifa za haki za binadamu. Hali hii ilisababisha Tume kushindwakutekeleza majukumu yake ya kufikia wananchi wenye mahitaji kwa wakati. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Tume ilitengewa kiasi cha Tsh5, 005,949,000.00 ambazo ni Shs 2,226,368,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Juni 2016, Tume ilipokea Shs 1,241,701,100.00 ambacho ni asilimia 55 iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi mengineyo(OC).

Kwa matumizi ya Fedha za Maendeleo, Tume ilitengewa Tshs. 382,122,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa UNDP Support Program. Hata hivyo kiasi kilichopatikana na kutumika ni Tsh 324,212,100.00 ambacho ni asilimia 84 ya kiasi kilichotengwa. Kutokupata kiasi cha fedha zilizotengwa na kuchelewa kutolewa kwa fedha za utekelezaji wa majukumu ya Tume kinyume na mpangokazi uliopo wa Tume (Commission's Action Plan) kuliathiri kutekeleza majukumuyote ya Tume.
Kwa upande wa makusanyo, kwa kuwa kazi kubwa ya Tume ni kutoa huduma hasa kwa wahitaji, haina vyanzo vikubwa vya mapato kwa Serikali. Kwa mwaka huu wa fedha Tume ilipanga kukusanya kiasi cha Tshs 5,131,000/= ikiwa ni mapato yanayotokana na uuzaji wa vitabu vya zabuni za Tume. Hata hivyo, Tume haikufanikiwa kukusanya kiasi chochote cha maduhuli kutokana na kutokuwepo kwa uuzaji wa vitabu vya tenda .

1. Tume imeshindwa kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika mikutano muhimu ya kimataifa na kikanda ambayo Tume ni mwanachama kama vile mikutano ya *International Coordinating Committee (ICC) ambayo sasa hujulikana kama General Assemby of National Human Rights Institutions (GANHRI), Commonwealth, Ombudsman ( International Coordinating Commttee)).*

2. Tume inashindwa kutekeleza majukumu yake ya kuhamasisha, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu nchini ipasavyo kutokana na upungufu wa vit kulinda na kukuza haki za binadamuendea kazi ikiwa ni pamoja na kompyuta, samani za ofisi na magari. Ukosefu wa rasilimali na vitendea kazi unaifanya Tume kushindwa kutekeleza jukumu lake la kwa viwango vinavyotakiwa hali inayowafanya wananchi kukata tamaa na kuilaumu kutoshughulikia matatizo yao.

3. Kutokuwepo kwa ofisi za kanda za Tume katika mikoa mbalimbali hali inayosababisha huduma za Tume kuwa mbali na wananchi, ikizingatiwa kuwa Tume ina ofisi zilizopo Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Lindi na tawi jipya la Pemba tu.

### 5.1.2 Ushirikiano kutoka kwa baadhi ya taasisi za umma

Changamoto nyingine ni ushirikiano mdogo kutoka kwa baadhi ya taasisi za umma hususani katika kutekeleza maamuzi na mapendekezo ya Tume, jambo linalochelewesha upatikanaji wa haki kwa waathirika kwa wakati. Kwa upande mwingine ushirikiano mdogo husababisha mchakato wa uchunguzi wa malalamiko kuchukua muda mrefu isivyostahili.

### 5.1.3 Upungufu wa Watumishi katika ofisi za Tume

Tume imekumbwa na upungufu wa watumishi katika ofisi zake za matawi. Kwa mafano ofisi za Lindi na Pemba ambako kuna watumishi wawili tu (kila moja )kutokana na kukosekana fedha kwa ajili ya kulipia stahili za uhamisho za watumishi wanaoweza kuhamishiwa katika ofisi hizo.

### 5.1.4 Changamoto zinazoikumba ofisi mpya ya Pemba

Katika mwaka 2014/2015 Tume ilifungua ofisi ya Pemba pamoja na umuhimu wake kwa mikoa ya visiwa vya Pemba, uendeshaji wa ofisi hiyo unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa rasilimali watu, vitendea kazi na ofisi kutofahamika kwa viongozi wa serikali na wananchi kwa ujumla kisiwani Pemba. Watumishi waliopo kwa sasa ni wawili akiwemo Afisa Uchunguzi Mkuu ambaye pia ni Afisa Mfawidhi na Mlinzi mmoja.

## 5.2 Mikakati ya kukabili changamoto zilizojitokeza

1. Tume inaendelea kuiomba Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba na Kisheria.
2. Tume imekuwa ikitumia njia ya usuluhishi na upatanishi kama mbinu mbadala na ya gharama nafuu za kuharakisha utatuzi wa baadhi ya migogoro kwa wakati.
3. Tume imekuwa ikishirikiana na wahisani mbalimbali ili iweze kutekeleza baadhi ya majukumu yake kwa ufanisi.
4. Tume inawatambua "*Focal Persons*" kutoka Wizara na Idara mbalimbali za Serikali kwa kurahisisha mawasiliano kati ya Tume na Taasisi hizo pamoja na kupeleka huduma karibu na wananchi. Kuendelea kuufanyia maboresho Mfumo wa Kielektroniki wa kushughulikia malalamiko (Complaints Management System-CMS) kwa lengo la kuharakisha ushughulikiaji wa malalamiko.

## *5.3* Mapendekezo ya kuboresha haki za binadamu na utawala bora nchini

(i) Tume ipate fedha za kutosha kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi na kuwajengea uwezo watumishi wa umma kuhusu utawala bora na manufaa yake kwa jamii na taifa kwa ujumla.

(ii) Serikali na wananchi kuongeza juhudi kuhakikisha kuwa mianya ya rushwa inadhibitiwa katika sekta mbalimbali nchini, kwani rushwa ni adui wa haki.

(iii) Kasi ya kushughulikia watuhumiwa wa makosa ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina iongezwe ili kuhakikisha kuwa haki ya kuishi ya wazee hasa wanawake na watu wenye ualbino inalindwa

(iv) Taasisi za umma na za binafsi zinazohusika na utoaji wa huduma kwa wananchi zitekeleze majukumu yao kuendana na mikataba ya huduma kwa wateja waliyojiwekea.

(v) Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ili kulinda haki na ustawi wa mtoto wa kike Tanzania.

(vi) Kupanua mfuko wa fidia ili kuharakisha malipo mbali mbali ya fidia hasa zinazohusu utwaaji wa ardhi inayomilikiwa na wananchii yanafanyika kwa wakati.

(vii) Wizara zinazohusika na sheria, mambo ya ndani , afya na ustawi wa jamii kupitia upya mfumo wa tiba za jadi ili kuzuia wanaofanya kazi kinyume na maadili ya kazi zao.

(viii) Wizara zinazohusika na ustawi wa jamii, mambo ya Ndani na Sheria kuimarisha haki za watoto walio katika mkinzano na sheria

(ix) Wizara ya Habari ihamasishe vyombo vya habari, hasusan redio jamii *(community radio)* katika kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na wajibu wa jamii hususani katika kutambua na kuheshimu haki za wazee, watu wenye ulemavu, wanawake na watoto .

(x) Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau lifanye uchunguzi na upelelezi wa kina kubaini mtandao wa wanaohusika na mauaji ya watu wenye ualbino wakiwemo waganga wa jadi, pamoja na watu wanaotenda ukatili dhid ya watu wenye ualbino na watumiaji wakuu wa viungo hivyo.

(xi) Mahakama ziharakishe usikilizaji wa mashauri ya mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino na kutoa hukumu kwa wakati ili kulinda haki za kundi hilo.

(xii) Wizara ya Ardhi ishirikiane na Halmashauri za wilaya kuhakikisha wilaya zote zinakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi inayotekelezeka

## 5.3 Matarajio ya utekelezaji wa majukumu yaTume kwa mwaka 2016/2017

Katika mwaka wa fedha **2016/2017** Tume inatarajia kufanyia kazi maeneo yaliyoorodheshwa hapa chini endapo itapata kiasi cha kutosha kulingana na makadirio ya mahitaji yake. Maeneo ambayo Tume imeyapa kipaumbele katika bajeti ni kama ifuatavyo:-

1. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu, wajibu kwa jamii na misingi ya utawala bora kwa wadau mbalimbali wa Tume. Tume inapanga kuimarisha utoaji wa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa kuandaa, kuchapisha na kugawa machapisho mbalimbali kwa umma, kuandaa na kurusha vipindi vya redio na runinga na kujenga uwezo wa vyombo vya habari katika utoaji wa taarifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora.
2. Kukamilisha uchunguzi wa mashauri ambayo hayakukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016 na kufanya uchunguzi wa malalamiko yatakayopokelewa katika mwaka wa fedha wa 2016/2017. Kwa kuongeza kasi ya ukusanyaji taarifa zitakazosaidia

kukamilisha na kutumia mbinu za usuluhishi kati ya walalamikiwa na walalamikaji na Kutoa ushauri wa kisheria na mafunzo kwa walalamikaji, walalamikiwa na watumishi ili kupata mbinu za kisasa za uchunguzi, na usuluhishi.

3. Kufanya utafiti kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora zinazolenga kuboresha maisha ya wananchi walio kwenye mazingira magumu katika jamii.
4. Kuboresha mfumo wa kompyuta katika kushughulikia malalamiko (Case Management System), kuboresha mfumo unaopokea malalamiko kwa njia ya ujumbe wa simu, mfumo huu pia utawawezesha walalamikaji kufuatilia hatua za malalamiko kwa kupitia ujumbe wa simu ya mkononi.
5. Kuimarisha ofisi za Tume, ofisi za makao makuu, ofisi ya Zanzibar na ofisi za matawi
6. Kuhamishia watumishi katika ofisi za matawi, na kuimarisha vitendea kazi katika ofisi hizo kwa lengo la kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.
7. Kupitia miswada na Sheria iwapo inakidhi vigezo vya kimataifa na vya kikanda vya kutetea na kulinda haki za binadamu na utawala bora ili kuweza kuishauri serikali.
8. Kuendelea kukagua sehemu wanamoshikiliwa watu kama vile (Magereza, Vituo vya Polisi, vituo vya watoto na sehemu nyinginezo kushirikiana na mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora inazingatiwa.
9. Kuandaa mpango mkakati wa kuitangaza Tume na kazi zake kwa wananchi, viongozi wa umma na sekta binafsi.

# Viambatanisho; A

**Mikoa na Wilaya zilizopata elimu na Mafunzo juu ya a Mpango kazi wa Kitaifa**

| S/n | Mkoa | Halmashauri/Manispaa |
|---|---|---|
| 1 | Arusha | Halimashauri wilaya ya Meru |
| | | Halmshauri ya Mji ya Arusha |
| | | Halmashauri wilaya ya Karatu |
| | | Halmashauri wilaya ya Longido |
| | | Halmashauri wilaya ya Monduli |
| | | Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro |
| 2 | Dar Es Salaam | Manispaa ya Ilala |
| | | Manispaa ya Kinondoni |
| | | Manispaa ya Temeke |
| | | Manispaa ya Kigamboni |
| | | Manispaa ya Ubungo |
| | | |
| 3 | Dodoma | Halmashauri ya wilaya ya Bahi |
| | | Halmashauri ya wilaya ya Chamwino |
| | | Halmashauri ya wilaya ya Chemba |
| | | Manispaa ya Dodoma |
| | | Halmashauri wilaya ya Kondoa |
| | | Halmashauri wilaya ya Kongwa |
| | | Halmashauri wilaya ya Mpwapwa |
| 4 | Manyara | Halmashauri ya Mji Babati |
| | | Halmashauri wilaya ya Babati |
| | | Halmashari wilaya ya Hanang |
| | | Halmashauri wilaya ya Kiteto |
| | | Halmashauri wilaya ya Mbulu |
| | | Halmashauri wilaya ya Simanjiro |
| 5 | Kusini Unguja | Halmashauri wilaya ya Kati |
| | | Halmashauri wilaya ya Kusini |
| 6 | Lindi | Halmashauri wilaya ya Kilwa |
| | | Halmashauri wilaya ya Lindi |
| | | Manispaa ya Lindi |
| | | Halmashauri wilaya ya Liwale |
| | | Halmashauri wilaya ya Nachingwea l |
| | | Halmashauri wilaya ya Ruangwa |
| | | |
| 7 | Kilimanjaro | Halmashauri wilaya ya Hai |
| | | Halmashauri wilaya ya Moshi |
| | | Manispaa ya Moshi |
| | | Halmashauri wilaya ya Mwanga |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri wilaya ya Rombo |
| | | Halmashauri wilaya ya Same |
| | | Halmashauri wilaya ya Siha |
| 8 | Kigoma | Halmashauri wilaya ya Buhigwe |
| | | Halmashauri wilaya ya Kakonko |
| | | Halmashauri wilaya ya Kasulu |
| | | Halmashauri ya mji Kasulu |
| | | Halmashauri wilaya ya Kibondo |
| | | Halmashauri wilaya ya Kigoma |
| | | Manispaa ya Kigoma-Ujiji |
| | | Halmashauri wilaya ya Uvinza |
| 9 | Katavi | Halmashauri wilaya ya Mlele |
| | | Halmashauri wilaya ya Mpanda |
| | | Halmashauri ya mji Mpanda |
| 10 | Kagera | Halmashauri wilaya ya Biharamulo |
| | | Halmashauri wilaya ya Bukoba |
| | | Manispaa ya Bukoba |
| | | Halmashauri wilaya ya Karagwe |
| | | Halmashauri wilaya ya Kyerwa |
| | | Halmashauri wilaya ya Missenyi |
| | | Halmashauri wilaya ya Muleba |
| | | Halmashauri wilaya ya Ngara |
| 11 | Iringa | Halmashauri wilaya ya Iringa |
| | | Halmashauri wilaya ya ringa |
| | | Halmashauri wilaya ya Kilolo |
| | | Halmashauri ya mji |
| | | Halmashauri wilaya ya Mufindi |
| 12 | Geita | Halmashauri wilaya ya Bukombe |
| | | Halmashauri wilaya ya Chato |
| | | Halmashauri ya mji na wilaya Geita |
| | | Halmashauri wilaya ya Mbogwe |
| | | Halmashauri wilaya ya Nyang'hwale |
| | | Halmashauri wilaya ya Bukombe |
| 13 | Tanga | Halmashauri wilaya ya Handeni |
| | | Halmashauri ya mji Handeni |
| | | Halmashauri wilaya ya Kilindi |
| | | Halmashauri wilaya ya Korogwe |
| | | Halmashauri wilaya ya Lushoto |
| | | Halmashauri wilaya ya Muheza |
| | | Halmashauri wilaya ya Mkinga |
| 14 | Tabora | Halmashauri wilaya ya Igunga |
| | | Halmashauri wilaya ya Kaliua |
| | | Halmashauri wilaya ya Nzega |
| | | Halmashauri wilaya ya Sikonge |
| | | Manispaa ya Tabora |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri wilaya ya Urambo |
| | | Halmashauri wilaya ya Uyui |
| | | Halmashauri wilaya ya Igunga |
| 15 | Singida | Halmashauri wilaya ya Ikungi |
| | | Halmashauri wilaya ya Iramba |
| | | Halmashauri wilaya ya Manyoni |
| | | Halmashauri wilaya ya Mkalama |
| | | Halmashauri wilaya ya Singida |
| | | Manispaa ya Singida |
| 16 | Simiyu | Halmashauri wilaya ya Bariadi |
| | | Halmashauri wilaya ya Busega |
| | | Halmashauri wilaya ya Itilima |
| | | Halmashauri wilaya ya Maswa |
| | | Halmashauri wilaya ya Meatu |
| 17 | Shinyanga | Halmashauri wilaya ya Kahama |
| | | Halmashauri wilaya ya Kishapu |
| | | Halmashauri wilaya ya Shinyanga |
| | | Manispaa ya Shinyanga |
| | | Halmashauri ya mji Kahama |
| 18 | **Ruvuma** | Halmashauri wilaya ya Mbinga |
| | | Halmashauri wilaya ya Songea |
| | | Manispaa ya Songea |
| | | Halmashauri wilaya ya Tunduru |
| | | Halmashauri wilaya ya Namtumbo |
| | | Halmashauri wilaya ya Nyasa |
| 19 | Rukwa | Halmashauri wilaya ya Kalambo |
| | | Halmashauri wilaya ya Nkasi |
| | | Halmashauri wilaya ya Sumbawanga |
| | | Manispaa ya Sumbawanga |
| 20 | Pwani | Halmashauri wilaya ya Bagamoyo |
| | | Halmashauri wilaya ya Kibaha |
| | | Halmashauri ya mji Kibaha |
| | | Halmashauri wilaya ya Kisarawe |
| | | Halmashauri wilaya ya Mafia |
| | | Halmashauri wilaya ya Mkuranga |
| | | Halmashauri wilaya ya Rufiji |
| 21 | Njombe | Halmashauri wilaya ya Ludewa |
| | | Halmashauri ya mji Makambako |
| 22 | | Halmashauri wilaya ya Makete |
| | | Halmashauri wilaya ya Njombe |
| | | Halmashauri ya mji Njombe |
| | | Halmashauri wilaya ya Wanging'ombe |
| 23 | Mwanza | Manispaa ya Ilemela |

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri wilaya ya Kwimba |
| | | Halmashauri wilaya ya Magu |
| | | Halmashauri wilaya ya Misungwi |
| | | Manispaa ya Nyamagana |
| | | Halmashauri wilaya ya Sengerema |
| | | Halmashauri wilaya ya Ukerewe |
| 24 | Mtwara | Halmashauri wilaya ya Masasi |
| | | Halmashauri ya mji Masasi |
| | | Halmashauri wilaya ya Mtwara |
| | | Halmashauri wilaya ya Nanyumbu |
| | | Halmashauri wilaya ya Newala |
| | | Halmashauri wilaya ya Tandahimba |
| 25 | Morogoro | Halmashauri wilaya ya Gairo |
| | | Halmashauri wilaya ya Kilombero |
| | | Halmashauri wilaya ya Kilosa |
| | | Halmashauri wilaya ya Morogoro |
| | | Manispaa ya Mvomero |
| | | Halmashauri ya Ulanga |
| 26 | **Mjini Magharibi** | Magharibi |
| | | Mjini |
| 27 | **Kaskazini Unguja** | Kaskazini A |
| | | Kaskazini B |
| 28 | Mbeya | Halmashauri wilaya ya Busokelo |
| | | Halmashauri wilaya ya Chunya |
| | | Halmashauri wilaya ya Kyela |
| | | Halmashauri wilaya ya Mbarali |
| | | Halmashauri ya Jiji la Mbeya |
| | | Halmashauri wilaya ya Mbeya |
| 29 | Mara | Halmashauri wilaya ya Bunda |
| | | Halmashauri wilaya ya Butiama |
| | | Halmashauri wilaya ya Musoma |
| | | Manispaa ya Musoma |
| | | Halmashauri wilaya ya Rorya |
| | | Halmashauri wilaya ya Serengeti |
| | | Halmashauri wilaya ya Tarime |
| | | |
| 30 | Kaskazini Pemba | Micheweni |
| | | Wete |
| 31 | Kusini Pemba | Chake chake |
| | | Mkoani |
| | | |

## B; TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI